ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32 Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50. Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni

52.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

54.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

55. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

56.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

57.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

58. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

62.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

63.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

64.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

66.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

68.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

69.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

70.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

76.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

78.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tano – Tarehe 21 Juni, 2012

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani kuhusu taarifa ya Utekelezaji wa Haki za Watoto Zanzibar 2012. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Taarifa ya Utekezaji wa Haji za Watoto Zanzibar 2012. Naomba kuwasilisha .

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka mezani Hotuba ya Kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi, Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: (Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya wenyeviti wa kamati za Baraza lako tukufu, naomba kuwasilisha marekebisho yaliyofanywa na Kamati ya Wenyeviti kuhusu Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuendelea na mjadala wetu kama kawaida, na leo tumepata wageni kutoka maeneo mawili muhimu. Wageni wetu walioko katika ukumbi wa juu kwenye ukumbi wa wageni ni wageni kutoka Baraza la Habari Tanzania (MCT). Nawaomba wote kwa pamoja wasimame. (*Makofi*).

Ahsante sana wageni wetu ambao hao walikuwa wanachanganya pamoja na Ndugu yetu Kajubi Mukanyanga – huyu ni Katibu Mtendaji, mwengine ni Ndg. Ziada Kilobo – Meneja Raslimali Watu na Uratibu, mwengine ni Ndg. John Miremi – huyu ni Meneja Machapisho na Utafiti na mwengine ni Suleiman Seif Omar – Meneja wa MCT ofisi ya Zanzibar.

Naona kuna watano pale, na huku kuna wanne na huyo mwengine ambaye sikumtaja naye naomba ajitambulishe kwa kusimama ni yule pale, karibuni sana.

Wageni wengine ni wawakilishi wa watoto kutoka Mabaraza ya Watoto Unguja na Pemba. Nawaomba na wao kwa pamoja wasimame.

Waheshimiwa Wajumbe mutakumbuka kwamba kuna utaratibu wa vijana wetu kutoka skuli mbali mbali wanafanya vitu vya aina hii, wana *youth parliament*. Sasa na hawa ni watoto wana Baraza lao la Watoto, ndani mule pengine muna spika na wajumbe wengine. Na mambo haya yanakuwemo katika skuli mbali mbali za msingi na hasa sekondari.

Vijana ahsanteni sana na karibuni sana.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 136

Changamoto Zinazolikabili Jeshi la Polisi Zanzibar

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa – Aliuliza**:-**

Jeshi la Polisi ni taasisi ya Muungano ambayo inafanya kazi zake Tanzania Bara na Zanzibar. Hata hivyo, kwa muda mrefu wananchi wamekuwa wakilalamikia utendaji wa jeshi hilo hasa wanapokwenda vituoni kupeleka malalamiko yao, ambapo mara nyingi jeshi hilo hudai gari, mafuta ya kufuatilia matukio ya uhalifu au upungufu wa askari.

(a) Kwa vile bajeti ya Jeshi hilo huwa inapitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Je bajeti hiyo hailihusu jeshi hilo kwa upande wa Zanzibar. Kama wanapewa ni kiasi gani cha fedha wameidhinishiwa kwa mwaka 2011/2012.

(b) Je, ni lini Jeshi hilo litazifanyia matengenezo nyumba zao chakavu ambazo hazilingani na hadhi yao.

(c) Uanzishwaji wa Polisi jamii umesaidia sana ulinzi katika mitaa. Je, kuna mpango wowote wa utoaji wa motisha kwa askari jamii wa Shehia ambayo itafanya vizuri zaidi.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri alikuwa anatafakari mambo mazito na Mwanasheria Mkuu. Karibu sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais – Alijibu**:-**

Mhe. Spika**,** ahsante sana kwanza nikushukuru kwa kunielezea yaliyomo ndani ya moyo wangu, lakini pia nichukue nafasi hii kuwapongeza ndugu zetu waliokuja kututembelea kwa Baraza la Habari Tanzania, pamoja na Baraza la Watoto ambalo lina wawakilishi wao katika Baraza hili tukufu. Naamini ni mwanzo mzuri, ninawapongeza sana kwa kuja kwao.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 136 lenye vifungu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli bajeti ya Jeshi la Polisi inapitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bajeti hiyo pia inajumuisha bajeti ya Jeshi hilo kwa upande wa Zanzibar. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 Jeshi hilo kwa upande wa Zanzibar limeidhinishiwa matumizi ya jumla Tshs 11,517,289.800/-.

(b) Mhe. Spika**,** nyumba za polisi zilizopo Zanzibar hufanyiwa matengenezo kila mwaka wa fedha kulingana na fedha zilizopangiwa katika Bajeti.

(c) Mhe. Spika, ni kweli sera ya Polisi Jamii imeleta mafanikio makubwa sana katika kupunguza uhalifu na kuleta utulivu ndani ya jamii ya Wazanzibari. Jeshi la Polisi likishirikiana na wadau wengine linaendelea kutoa michango yake ya hali na mali kwa maeneo yote yanayofanya vizuri. Aidha Jeshi hili pia hutoa mchango wake hata kwa yale maeneo ambayo hayajafanya vizuri ili kuleta ustawi kwa jamii katika maeneo yote ya nchi yetu.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize kama hivi ifuatavyo.

(a) Kuhusu majengo mengi ya vituo vya Polisi ni ya muda mrefu na bahati mwaka 2002 walijengewa nyumba Polisi sehemu ya Mfikiwa Pemba, tukaambiwa ni awamu ya kwanza, lakini hivi sasa ni miaka kumi imeshapita hatujaona awamu ya pili imejengwa wapi. Jee, hili mheshimiwa analizungumzaje.

(b) Hivi sasa Polisi wengi waliomo kwenye vituo wameshakaa muda mrefu na wamezoeleka na raia, kwa hivyo kazi haifanyi vizuri. Jee, na hili anasemaje Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, kuhusu uchakavu wa nyumba za Polisi ni askari hao wengi wanaishi uraiani jambo ambalo ni kinyume na desturi na mila za Polisi. Wanatakiwa askari wetu hawa waweze kuishi katika kambi zao maalum.

Lakini kutokana na uwezo wa kifedha wa nchi yetu ndio ambao umesababisha operesheni hii ya ujenzi wa nyumba za Polisi kuweza kuenea katika maeneo yote kwa wakati unatakiwa umekuwa mgumu.

Ni kweli Polisi wamekuwa na mkakati na mipango ya kujenga nyumba za Polisi kwa nchi nzima, na walianzia kwa upande wa Zanzibar kule Mfikiwa Pemba. Lakini kutokana na ufinyu wa bajeti ndio wanakwenda kidogo kidogo lakini kadri ya fedha zitakavyopatikana ndipo watakapoweza kuendelea na shughuli hiyo ya ujenzi wa nyumba zao.

Kuhusu kubadilishwa kwa askari wanaokaa katika vituo. Mhe. Spika, katika maboresho ya Polisi huo ni mpango wao na tatizo ni hilo hilo kutokana na upungufu wa fedha katika kutekeleza suala hili la kubadilisha askari wasikae kituo kimoja kwa muda mrefu ndio wanalopata sana, lakini nia ni kufanya mabadiliko kadri ya uwezo wa fedha utakavyoruhusu, ili askari asiweze kukaa muda pahali pamoja na akaweza kuzoeleka na hivyo inamnyima fursa ya kufanya wajibu wake vizuri kama inavyotakiwa katika Jeshi la Polisi.

Mhe. Nassor Ali Salim: Ahsante sana Mhe. Spika**,** na mimi kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe. Waziri amekiri kwamba Polisi jamii imesaidia katika kupunguza uhalifu katika nchi yetu. Jee, haoni ipo haja kuwapatia sare maalum Polisi Jamii wale ili kuweza kuwatambua na kutekeleza kazi zao kwa urahisi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Polisi Jamii kwa ufupi ni wananchi wanaofunzwa utaratibu mzuri wa kulinda maeneo yao wanayoishi. Kwa hivyo ushauri huu wa Mhe. Mwakilishi kidogo naona haulingani na mwelekeo ulivyo, kwa sababu ni wananchi wenyewe wanaolinda maeneo yao. Tusije tukawapa sare matokeo yake wakadhani sasa wao ni Polisi kamili na wakafanya mambo kinyume na utaratibu za nchi na sheria zilizopo.

Lakini wacha tulichukue hili wazo tuwashauri Jeshi la Polisi tuone watasemaje kwenye wazo hili.

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata fursa hii kuuliza swali moja la nyongeza.

Nilikuwa ninataka kufahamu tu ni sababu zipi zilizopelekea kituo kidogo cha Mangapwani kufungwa kwa muda mrefu hadi hivi sasa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kilichopelekea kufungwa kituo kidogo cha Mangapwani ni suala zima kama nilivyolieleza awali la ukosefu wa fedha kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo ya kutosha ili kiwe kituo chenye hadhi kinachoweza kufanya shughuli zake za Kipolisi.

Lakini mawazo yako nitachukua, nitawasiliana na Kamishna wa Polisi tuone namna gani jambo hili linaweza kurekebishwa.

Na. 17

Wanafunzi wa Vyuo vya Mafunzo

Mhe. Mohamed Haji Khalid – Aliuliza**:-**

Kuna malalamiko ya wanafunzi wa Vyuo vya Mafunzo Pemba kwamba, wenzao wa Unguja wanapata milo mitatu (3) wakati wao wanapata mlo mmoja tu.

(a) Je, Mhe. Waziri ni sababu zipi zinazopelekea kuwepo kwa tofauti hii wakati taarifa za Ofisi ya Rais – MBLM iliyowasilishwa mbele ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, mwishoni mwa Disemba 2011, iliainisha kwamba wanafunzi wote wa Vyuo hivyo wanapata mlo mara tatu (3).

(b) Je, hatua gani zinachukuliwa kurekebisha hali hii.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu**:-**

Mhe. Spika**,** kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 17 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa nia safi tu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzia mwaka jana iliamua kurejesha mlo wa tatu kwa wanafunzi waliopo katika Chuo cha Mafunzo katika kambi zote walimofungwa. Sasa katika utekekezaji wake kweli hatukwenda sambamba mote kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Kwa kweli mwaka jana ilikuwa hakuna bajeti iliyoongezwa kwa mlo wa tatu kote Unguja na Pemba, sio Unguja tu.

Yaani utekelezaji wake ulifanywa lakini kwa kusuasua kote Unguja na Pemba lakini Pemba ilichelewa. Kwa hivyo Mhe. Spika, ilibidi wizara ifanye mipango yake wenyewe ya kutafuta fedha, na juhudi nyengine za kuzalisha chakula kutoka katika mashamba yake yote ya Chuo cha Mafunzo.

Jibu la pili naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwa mwaka huu wa fedha tayari mambo yamekaa sawa tumeongezewa bajeti ya chakula kutoka shilingi milioni mia nne hadi shilingi milioni mia sita ili kuziba lile pengo la mlo wa tatu. Kwa hivyo tunamuhakikishia kwamba mwaka huu wa fedha jambo hili litakaa sawa kote Unguja mpaka Pemba.

Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali hili la nyongeza.

Mhe. Spika, ninamshukuru sana Mhe. Waziri kutokana na taarifa yake nzuri ambayo ni ya uhakika milo ni mitatu katika maeneo ambayo wafungwa wanaendelea na shughuli. Lakini kadri ya watu wanavyokula vizuri vile vile watakuwa wanahitaji kwenda haja vile vile. Jee sehemu hii ya kwenda kujisaidia katika haja kubwa na ndogo zipo katika utaratibu gani kwenye maeneo yao.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Ninakubaliana na yeye kwamba ni kweli kuwa baada ya binadamu kupata lishe nzuri, basi anahitaji ki-*biologically* lazima kidogo kwenda uwani. Ninafikiri nimeshaeleza mara nyingi kwamba tupo katika juhudi za kuziendeleza kambi zote za Chuo cha Mafunzo kuondokana na ule utaratibu wa zamani wa mtondoo. Sasa tumeshaanza kila panapo marekebisho yanafanyika kutiliwa vyoo vya kisasa, ili kutimiza lile lengo la haki za binadamu.

Mhe. Rufai Said Rufai: Ahsante sana Mhe. Spika, nishukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Vyuo hivi vya Mafunzo vinazalisha mpunga, muhogo, viazi vitamu na kadhalika.

Ni kipi kinachopelekea kwa muda huo kukosa kwa milo hii mitatu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Ninakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli kambi zetu zinajitahidi sana kuzalisha mpunga na muhogo kwa wingi sana, tena ukija kwa upande wa muhogo wanayo ile mihogo mifupi, yaani ya muda mfupi na mrefu, yaani wanajiwekea wenyewe akiba.

Kama nilivyosema kwa kweli kwa mwaka jana kwa uamuzi wetu wa serikali ilikuwa hakuna fedha za ziada, kwa hivyo kilichookoa kwa kweli ndio hayo mazao katika mashamba yetu.

Kwa kweli wanajitahidi kuzalisha na niseme nusu ya chakula basi kinatoka kwenye mashamba yao.

Na. 79

Tatizo la Ajira kwa Vijana Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza**:-**

Zanzibar inakabiliwa na tatizo kubwa la ajira na waathirika wakubwa ni vijana, kwani Serikali inaendelea kutoa ajira za kazi kwa mikataba kwa watu ambao wameshastaafu na kulipwa mafao yao.

(a) Kwa nini Serikali isipige marufuku utaratibu wa utoaji wa ajira hizo, ili kuwasaidia vijana na kundi la wasomi ambao wamegeuka wapiga soga kutokana na ukosefu wa kazi.

(b) Serikali inatekeleza vipi kauli ya kuwa, "vijana ndio nguvu kazi ya Taifa".

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu**:-**

Mhe. Spika**,** kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 79 kama ifuatavyo:-

Kwanza nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kwamba Zanzibar inakabiliwa na tatizo kubwa la ajira na waathirika wakubwa wa tatizo hili ni vijana. Serikali inaelewa hali hii na kwamba hatua kadhaa zimeanza kuchukuliwa na Wizara mbali mbali ili kulitafutia ufumbuzi tatizo hili.

Mhe. Spika**,** baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe, Mwakilishi suali lake lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Nambari 2 ya mwaka 2011, imeondosha utaratibu wa ajira za mikataba kwa waajiriwa wa Utumishi wa Umma waliofikia umri wa kustaafu kazi kwa lazima, isipokuwa kwa nafasi ambazo zinahitaji utaalamu, ujuzi na uzoefu maalum na ambazo zitatangazwa rasmi katika Gazeti Rasmi la Serikali na Mhe. Waziri anayeshughulikia masuala ya Utumishi wa Umma.

(b) Serikali imetekeleza kauli ya "Vijana ndio nguvu kazi ya Taifa" kwa kufuata maelekezo ya kifungu cha 57 (1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma nambari 2 ya mwaka 2011, kwamba kila Taasisi ya Utumishi wa Umma ina uwezo wa kuajiri idadi ya watumishi kwa mwaka wa fedha kulingana na mpango wa raslimali watu wa taasisi husika, kwa taarifa ya Mhe. Mwakilishi kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, Serikali imetenga jumla ya nafasi mpya 2552 kwa ajili ya kuwapatia vijana ajira ambao ndio nguvu kazi ya taifa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri tu. Nitakuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mhe. Waziri mpaka sasa watumishi wangapi waliofika umri wa kustaafu na ukawapa muda wa nyongeza kwa mkataba, na fani zipi ambapo pana vijana wetu wasingeweza kuziba mapengo hayo. Jee utakuwa tayari kuleta vijana wenye sifa hizo kuwaajiri.
Pili kumekuwa na upungufu wa wafanya kazi wenye sifa za kitaalamu wasomaji wa X-Ray, ardhi na wengineo. Ikiwa wewe ndiye waziri mwenye dhamana, jee unawaambia nini wananchi ili kuokoa maisha yao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Ni wafanya kazi 25 ambao walikuwa wastaafu kwa hiyari ndio waliongezewa ya mkataba wa ajira na wafanya kazi 5 waliokuwa wastaafu kwa lazima ndio waliopewa mkataba wa ajira ya mkataba.

Na wafanyakazi hao waliokuwa wastaafu kwa lazima wameajiriwa katika Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA) wafanyakazi wawili, Wizara ya Afya wafanyakazi wawili; mmoja ameajiriwa Hospitali ya Kivunge na mmoja Chuo cha Afya na mfanyakazi mmoja ameajiriwa Ofisi ya Rais Ikulu kwa maana ya mwandishi wa hotuba za Mhe. Rais.

Wizara yangu imejiandaaje katika kuwaajiri wataalamu vijana? Katika kulifanikisha suala hilo ninapenda niliarifu Baraza lako tukufu kwamba ndio mwaka jana nilikuja na mpango wa *suspension plan*, lakini vile

niliahidi kwamba nitaanzisha *human resources data base*. Na hiyo human resources database inategemea kuwepo kwa *human resources capacity assesement*.

Hayo mambo baada ya kutengenea ndio yatakayoweza kutuwezesha kujua ni wataalamu wangapi tulionao katika fani gani, wakati huo huo tutakuwa tuna mpango wa kuandaa *training policy*, ili kujua mahitaji halisi ya wale tunaowasomesha.

Kwa hivyo wizara yangu imefanya juhudi kubwa katika kukabiliana na changamoto hii. Lakini pia hivi sasa tunachofanya ni kuhakikisha katika hizo nafasi 2552, sio tu suala la kuajiri lakini tunaangalia mahitaji yaliopo katika taasisi na wataalamu tulionao ili tuweze kuwaajiri.

Hivyo ni kusema kwamba katika mwaka huu kama nilivyosema kwenye swali langu mama kwamba, tutaajiri watumishi 2552 kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya taasisi za umma na wananchi yaliopo.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, ninashukuru kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza.

Katika sifa za kuajiri mara nyingi kuna kipengele cha kuwa na uzoefu wa kufanya kazi katika muda fulani, sifa ambayo huwakosesha fursa vijana wengi ambao wamemaliza vyuo mbali mbali katika maskuli. Kama ni hivyo Mhe. Waziri huoni kwamba wakati umefika wa kuondosha sifa hii katika uajiri ili kuwapa fursa vijana wanaomaliza skuli na kuajiriwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, nakubaliana naye kwamba kuna baadhi ya nafasi za kuwaajiri watumishi katika sekta ya umma zinahitaji uzoefu. Lakini nafasi hizo mara nyingi sana huzingatia uhamisho na sio uajiri. Kwa zile nafasi ambazo zinaajiriwa, nafasi mpya tabaan huwa hazizingatii sana masuala ya uzoefu. Suala la uzoefu linakuja pale inapotokea kwamba kuna nafasi ambayo inaonekana ndani ya serikali hakuna mtaalamu yule, lakini kwa nafasi za kawaida zinahitaji elimu zaidi ya mtu kuliko suala la uzoefu.

Kwa maana hiyo nakubaliana naye pia kadri tutakavyokuwa tunakwenda, kama nilivyosema jana kwamba suala la utumishi kwa Zanzibar ni *reform* na kwa sababu tuko kwenye *reform,* kwa hivyo tutakuwa tunakwenda hatua kwa hatua, pale tukifikia pahala kwamba hatuhitaji uzoefu tunahitaji ujuzi tu basi bila shaka Baraza lako hili tukufu litaelewa mipango hiyo na tutaweza kulifanyia kazi kama Mhe. Mwakilishi alivyolishauri.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ili nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi la Mhe. Jaku, alikubaliana naye kwamba kuna tatizo kubwa la ajira hapa Zanzibar na akaeleza kwamba wizara mbali mbali zinaandaa mikakati katika kukabiliana na tatizo hili.

Mhe. Spika, mimi nilitaka kujua wizara yake ambayo inahusika na utumishi, ina mikakati gani katika kuondosha tatizo hili.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, wizara yangu mikakati iliyonayo kwanza tumetambua vijana ambao wana sifa za kuajiriwa katika maeneo mbali mbali, kuanzia chini ya kidato cha nne mpaka *PhD level*. Hao wako karibu vijana zaidi ya 4,000. kwa mwaka huu katika mpango wetu wa ajira kwenye sekta ya umma ndio maana tumetenga hizi nafasi 2,552, huo ndio mkakati mkubwa ambao tunao.

Mhe. Spika, mkakati mwengine ni wa serikali nzima kwa jumla, kwa sababu hawa vijana sio tu wanaweza wakaajiriwa katika sekta ya umma, lakini kuna sekta binafsi ambazo zitaajiri vijana wengine ambao wana tatizo hili la ajira. Kila waziri atakayekuja hapa ambaye anahusika na masuala ya ajira kwa vijana, basi atakuja na mpango au mkakati wake wa kuweza kusema yeye kwa wizara yake katika mwaka huu wa bajeti ataajiri vijana wangapi. Lakini kwa upande wa serikali mkakati tulionao ni huo. Tumeangalia hali halisi ya wingi wa vijana tulionao na tukasema basi kwa mwaka huu angalau tuajiri vijana 2,552.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaendelea na shughuli inayofuata baada ya hapa, nataka tufanye marekebisho kidogo ya hii *order paper* yetu. *Item* ya tatu ya shughuli zetu ina kichwa cha maneno kinachosema ‘kauli za mawaziri’. Tutakumbuka kwamba katika marekebisho ya kanuni tuliyofanya kitu hiki tumekiondoa kwa mujibu wa kifungu cha 43 cha kanuni zetu toleo la mwaka huu, badala ya kuita kauli za mawaziri, sasa ni kauli za serikali.

Hii tuliifanya kwa makusudi kwa sababu tulipokuwa tunazungumzia kauli za mawaziri, ilikuwa ina *limit* kwamba sasa Makamu wa Pili wa Rais, anapotaka kutoa kauli ya serikali itaangukia wapi ambayo haimo katika mtiririko wa shughuli za Baraza. Bila shaka mawaziri wanafanyakazi ya serikali, ndio tukaona basi tugeuze kauli za mawaziri iwe ni kauli za serikali, kwa utaratibu ule ule kwamba kauli hizi zikiwasilishwa hapa itakuwa hakuna majadiliano, isipokuwa kwa idhini ya Spika na kwa sababu ya muda kama utakuwepo, basi maswali yanaweza yakaulizwa juu ya kauli hizo. Kwa hivyo, marekebisho ya kufanywa ni kwamba badala ya kusema kauli za mawaziri, iwe kauli za serikali kwa mujibu wa ibara ya 43 ya kanuni zetu. Tunaendelea.

KAULI ZA SERIKALI

Taarifa ya Utekelezaji wa Haki za Watoto Katika Kilele cha Siku ya Mtoto wa Afrika, Tarehe 16 Juni, 2012

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa tukiwa wazima. Pia napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipatia nafasi hii muhimu na adhimu.

Mhe. Spika, naomba sasa kuwasilisha taarifa ya maadhimisho ya siku ya Mtoto wa Afrika, tarehe 16 Juni, 2012, ni siku ya Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika ambapo maadhimisho hayo yanafanyika katika nchi zote wanachama wa umoja wa Afrika kwa namna tofauti.

Mhe. Spika, wakati wa maadhimisho haya tunakuwa tunawakumbuka watoto waliouwawa kikatili mjini Soweto Afrika ya Kusini, mwaka 1976, wakipinga ubaguzi na utumiaji wa lugha za Kikaburu maskulini.

Mhe. Spika, siku hii inatoa fursa kwetu kupima utekelezaji haki za watoto na kupendekeza hatua madhubuti za kuchukuliwa kwa nia ya kuimarisha huduma zinazowalenga watoto pamoja na watendaji. Pia inatupa msukumo wa kuzidisha mashirikiano baina ya wazazi, walezi, sekta zinazohudumia mama na mtoto pamoja na wadau wa maendeleo kwa kusimamia na kuitekeleza sheria ya mtoto ya mwaka 2011

Mhe. Spika, kwa kutekeleza hili Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, ikiwa ni mratibu na msimamizi wa shughuli za maendeleo ya watoto Zanzibar, imeandaa utaratibu wa kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu, taarifa ya utekelezaji wa haki za mtoto ifikapo tarehe 16 Juni, ya kila mwaka.

Mhe. Spika, taarifa hii inajumuisha sekta zote za serikali na zisizo za kiserikali, zinazoshughulikia masuala ya watoto kulingana na mikataba, sera na kuzingatia mpango wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini Zanzibar, MKUZA II 2010 hadi 2015.

Mhe. Spika, Dira 2020 na Malengo ya *Millennium*. Utaratibu huu pia ni moja ya shughuli za wizara kuratibu na kutathmini utekelezaji wa haki za watoto kisekta na watoa huduma kwa maendeleo ya mama na mtoto Zanzibar.

Mhe. Spika, ujumbe wa mwaka huu wa 2012 haki za watoto wenye ulemavu ni jukumu letu kuzilinda, kuziheshimu, kuziendeleza na kuzitekeleza. Ujumbe huu umetolewa na kamati ya wataalamu wa haki na ustawi wa mtoto ya Umoja wa Afrika, baada ya kuonekana kuwa pamoja na hatua nyingi nzuri zinazochukuliwa na serikali na taasisi zote zinazotoa huduma kwa watoto wenye ulemavu. Lakini bado kuna mapungufu mengi yanaonekana kwa kutotendewa haki watoto, hasa wenye ulemavu kutokana na kukosekana kwa mazingira mazuri na jamii kuonekana.

Mhe. Spika, katika maadhimisho haya pamoja na taarifa hii, zipo shughuli nyengine ambazo zinafanyika kupitia vipindi vya televisheni, semina na maadhimisho kwa watoto wenye ulemavu kwa mashindano ya uchoraji picha na kadhalika.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa kauli mbiu ya mwaka huu wa 2012, malengo makuu ya nchi za Afrika yaliyotolewa na Umoja wa Afrika ni kama ifuatavyo.

- Kuinua uelewa juu ya haki za watoto wenye ulemavu, uwezo wao na uwezekano wa kutambua hali halisi ya kwamba wao ndio waliokatika hali hatarishi.
- Kusaidia ufahamu juu ya vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa mikataba ya kikanda.
- Kuchukua juhudi za makusudi kuzipitia sheria na sera za nchi ngazi ya kitaifa ili ziweze kuzingatia mahitaji ya watoto wenye ulemavu na kuona kwamba hawabaguliwi.

- Kutetea kwa njia ya kauli mbiu shawishi kuitaka serikali na taasisi binafsi kuwa mstari wa mbele kuelimisha haki za watoto wenye ulemavu, kwa kuchagua maeneo ya kuyafanyia kazi na kusimamia utekelezaji wake.
- Kuchukua hadhari kwa kupanga mikakati ya kukinga ulemavu wa watoto usitokee kwa uzembe.

Mhe. Spika, utekelezaji wa ustawi wa watoto unajumuisha watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi, uhifadhi wa mtoto huduma kwa familia na watoto wanaolelewa na wazazi wasiojiweza, huduma za malezi kwa watoto wanaoishi katika nyumba ya watoto mzizini na vituo vya kulelea watoto vya binafsi.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya Wizara ya Afya imechukua hatua nyingi katika kuhakikisha afya za mama na watoto zinalindwa, na kuwa bora kwa kuanzisha utaratibu wa kukusanya na kutoa taarifa za afya pamoja na upatikanaji wa takwimu sahihi, kuanzia ngazi za wilaya, kanda hadi taifa. Utaratibu huu unasaidia sana kutoa maamuzi katika ngazi zote.

Mhe. Spika, ripoti ya utafiti wa hali ya mama na mtoto Zanzibar, uliofanywa kwa mashirikiano baina ya Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto na UNICEF, imeonesha maeneo ya kuchukuliwa hatua za haraka ili watoto waweze kuishi, kulindwa, kuendelezwa na kupewa fursa za kushiriki katika mambo yanayowahusu, ambapo kuyatekeleza haya yanahitaji kutengewa rasilimali ya kutosha. Kwa hivyo, taarifa hii inalenga maeneo manne ya utekelezaji wa haki za msingi kwa watoto Zanzibar.

- haki ya kuishi
- haki ya kuendelezwa
- haki ya kulindwa na
- haki ya kushirikishwa

Mhe. Spika, nikianza na haki ya kuishi. Wizara ya Afya inatekeleza malengo yake ya kuzuwia na kupunguza idadi ya vifo vya watoto walio chini ya miaka 5, kwa kuzingatia mikakati ya kinga na tiba chini ya mpango shirikishi wa mama na mtoto, wa kudhibiti maradhi ya kuharisha na magonjwa ya watoto. Mpango huu unatekelezwa katika wilaya zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia idadi ya vizazi na vifo katika kipindi cha mwaka 2011/2012, kitengo cha afya ya uzazi kimewapatia mafunzo wafanyakazi 40. Wafanyakazi 20 Unguja na wafanyakazi 20 Pemba, namna ya kuwahudumia watoto wachanga wanapozaliwa, ili waweze kutambua na kushughulikia matatizo ipasavyo pindi yanapotokea. Wafanyakazi 25 wa afya wamepatiwa mafunzo ya kuwahudumia watoto chini ya umri miaka 5. Ufuatiliaji wa wafanyakazi wa afya wa vituo vya Wilaya ya Kaskazini A na B, pamoja na Wila ya Kati na Kusini ulifanyika kwa nia ya kuona maendeleo kwa mafunzo waliopatiwa.

Mhe. Spika, huduma za chanjo kwa mama na watoto wachanga dhidi ya magonjwa tisa yanayozuilika kwa chanjo zilitolewa kwa Unguja na Pemba. Magonjwa hayo ni pamoja na kifua kikuu, donda koo, kifaduro, pepopunda, homa ya ini, homa ya uti wa mgongo, kichomi yaani polio, kupooza na surua.

Kwa mwaka 2011/2012 lengo la kuchanja lilikuwa ni asilimia 90 kwa chanjo zote. Lengo hili lilivukwa kwa chanjo zote isipokuwa chanjo ya pepopunda.

Mhe. Spika, ibara ya saba, mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu, unatilia mkazo nchi zilizoridhia mkataba huo, zichukuwe hatua zote za lazima ili kuhakikisha kwamba watoto wenye ulemavu wanapatiwa na wanafurahia kikamilifu haki zote za binadamu, na za msingi wa uhuru kwa usawa kama watoto wengine katika jamii. Maeneo yetu mengi ya majengo, barabara, vyombo vya usafiri, kumbi za burudani na televisheni bado haziko rafiki na watu wenye ulemavu na kusababisha usumbufu mkubwa wa kupata huduma hizo. Sheria zipo wazi hivyo ni vizuri basi zikawekewa mkazo ili kuwaondoshea usumbufu watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, kwa kulizingatia hilo idara ya watu wenye ulemavu iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, inaratibu masuala ya watu wenye ulemavu kwa kupitia Baraza la Taifa la watu wenye ulemavu, kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, Umoja wa Watu wenye Ulemavu ambao umewaunganisha watu wenye ulemavu kulingana na Jumuiya zao, wote hao wanafanyakazi ya kutetea ili kuona haki na fursa sawa zinapatikana katika jamii. Ni lazima kuwaunga mkono ili tupate mafanikio.

Mhe. Spika, katika haki ya kuishi ni ile hali ya lazima ambapo mtoto mwenye ulemavu anahitaji chakula, malazi, mavazi, elimu, afya bora na ulinzi. Suala hili linagusa zaidi lishe ya mtoto, maji safi na salama, kinga dhidi ya maradhi na chanjo ambazo endapo zitakosekana basi inaweza kusababisha ulemavu na adhari nyengine kwa afya ya mtoto.

Mhe. Spika, nasikitika sana kusema kwamba changamoto kubwa iliopo mbele yetu ni kwamba bado baadhi ya watoto wenye ulemavu, wanakosa matunzo mazuri na lishe bora na kusumbuliwa na maradhi yatokanayo na lishe. Hiyo hutokana na hali duni inayowakabili familia kimazingira na mapato ya kujikimu kimaisha na kukosa misaada. Kwa hivyo, ipo haja kwa jamii kulielewa vizuri suala hili na kuliwekea mikakati itakayosaidia kulipunguza na kuliondoa kabisa, jambo hili linahitaji ushirikiano wa pamoja, baina ya serikali na wananchi kwa jumla.

Mhe. Spika, elimu ya afya kwa jamii ni muhimu sana iendelee kutolewa kwa kushirikiana na taasisi za serikali na zisizo za kiserikali, ili elimu hiyo ifike kwa walengwa. Vikundi vya kinamama na familia zenye watoto wenye ulemavu na walezi ili wanufaike na kuitumia elimu hiyo kwa faida yao na taifa.

Mhe. Spika, Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo, ni moja kati ya wadau ambao shughuli zake ni kusajili, kutunza kumbukumbu na utoaji wa takwimu sahihi.

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inajukumu maghususi la kutoa elimu kwa watoto wote nchini, katika kuhakikisha watoto wanapata elimu kuanzia maandalizi, msingi hadi sekondari. Wizara pia imeimarisha vituo vya kujiendeleza, kuwaendeleza watoto waliomaliza sekondari ya awali na wale wanaoacha masomo kwa sababu ya mazingira mbali mbali. Uimarishaji mazingira ya utoaji elimu kwa kuwashirikisha watoto kujifunza uongozi, kuwapatia ushauri nasaha na kuwa karibu na walimu kwa kupitia serikali za wanafunzi maskulini, kunasaidia kujenga msingi wa maelewano baina ya walimu na wanafunzi wao.

Mhe. Spika, mradi wa elimu ya msingi *Tanzania 21 Century Basic Education Program*, uliozinduliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tarehe 28 February, 2012, ni mradi muhimu sana kwa kukuza vipaji vya watoto, hasa katika masomo ya sayansi. Mradi huu una lengo la kuimarisha ubora wa elimu ya msingi, katika kujua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano, kutaleta mabadiliko makubwa ya elimu nchini.

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imeweka kitengo cha elimu mjumuisho, watoto wenye ulemavu wana haki sawa ya kupata elimu. Sera ya elimu ya mwaka 2006 ina lenga kuhakikisha haki na fursa sawa za kielimu, zinatolewa kwa watoto wote, wakiwemo wenye ulemavu kwa misingi sawa na ile itolewayo kwa Wazanzibari wote. Lakini bado inaonesha idadi ya watoto wenye ulemavu kwenye maskuli ni ndogo, hii inatokana na mwamko mdogo wa wananchi wetu. Kwa hivyo, ipo haja kubwa ya kufanya kampeni na kuwaelimisha wananchi, hasa wale wenye kuwalea na kuwatunza watoto wenye ulemavu kwamba wawapeleke watoto wao skuli ili wapate elimu ambayo ni haki yao kama watoto wengine.

Mhe. Spika, sekta ya habari ni moja kati ya sekta muhimu sana zenye mahusiano makubwa na maisha ya mtoto. Kwa kulizingatia hilo, Shirika la Utangazaji la Zanzibar, yaani ZBC ikijumuisha redio na televisheni, limekuwa mstari wa mbele kutimiza wajibu wao wa kuelimisha jamii kuhusu haki, fursa na wajibu wa mtoto kupitia programu zao. hivyo, katika suala hili la kuwapatia haki na fursa sawa watu wenye ulemavu hasa watoto, vyombo hivyo vina wajibu mkubwa na nafasi ya kuongeza kasi ya kuwaelimisha wananchi. Taasisi za serikali na zisizo za kiserikali juu ya kutambua umuhimu wa kuwasaidia watoto wenye ulemavu.

Mhe. Spika, hapa Zanzibar hadi sasa kuna mabaraza ya watoto yapatayo 163, katika ngazi za shehia. Uundaji wa mabaraza hayo umetokana na mchango mkubwa unaotolewa na Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, kupitia idara yake ya maendeleo ya wanawake na watoto kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Hifadhi ya Watoto, yaani *Save the Children*.

Mhe. Spika, mpango wa uundaji wa mabaraza ya watoto Zanzibar, unakwenda sambamba na ule wa utoaji mafunzo kwa mabaraza hayo, wenye lengo la kuwapa watoto uelewa juu ya mambo ya msingi juu ya maisha yao, ikiwa ni pamoja na kutambua haki na wajibu wao katika maisha yao ya kila siku.

Aidha, mafunzo hayo yanalenga kuwapa watoto mwamko, juu ya kuwepo kwa vitendo vya udhalilishaji vinavyofanywa dhidi yao, na kuwajengea uwezo wa kujikinga na kukabiliana na vitendo hivyo.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya juhudi kubwa katika kuhakikisha malengo ya MKUZA II na malengo ya *Millennium*, yanatekelezwa na kuzingatia haki na ustawi wa mtoto, chini ya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Imepanga kutekeleza mikakati madhubuti iliyowezesha kutenga asilimia 34.5 ya bajeti ya serikali kwa huduma za watoto kwa kupitia sekta ya elimu, afya, maji safi na salama.

Mhe. Spika, mpango wa uhai, hifadhi, maendeleo ya mama na mtoto ni programu inayoratibiwa na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, chini ya idara ya maendeleo ya watenda kazi. Mpango huu unatekelezwa katika ngazi zote za shehia na wilaya za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, mashirikiano katika utekelezaji wa programu hii ni muhimu sana ili kufanikisha utekelezaji wa masuala ya mtoto kwa kujenga misingi mizuri.

Mhe. Spika, kwa kumaliza taarifa hii, naomba kuikumbusha jamii, watendaji na viongozi, kuwa sote tuna wajibu wa kusimamia watoto wetu wa Zanzibar, na kukemea yale yote yanayowadhalilisha watoto na kuwakosesha haki na ustawi wao.

Mhe. Spika, baada ya kutoa taarifa hii naomba kuchukua tena fursa hii, kutoa shukrani za dhati kwa uongozi wa Wizara ya Nchi Ofisi Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Jeshi la Polisi, Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, pamoja na wadau wa maendeleo, Shirika linalohudumia watoto, yaani UNICEF, Save the Children, FHI, EFAFASA, Shirika la Korea kwa ushirikiano na utekelezaji wa haki za mtoto.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri kwa kuwasilisha taarifa hiyo ya utekelezaji wa haki ya watoto, ambayo kilele chake ilikuwa kimefikia tarehe 16 mwezi huu wa Juni, 2012. Lakini Waheshimiwa Wajumbe, mtakumbuka kwamba haikuwezekana kuipata tarehe hiyo kwa sababu kipindi hicho tulikuwa tuko kwenye mapumziko madogo ya kujikita kupitia bajeti kwa undani zaidi, na hapakuwa na kikao hapo katikati. Vinginevyo ilitegemewa tarehe hii 16 ingekuwa kuna kikao basi tungeweza kufanya hivyo.

Waheshimiwa Wajumbe, kanuni chini ya ibara ya 43 inatuelekeza tusiwe na mjadala, isipokuwa kwa idhini ya Spika, tuweze kuuliza maswali. Tulijipanga kwamba baada ya shughuli hii na baada ya kumaliza kipindi kile cha muda wa maswali ambacho kilikuwa kinaishia saa 4:30 basi tumuite Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa ajili ya kufanya majumuisho ya bajeti ya serikali.

Kwa hivyo, tuna muda wa dakika zisizozidi 30 kumaliza jambo hili. Hivyo, niruhusu maswali mawili au matatu kama yapo. Mhe. Saleh Nassor Juma. Samahani sana. Kwanza tumruhusu Mwenyekiti kutoa taarifa ya kamati.

Hotuba ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii Kuhusu Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika 16 Juni, 2012

Mhe. Amina Iddi Mambrouk: (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa katika hali ya uzima na afya, na kuweza kuendelea kutekeleza wajibu na majukumu ya Baraza lako tukufu, kwa niaba na kwa ajili ya maendeleo ya Wazanzibar wote.

Mhe. Spika, aidha, napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, kuungana na wizara yetu muhimu inayosimamia mambo yote yanayohusu ustawi wa watu wetu, maendeleo ya wanawake na watoto, kwa kutoa maoni ya kamati juu ya maadhimisho ya siku ya Mtoto wa Afrika.

Mhe. Spika, Wajumbe wa Kamati yangu ni kama wafuatavyo:

Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Mwenyekiti
Mhe. Hijja Hassan Hijja	-	Makamo Mwenyekiti
Mhe. Ashura Sharif	-	Mjumbe
Mhe. Asha Abdu Haji	-	Mjumbe

Mhe. Saleh Nassor Juma	-	Mjumbe
Mhe. Nassor Salim Ali	-	Mjumbe
Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Mjumbe
Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Mjumbe
Ndg. Asha Mohd Said	-	Katibu
Ndg. Talib Enzi	-	Katibu

Mhe. Spika, Siku ya Mtoto wa Afrika ni siku muhimu katika kushajihisha jamii ya Waafrika hususan Zanzibar katika kuhakikisha kuwa haki za watoto zinalindwa na kusimamiwa ipasavyo. Ni siku ya kumbukumbu ya mauwaji ya watoto katika harakati za kupinga ubaguzi dhidi ya kupatiwa haki zao nchini Afrika ya Kusini mwaka 1976.

Mwaka 1991 Umoja wa Afrika uliona umuhimu wa kuwepo kwa siku hii. Kielelezo cha umuhimu huo kinatokana na historia hiyo katika maendeleo ya kudai haki za watoto katika ngazi ya Kimataifa na Kitaifa.

Mhe. Spika, watoto wengi katika nchi za Afrika bado wanakabiliwa na matatizo mbali mbali ikiwemo kutopatiwa huduma bora, ambapo pamoja na mambo mengine hali hiyo hutokana na hali ya umasikini unaozikabili nchi nyingi za Afrika.

Mhe. Spika, Kamati ya Ustawi wa Jamii inaipongeza sana wizara kwa hatua iliyofikia katika kuratibu na kusimamia shughuli zote za utekelezaji wa haki, wajibu na maendeleo ya watoto Zanzibar.

Mhe. Spika, kamati yetu inaisisitiza jamii upande mmoja na serikali upande wa pili, wakati huu kutafakari njia bora na zenye manufaa katika kumlinda mtoto pamoja na kumpatia yale yote muhimu anayostahili ikiwemo elimu, huduma za afya, chakula pamoja na matunzo bora kwa ujumla.

Usajili wa Vizazi na Vifo:

Usajili wa watoto na utoaji wa vyeti ni haki ya pili ya msingi ya mtoto baada ya kupewa jina. Jukumu hili kwa mujibu wa Sheria Nam. 6 ya mwaka 2006, hutekelezwa na Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo. Kamati yetu Mhe. Spika imeona kwamba kuna changamoto kubwa inayoikabili ofisi hiyo, katika kutekeleza haki ya pili ya mtoto ya kusajiliwa na kupatiwa vyeti vyao vya kuzaliwa. Suala hili Mhe. Spika, huchangiwa na mfumo wanaoutumia kiutendaji na utunzaji kumbukumbu, ambao unaosababisha kudorora kwa kazi na upotevu wa nyaraka.

Aidha, mazingira ya kiofisi pia yanasababisha msongamano pamoja na bajeti finyu ambayo inazuia utekelezaji wa mipango mizuri. Hivyo, lazima serikali iliangalie kwa umakini mzuri.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya ina jukumu kubwa la kuimarisha *progam* za elimu na kuwa endelevu kwa jamii juu ya umuhimu wa chanjo, kinga dhidi ya malaria, utoaji wa vitamin A na dawa za minyoo, kinga dhidi ya UKIMWI pamoja na huduma za afya ya uzazi. Elimu hiyo itasaidia katika kupunguza vifo vya watoto wachanga chini ya miaka mitano na hata vile vifo vitokanavyo na uzazi kwa kina mama wajawazito.

Hata hivyo, ipo haja kwa wizara kuitafutia ufumbuzi changamoto ya upungufu wa watoa huduma za chanjo katika vituo vya afya, kiwango kidogo cha chanjo kanda ya Pemba na ukosefu wa fedha za uendeshaji wa huduma hiyo kila siku.

Mhe. Spika, Kamati ya Ustawi wa Jamii inapongeza juhudi za serikali katika utekelezaji wa kuwaendeleza watoto kielimu pamoja na kuwepo kwa baadhi ya changamoto. Uchukuaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza umepiga hatua nzuri ya mafanikio. Hata hivyo, serikali ni vyema kuzingatia changamoto ya kuwepo kwa ongezeko kubwa la watoto kila mwaka, ili kuweza kuandaa mazingiriza bora ya elimu kwa ajili ya watoto hao baadaye.

Aidha, kamati yetu imebaini kuwa katika sekta ya elimu watoto wenye mahitaji maalum bado huandikishwa kwa kiwango kidogo sana, kukatisha masomo watoto kutokana na utoro na ndoa za mapema kunakosababishwa na hali duni ya maisha pamoja na udhalilishaji wa kijinsia kwa watoto wa kike na kiume.

Mhe. Spika, licha ya juhudi kubwa za Wizara yetu ya Ustawi wa Jamii, udhalilishaji wa watoto wetu bado upo, ambapo watoto wanaendelea kuathirika kutokana na kukosa usalama, kutendewa ukatili, kukandamizwa, kunyanyapaliwa, kubaguliwa na hata kutelekezwa.

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inaiomba serikali kuwasilisha ripoti rasmi ya Kamati iliyoundwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kufuatilia masuala ya udhalilishaji wa watoto mbele ya Baraza lako. ili Baraza liweze kuelewa kiini cha matatizo hayo na hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa ikiwezekana kuliondoa kabisa.

Mhe. Spika, kamati yangu inaishauri wizara husika kusambaza taarifa mbali mbali za udhalilishaji wa watoto kwa wadau wengi wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ili kila mmoja wetu aweze kuanza kuchukua hatua pale alipo badala ya kuziachia pekee familia za waathirika na matukio haya yanapotokea.

Ajira za Watoto:

Tatizo la ajira mbaya kwa watoto pia bado ni sugu hapa Zanzibar. Tafiti ndogo zilizofanywa zimeyataja baadhi ya maeneo ambayo huendeshwa ajira hizo yakiwemo Soko la Mwanakwerekwe, Bandari ya Malindi na Chumbuni kwa upande wa Unguja na Wilaya ya Micheweni Pemba.

Tatizo hili limeelezwa kuwa limekosa msukumo na kupata mafanikio kutokana na wazee wenyewe wengi wao kutoona umuhimu wa kuhakikisha watoto wanapata elimu ya lazima. Mhe. Spika lazima tukubali kwamba suala la ajira mbaya kwa watoto ni tatizo kubwa la kila taifa, hivyo hatuna budi sote tuungane na kupiga vita tatizo hilo.

Mpango wa Kuwatambua Watoto Wenye Mazingira Magumu Zaidi:

Kamati yetu inaipongeza wizara kufikia hatua ya kuanzisha mpango wa kitaifa unaolenga kuwatambua na hatimaye kuhakikisha kuwa wanapata haki zao za msingi watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

Mhe. Spika, kamati yetu imevutiwa sana na mpango huu, ambao hatua zake za awali za utekelezaji zinaleta matumaini. Huu ni mpango mzuri ingawa umeonesha kuwa ni wa gharama kubwa. Hivyo, tunaishauri serikali kuunga mkono mpango huu, ili tuweze kukabiliana na matatizo yanayowakabili watoto wetu ambao ni taifa la kesho.

Mhe. Spika, Kamati ya Ustawi wa Jamii inaikumbusha serikali kuwa bado ina changamoto kubwa katika utekelezaji wa haki ya kulindwa watoto wetu. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na upatikanaji wa fedha za kuendeshea huduma za kitaifa za watoto.

Kamati yetu inaishauri serikali kuangalia na kuipitia upya kiwango cha asilimia 34.5 ya bajeti ya serikali iliyopangwa kwa ajili ya kutekeleza kuendeshea huduma za watoto katika Sekta ya Elimu, Afya, Maji Safi na Salama. Kwa kweli kiwango hicho kamati yetu inaona kwamba ni kidogo sana kulingana na kuongezeka kupanda kwa gharama za huduma za kijamii zinazomhusu mtoto. *(Makofi)*

Mwisho Mhe. Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inaungana na ujumbe wa mwaka huu wa Maadhimisho ya Mtoto wa Afrika, kuwa “Haki za Watoto Wenye Ulemavu ni Jukumu Letu Kuzilinda, Kuziheshimu, Kuziendeleza na Kuzitekeleza”. *(Makofi)*

Mhe.Spika, naomba nichukue fursa hii tena adhimu kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti, tunakushukuru kwa Taarifa hiyo ya Maoni ya Kamati na muda wetu ni mchache sana, naomba niruhusu maswali kama watatu mpaka manne kutoka kwa Waheshimiwa Wajumbe kama yapo.

Waheshimiwa Wajumbe, nimewaona Waheshimiwa wanne ambao wananitosha Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Subeit Khamis Faki pamoja na Mhe. Raya Suleiman Hamad.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipatia fursa kidogo ya kuweza kutia nyalio kuhusiana na taarifa hii aliyoitela Mhe. Waziri.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, uliza maswali.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kwanza naomba uniruhusu kidogo niipongeze serikali kwa kuleta hii taarifa na kwa sababu mimi ni mdau wa wanawake na watoto, kwanza mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, pili ninaye mke pamoja na watoto kwa hivyo ni mdau katika suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba niulize swali la mwanzo. Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye sura ya Umoja wa Kitaifa, kwa kweli katika suala la wanawake na watoto kuna changamoto kadhaa, ikiwa ni muitikio mdogo wa hawa wanawake katika suala zima la Uzazi wa Mpango, ambapo kwa mujibu wa *World Health Organization (WHO),* yaani kwa Zanzibar ni kama asilimia 12 waliojiunga na Uzazi wa Mpango.

Je, serikali ina mpango gani wa kuwahamasisha zaidi wananchi kujiunga na uzazi wa mpango kwa lengo la kupatikana kwa afya ya mama na mtoto? Hilo la kwanza.

Pili wale wanaojifungua katika vituo kwa mujibu wa *World Health Organization (WHO)* pia ni kama asilimia 49, yaani kuna karibu asilimia 51 ambao wanaozalia majumbani jambo ambalo ni hatari mno na sio kwa akinamama tu hata kwa vile vichanga. Mhe. Spika, serikali katika suala hili ina mkakati gani kuhakikisha kwamba hizi asilimia za akinamama wanaojifungulia majumbani wanakwenda vituoni kwa ajili ya kujifungua?

Vile vile kuna suala hili la ajira za watoto. Mhe. Spika, kwa kweli kazi hizi zimekithiri hususan katika sehemu za madiko. Kwa mfano, Mkokotoni, Wesha, tumejitahidi sana katika masuala ya kuchimba kokoto kule Micheweni tunawaona watoto vidole. Kutokana na hali hiyo, serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba inazuia hizi ajira za watoto. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mwisho kabisa ni suala zima la vitangi. Kwa kweli watoto katika maeneo kadhaa huwa wanabakwa na hawa vitangi. Je, ni lini serikali italeta mswada hapa Barazani kusudi yeyote anayeshughulika na mambo ya kuwabaka watoto ahasiwe? *(Makofi)*

Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, na mimi kwa idhini yako naomba nimuulize Mhe. Waziri maswali mawili kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwenye ripoti yake Mhe. Waziri ukurasa wa 9 amesema kwamba kila nyumba yenye mtoto chini ya miaka mitano ilipata chandarua kupitia Wizara ya Afya, lakini zipo nyumba hadi hii leo kwa bahati mbaya hazikupata vyandarua hivyo.

(a) Je, yeye kama Waziri ambaye anasimamia maslahi ya mtoto atakuwa tayari kushirikiana na viongozi, ili kuzitafuta nyumba ambazo hazikupata vyandarua kwa ajili ya kupatiwa haki hii?

(b) Mhe. Spika, dunia sasa imeamua kutenga bajeti maalum kwa ajili ya maendeleo ya mtoto na SMZ chini ya Wizara ya Fedha ilitamka wazi kwamba bajeti hii itaangalia maslahi ya mtoto. Lakini kwa bahati mbaya fungu ambalo limetengwa ndani ya wizara yake ni asilimia 0.8 tu ya maendeleo kwa ajili ya mtoto. Je, fungu hili litamsaidia vipi mtoto wa Zanzibar kwa ajili ya kujikwamua na matatizo ya watoto?

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, mimi leo ninalo swali dogo sana nimesoma hiki kitabu na kimeeleza kuhusu watoto waliofanyiwa upimaji wa afya zao, yaani wanafunzi na kwenye jaduweli kwenye ukurasa wa 28.

Kwa upande wa Unguja jumla ya wanafunzi 2,451 walifanyiwa upimaji wa afya zao na waliogundulikana na matatizo ni wanafunzi 2,045 na hii ni sawa na asilimia 83.1. Kwa upande wa Pemba jumla ya wanafunzi 1,465

walifanyiwa upimaji wa afya zao na waliogundulikana na matatizo ni wanafunzi 507 tu ambao ni sawa na asilimia 34.61.

Mhe. Spika, nataka kujua katika kufanya upimaji huu kwa vile Unguja wenye matatizo ni asilimia 83.1 na Pemba ni asilimia 34.6. Je, wizara imebaini nini, kwa nini Pemba hali ikawa ni afadhili na Unguja ikawa hali ni mbaya sana na wana ushauri gani juu ya hilo?

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali kuhusu Taarifa hii ya Mtoto wa Afrika. Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu kuishukuru sana serikali yetu kupitia Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa kukumbuka siku hii ya Mtoto wa Afrika.

Kwa kweli napenda nimuulize Mhe. Waziri, kwa sababu Siku hii ni ya Mtoto wa Afrika na watoto wako wa aina mbili, yaani kuna watoto wenye ulemavu na wengine wasio na ulemavu.

Sasa napenda nimuulize Mhe. Waziri katika kuadhimisha Siku hii ya Mtoto wa Afrika, kwa sababu kuna watoto wenye ulemavu wengi kama vile wa akili na wengine walemavu wa viungo. Je, namuuliza Mhe. Waziri kupitia serikali yetu ni zawadi gani zilitolewa kwa watoto hawa ambao wenye ulemavu ukizingatia wengine wanahitaji vigari kwa ajili ya kuwasaidia katika kwenda pamoja na vifaa vya kusikilizia.

Je, kupitia serikali yetu imetoa zawadi gani kwa watoto, ili kujisikia kama siku hiyo ni ya Mtoto wa Afrika na kama hakuna, basi je haioni kama serikali kwamba kuna haja ya kuandaa utaratibu maalum wa Siku hii ya Mtoto wa Afrika wakapewa watoto zawadi kama vile vigari au vifaa vya kuwasaidia katika kusikia, ili wakaona ni siku yao kweli na kujisikia?

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Spika, ahsante kwanza naipongeza serikali pamoja na Mhe. Waziri wangu kwa jitihada kubwa na tukaweza leo kupata ripoti hii.

Mhe. Spika, swali langu la kwanza ni kwamba kutakuwa na mkakati gani maskuli kuhusu unyanyasaji wa watoto wenye ulemavu kwa walimu na watoto wenzao. Kwa kweli hivi sasa nimepigiwa siku kuna watoto katika Skuli ya Mbuzini ambao ni walemavu wa akili, wasioona na wale wasiosikia, yaani wengine hawendi tena skuli kutokana na unyanyasaji.

Kwa upande wa walimu kutakuwa na mkakati gani kuweza kuelimishwa juu ya watoto hawa wakati wanapochelewa kufika skuli wasiwachape, kwa sababu hawa wanapowachapa ndipo wanapokimbia skuli na ikakosekana hiyo elimu.

Mhe. Spika, pia kuhusu Wizara ya Afya. Je, serikali ina mkakati gani kwa watoto wenye ulemavu Wizara ya Afya kupewa kipambele wakati watakapokwenda hospitali kupata matibabu haraka. Kwa kweli tunashuhudia watoto hospitali wanapelekwa na mtoto akiwa hajiwezi, basi watu wengine watapata matibabu mpaka daktari ataondoka na mtoto mwenye ulemavu hawezi kushughulikiwa.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika kupata maelezo kuhusu mikakati hii dhidi ya watu wenye ulemavu.

Jambo la tatu ni Kuhusu ubakaji. Mhe. Spika, swali langu la ubakaji ni kwamba watoto wanabakwa sana. Je, serikali ina mkakati gani ya watoto hawa wanaobakwa hasa watu wenye ulemavu, watoto, wanawake na wanaume na ikawa kesi zinatupiliwa mbali hata kama utapelekwa ushahidi.

Kwa mfano, mtoto ni bubu anaambiwa lazima afumbue mdogo na aseme, lakini aliyeona hayupo. Kwa hivyo, tunaomba serikali itueleze katika mambo kama haya.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, wazazi wamechangamka kweli, mwisho kabisa Mhe. Fatma Mbarouk Said.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuichangia taarifa hii aliyoiwasilisha Mhe. Waziri. Lakini mimi naomba niende kwenye suala la Elimu Mbadala. Kwa kweli hapa watoto tunawasomesha na tunawapa mafunzo na baada ya kutoka pale wanakuwa na changamoto kwamba hawana kazi za kufanya.

Kwa hivyo, ninaomba suala hili serikali ikalitilia mkazo kwamba wanapoondoka pale, basi ni vizuri kuwawezesha hawa watoto, kukaa pamoja na wakafanya zile kazi za amali ambazo wamepewa na itakuwa ni ajira kwao.

Vile vile kuna changamoto hizi kwenye ukurasa wa 29 nimeona kuna changamoto hizi ambapo moja ni idadi kubwa ya wanafunzi madarasani. Mhe. Spika, hizi zisiwe ni changamoto tu kila siku, hivyo ingefaa kwa serikali ikatafuta *solution* kuhusu suala la watoto kuzidi madarasani na uhaba wa vifaa.

Nadhani nishukuru tu kwamba bajeti yetu hivi sasa imezingatia hayo na kutafuta vifaa hivi, kwa kulipa kodi mbali mbali ili kuondosha tatizo hili. Kwa hivyo, hizi changamoto nafikiri ni vizuri serikali ikae na izingatie namna gani ya kuzisawazisha changamoto hizi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika suala la lishe tunaona serikali kwamba.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, unatakiwa uulize maswali.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, maswali niseme Mhe. Waziri atachukua juhudi gani kuhusiana na changamoto kuzisahihisha, ili tuone watoto wetu wanaondokana na matatizo haya katika skuli zetu mbali mbali kama vile suala la kuwepo wanafunzi wengi madarasani?

Mhe. Spika, ni hayo tu na ninashukuru sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kumwita Mhe. Waziri anayehusika Wizara ya Afya ina mashirikiano makubwa juu ya jambo hili, basi ni vizuri tukapata maelezo kutoka Wizara ya Afya kuhusu maswali yaliyoulizwa.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kutoa maelezo kidogo kuhusu suala la Siku ya Mtoto wa Afrika. Mhe. Spika, naomba niwaeleze Waheshimiwa Wajumbe kama siku tatu mpaka nne ilikuwa sipo Barazani na nilikuwa *Washington* kwenye mkutano wa siku mbili, ambapo siku mbili zote hizo zilikuwa zinajadili jinsi ya kunusuru maisha ya mama na watoto wachanga. Kwa kweli tumejadili kwa urefu na yamezingatia matatizo yanayowakabili akinamama. *(Makofi)*

Kwa hivyo, hoja ya kuwalinda watoto duniani iko katika kazi ya kimataifa na wala haiko tena kwamba ni suala la Wizara ya Afya au Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, zilikuja pale nchi kama nne mpaka tano zilizoonesha *Case Study* kiasi gani wamefanikiwa. Miongoni mwa nchi hizo ilikuwa ni India, Ethiopia, Malawi na nyengine utashangaa pamoja na shida zao, lakini ni *Democratic Republic of Congo*, hawa walikuja kuonesha ni kiasi gani walivyoweza kulikabili tatizo hili na vipi au kiasi gani wamefanikiwa.

Mhe. Spika, wakubwa wadunia walikuwepo pale kama vile Dr. Margaret Chan wa *WHO*, mama Hillary Clinton alikuja na kutoa hotuba pale, pia alikuja na Waziri wa Afya wa Marekani pamoja na wataalamu waliofanya *research* juu ya matatizo haya yanayowakabili watoto.

Kwa ufupi suala la watoto linatizamwa katika sura ya kumlinda mama na mtoto kwa pamoja. Mhe. Spika, tulichoagizwa au kinachotakiwa kufanyika ni kwamba tusimtizame mtoto baada ya kuzaliwa tukaanza kutizama lishe au tusimtizame mtoto baada ya miaka mitano ambayo ndiyo dhamana ya Mheshimiwa.

Mimi kama Waziri wa Afya natakiwa nimtizame tangu mama anaanza kuchukua mimba. Kwa kweli moja katika kosa linalofanyika ni kwamba tunamuacha mama masikini hana uwezo anachukua mimba kwa shida anakizaa kitoto na kikesha kuzaliwa tu baada ya siku 28 anakufa na hilo ni moja.

Pili kinachonusurika baada ya siku 28 kinakuwa hakina lishe. Sasa atulichoambiwa tusiitizame lishe baada ya kuzaliwa na tuitizame lishe tangu iko kwenye mimba. Kwa kweli imegundulikana kwamba moja katika maradhi yanayosababisha watoto kufa ni *Diarrhea* na *Pneumonia*, yaani wengi wanakufa kwa sababu hizo na kuna maradhi mengine, lakini hayo ndio yaliyochukua nafasi kubwa. Kwa hivyo, tumepewa jukumu tutayarishe katika daraja ya serikali kulitizama suala la mama na mtoto kwa upeo wake.

Mhe. Spika, kuna Mhe. Mjumbe mmoja alizungumza hapa suala la walemavu kushughulikiwa hospitali hilo tumelisikia na tutalizingatia, ili kuwapa kipaumbele kutokana na hali zao. Vile vile kumekuwa na suala la

kuambiwa na wazee pia wakija washughulikiwe. Kwa hivyo, haya ni masuala ya kushirikiana kati yetu na wahusika wa idara hizi.

Kwa hivyo, ninachotaka kusema ni kwamba suala la watoto ndio taifa la kesho na suala la mama ndio anayetayarisha taifa la kesho. Kwa maana hiyo, tunahitaji kulipa kipaumbele, kwamba hasa sisi hapa tumekuwa Maspika na Waziri wa Afya, kwa sababu mama zetu walitutunza na wakatushughulikia. Vile vile tumeambiwa kama tunataka taifa la 2021 na 2022 basi tunanze leo.

Mhe. Spika, mkakati wa kuimarisha huduma hii kwa miaka 10 iliyopita imeweza kunusuru watoto milioni 5,700,000 na imeonekana kwamba kumbe inawezekana kama tutatoa umbele suala hilo la kuwanusuru watoto linawezekana.

Lengo la dunia ni kwamba ifikapo mwaka 2035 na sisi wengi wetu nadhani tutakuwa tumeshafika mbele ya Subuhana iwe linazungumzwa suala la watoto na akinamama kupoteza maisha yao iwe chini ya asilimia 20 katika *level* ya kimataifa na iwe chini ya asilimia 15 katika *level* ya nchi. Kwa hivyo, tunalo jukumu kubwa na tunao wajibu sote na sisi Waheshimiwa Wajumbe hapa ndio wazazi na na sisi ndio waume na sisi ndio wake na sisi ndio walezi. Tunahitaji kulipa umbele suala hilo.

Mhe. Spika, kumekuwa na tabia kuonekana kwamba suala la watoto ni suala la mzazi tu. Nakumbuka zamani ilikuwa malezi ya watoto ni malezi ya jamii. Tunahitaji kurudi huko. Mimi nilikuwa nikifanya makosa nilikuwa sihukumiwi na baba angu, nahukumiwa na mzee yoyote wa kijijini. Tumeliacha hilo na kila mmoja amejiona wanangu ni wanangu akigombwa anahamaki, akipigwa anashitaki, matokeo yake jamii inavurugika na gharama inaendelea kuwa kubwa.

Mhe. Spika, nilitaka kusema hili kuwaeleza Waheshimiwa, nashukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza na mimi nataka nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa kuwasilisha hii Ripoti ya watoto. Ukweli na mimi nataka nikubaliane nayo kwamba hawa watoto ni watoto wetu. Tunawajibu wa kuwasaidia ili wafikie kama vile sisi wazazi wao tulivyo.

Kwa upande wangu zaidi limezungumziwa suala zima la bajeti. Mimi nataka nisema tu kwamba bajeti ya mtoto huwezi ukaiona katika Wizara ya Watoto peke yake. Bajeti ya mtoto utaiona katika wizara nyingi sana, utaiona katika Wizara ya Afya kama Mhe. Waziri alivyoeleza, Wizara ya Elimu, vile vile utaiona katika Wizara ya Kilimo, kwa maana ya lishe ya mtoto jinsi gani tunavyojiandaa kwa kutengeneza lishe ya mtoto.

Mhe. Spika, mimi nataka nisema tu kwamba kila hali yetu itakapokuwa nzuri ni dhahiri kwamba bajeti ya mtoto tutakuwa tukiiongezea kupitia sekta mbali mbali. Mimi nilikuwa naangalia hii Ripoti ya Mhe. Waziri ambayo ametupa katika ukurasa wa 21. Nataka wenzangu waiangalie picha hiyo iliyokuwepo katika ukurasa wa 21, na kwa kweli picha hiyo ina ujumbe mzito sana kwa watoto wetu.

Watoto hawa tunawapatia mafunzo ya teknolojia ya hali ya juu. Tunawafundisha matumizi ya kompyuta lakini watoto wako chini. Ndio yale ambayo nilikuwa nayalilia katika bajeti yangu hii. Kwa hivyo haya yote tunayazingatia Mhe. Spika. Tunayazingatia katika Serikali Kuu, tunayazingatia pale ofisini kwangu ili kuhakikisha kwamba watoto hawa wanapata haki zao za msingi ili waweze kuishi vizuri.

Kwa upande wa bajeti kama nilivyoelezewa tutakuwa tukiliangalia siku hadi siku. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii nimshukuru kwa dhati Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii pamoja na Kamati yake kwa namna tunavyoshirikiana nao, wanavyotupatia miongozo yao, ushauri wao, maelekezo yao, yanatusaidia sana, ndio maana tunafanikiwa katika kazi zetu za siku hadi siku. Kwa hivyo nawapongeza sana Kamati ya Ustawi wa Jamii.

Mhe. Spika, nikianza na Mhe. Saleh Nassor Juma, pamoja na kuwashukuru wale wote waliotoa majibu yao. Huyu itabidi nimjibu mimi. Anasema tuna muiitiko mdogo wa uzazi wa mpango. Ni kweli kila mmoja anasema, kila mtoto ana rizki yake kwa hivyo tuendelee kuzaa tu. Hili lipo tena lipo sana hasa vijijini. Umefika wakati sasa tuwaelimishe wenzetu kwamba hali ya maisha imebadilika, lazima tuwasomeshe watoto wetu, sio kuwasomesha darasa la kwanza mpaka la 5 au la 6 ikawa basi. Nchi yetu itakuwa ipo chini kielimu. Kwa hivyo kama utakuwa na watoto wengi utashindwa kuwasomesha vizuri.

Akasema pia watoto wanabakwa kwa nini hatuletewi msaada hapa wa sheria wa kusema watu wahasiwe. Eeeeh sheria ni msumeno, inakwenda nyuma na mbele, leo unasema mwenzio ahasiwe je, likikutokea wewe utakuwa tayari kuhasiwa? Kwa sababu sisi tunayo sheria ya mtoto ambayo tumeileta hapa ina ufafanuzi mbali mbali. Tunachoomba Mahakama zitusaidie angalau hawa wabakaji wapate adabu. Adabu ikiwa ndogo kwa mfano mtu unamwambia toa laki moja na kifungo cha nje. Ataitoa laki moja, atakuwa na kifungo cha nje, lakini kule kule nje akimkutia mwengine basi atamshughulikia. Inakuwa haitoshi adhabu ile.

Kuhusu suala la bajeti naona Waziri pale ameshaijibu vizuri. Niingie kwa Mhe. Hija anasema kwamba kuna neno moja ambalo Mhe. Waziri hapa kalisahau kuhusu vyandarua. Wengine wamepata vyandarua, wengine hawakupata vyandarua. Serikali kwa kweli ilijitahidi kutoa vyandarua kwa watu waliokuwa na watoto na hata kwa wasiokuwa na watoto. Tatizo lililokuwepo basi hivyo vyandarua vyenyewe watu hawajifunikii wamevitia masandukuni. Hata hivyo Serikali ina matangazo maalum kuwambia watu wajifunike vyandarua kujihifadhi na malaria na kadhalika.

Zipo sehemu nyengine kweli walikosa vyandarua, lakini serikali inashughulikia, kidogo kulitokezea matatizo ya hapa na pale, baadae pengine huenda wakapata huu msimu mwengine wa ugawaji huenda wakapata.

Mhe. Salim Abdalla Hamad anasema kaona takwimu katika kijitabu kile. Bila shaka imeonekana kwamba sehemu nyengine zina matatizo, sehemu nyengine hazina matatizo. Naomba nimwambie kwamba tumebaini kwamba matatizo yapo, na ishallah tutayashughulikia. Serikali inajitahidi sana kutoa chanjo, kutoa maelekezo, kutoa misaada mbali mbali. Pamoja na hayo hatuachi kupata matatizo, kwa hivyo takwimu zinajieleza kama hali ilivyo.

Mhe. Subeti na yeye alisema kwamba sisi tulikuwa na sherehe ya Siku ya Mtoto yaani ile tarehe 16. Je, hawa watoto wenye ulemavu walipatiwa zawadi na kama hawajapatiwa zawadi basi mara nyengine tujitahidi wapate zawadi. Sisi kila tunapopata cha kuwapa watoto wenye ulemavu serikali inawapa. Kwa njia hii au nyengine watoto wenye ulemavu wanashughulikiwa sana na serikali.

Nije kwa Mhe. Raya Suleiman Hamad, anasema kuna mkakati gani huko maskulini kuhusu haya mambo ya unyanyasaji. Mkakati tulionao kwa maskuli ni kukaa pamoja na walimu, na walimu nao kuwaelimisha watoto kuhusu suala zima la unyanyasaji. Watoto wajue kwamba kuna unyanyasaji, watoto wajue kwamba kuna ubakaji, watoto wajue kwamba kuna udhalilishaji. Kwa hivyo wasikubali kubakwa, wasikubali kudhalilishwa, wasikubali kunyanyaswa kwa mambo madogo madogo. Mtu anakupa pipi anakutia kwenye chumba cha siri anakuhadaa anakubebesha mimba, hayo ni matatizo. Wakati tunao mkubwa na Ishalla tutajitahidi kuwaelimisha walimu ili wawaelimishe watoto juu ya suala hili.

Mhe. Fatma Mbarouk anasema tuna mambo ya elimu mbadala, yaani tunamtoa mtoto kwenye kupara samaki tunakuja nae skuli. Lakini pale anasoma halafu anamaliza. Akimaliza sasa afanyeje? Jamani kazi serikalini haiwezi kuajiri watu wote, lakini sisi jambo kubwa tunawafahamisha wenzetu kwamba tujitume tusisubiri serikali. Hivi kweli sisi hapa Zanzibar tunaweza sote tukaingia katika ofisi za serikali. Huko nje sasa atabaki nani. Kwa hivyo mtoto huyu tunayemtoa kwenye kupara samaki, tunamuweka skuli pale akishakupata elimu yake basi na yeye ajitume. Hatuwezi kusema kwamba watu wote tunao uwezo wa kuwaajiri. Tunasema kwamba kilimo ni muajiri mkubwa katika nchi yetu. Watu kilimo hawakitaki, vijana kilimo hawakitaki kabisa habari ya kilimo.

Lakini ni changamoto zipi tulizonazo? Changamoto kubwa sisi ni kuwaelimisha vijana kwamba ajira si ya serikali tu, vijana wafanye kazi wajiajiri wenyewe ili wajisaidie wao wenyewe, waisaidie na serikali. Nadhani tukifikia hapo wito huo vijana wakaushika tutasimama pahala pazuri. Nashukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ilikubaliwa na kuafikiwa)

HOJA ZA SERIKALI

Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi
kwa mwaka wa Fedha 2012/2013

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, jana tulifikia pahala pazuri sana baada ya kupokea maelezo kutoka kwa Waheshimiwa Mawaziri mbali mbali, kutokana na mijadala iliyokuwa inaendelea tangu siku ya Jumatatu. Tukakubaliana leo hii baada ya shughuli zilizofanyika basi tupate maelezo ya majumuisho na hatimae kukamilisha kazi hii inayohusika. Wakati Mhe. Waziri anapotoa majumuisho ningependa sana huu ukumbi ukajaa. Hii ni kazi moja muhimu sana ambayo niwaombe basi Wanadhimu wa pande zote mbili wawachunge Waheshimiwa wajumbe kila mmoja kwa upande wake wawemo ndani kumsikiliza Mheshimiwa.

Juzi na jana amepewa cheo cha Profesa wakati anafanya majumuisho, na hatimae kutoa hoja juu ya mpango huu wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2012/2013. Nichukue nafasi hii kumkaribisha Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nataka nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali maombi yangu ambayo nimeyaeleza wakati nikitoa hotuba hii.
La pili nataka niwashukuru Wajumbe vile vile na wao kwa kunikubalia. Sasa naomba basi ninukuu vifungu viwili tu, ili kila mmoja tuweze kufahamu yale maombi yalikuwa yepi. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba ninukuu kifungu cha 143 cha hotuba. Nimesema hivi:-

> "Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa umahiri wako wa kuliendesha Baraza hili katika hali ya amani na utulivu."

Ni matumaini yangu kwamba busara na hekma zako zitaendelea kuongoza vyema majadiliano ya vikao vya Baraza hili, kwa kadiri ya upeo wako na hekma zako ukisaidiwa na Naibu Spika, umeongoza vyema mjadala huu wa bajeti. Vile vile naomba ninukuu kifungu namba 150 nimesema hivi:-

> "Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa heshima, taadhima na unyenyekevu naomba sasa Baraza lako tukufu lipokee, lijadili na hatimae lipitishe mapendekezo juu ya muelekeo wa uchumi, mpango wa maendeleo na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2012/13"

Ndivyo nilivyowaomba Wajumbe, mpokee, mjadili. Mmejadili kadiri ya uwezo wenu, mjadili kwa ufasaha, naomba basi nitoe takwimu kidogo mwa yale mliyoyajadili. Mhe. Spika, wakati Waheshimiwa Wajumbe wakijadili bajeti hii kama wengi mlivyokuwa mnaniangalia sikutoka, vikusinzia, sikuacha kalamu kwenye mkono, maswali yaliyoulizwa, hoja, michango, maoni, yalikuwa ni 256, wajumbe walitumia masaa 15: 30 kujadili bajeti hii. Lakini nilichokifanya ili kuweza kuokoa muda wako na muda wa wajumbe nimeyapanga maswali na hoja na ushauri katika maeneo 22. Haya ndiyo leo nitayajibu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba niwataje wale wote ambao wamechangia. Waliochangia kwa kuzungumza au kwa kusema walikuwa ni 42:

1. Mhe. Hamza Hassan Juma
2. Mhe. Rashid Seif Suleiman
3. Mhe. Mohammed Raza
4. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
5. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
6. Mhe. Omar Ali Shehe
7. Mhe. Fatma Mbarouk Said
8. Mhe. Hassan Hamad Omar

9. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
10. Mhe. Ali Salum Haji
11. Mhe. Shawana Bukheti Hassan
12. Mhe. Mohammed Haji Khalid
13. Mhe. Hija Hassan Hija
14. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
15. Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa
16. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
17. Mhe. Ali Abdalla Ali
18. Mhe. Asha Bakari Makame
19. Mhe. Salma Mohammed Ali
20. Mhe. Asaa Othman Hamad
21. Mhe. Ashura Sharif Ali
22. Mhe. Saleh Nassor Juma
23. Mhe. Subeit Khamis Faki
24. Mhe. Mansoor Yussuf Himid
25. Mhe. Mussa Ali Mussa
26. Mhe. Pandu Ali Abdalla
27. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
28. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
29. Mhe. Mbarouk Mtando
30. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
31. Mhe. Salmin Awadh Salmin
32. Mhe. Rufai Said Rufai
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
34. Mhe. Haji Faki Shaali
35. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
36. Mhe. Waziri Haroun Ali Suleiman
37. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo
38. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
39. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
40. Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

41. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais

42. Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, wengine waliochangia kwa maandishi ni wanne, naomba na wao vile vile niwataje.

1. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman

2. Mhe. Mgeni Hassan Juma

3. Mhe. Salma Mussa Bilali

4. Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Spika, nawashukuru wote hao kwa kuwa wamewakilisha michango ya wananchi tunaowatumikia. Naomba Mhe. Spika, kabla sijaanza kujibu hoja moja moja, kwa ruhusa yako na kwa idhini yako niombe radhi kwa utata wa takwimu uliowasumbua Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Lakini hata hivyo nimetoa baadhi ya takwimu, marekebisho yake na nakuombeni tu kwamba lile buku kubwa lilikuwa ni *draft*, tutakapolikamilisha basi litakuwa ni buku safi kabisa, halitakuwa na utata wa takwimu.

Mhe. Spika, sasa nianze kwa hoja ya kwanza katika zile hoja 22 ambazo nimezieleza kwamba nitazitolea ufafanuzi asubuhi ya leo. Kwanza nianze na ile hoja nzito kukua kwa uchumi, pato la kila Mzanzibari. Waheshimiwa wengi walitaka ufafanuzi katika eneo hili. Baada ya kusikia michango ya waheshimiwa nimeona ipo haja kubwa sana. Tayari nimeshazungumza na Katibu Mkuu wangu Mwenyezi Mungu akitujaalia uhai na uzima katika kikao kijacho Tume ya Mipango ikishirikiana na Idara ya Takwimu, tutawafanyia Waheshimiwa semina katika eneo hili ili tulifahamu kwa undani kabisa nini maana ya kukua kwa uchumi na tafsiri yake kwa pato la kila mmoja wetu.

Niliona ili kufanya hivyo katika bajeti zijazo Mhe. Spika, nitaokoa muda sana kwa kutoa ufafanuzi juu ya eneo hili. Inshallah tuombeane uhai na uzima ili tutimize azma hiyo katika Baraza lijalo. Tuanze kuitizama kifungu hadi kifungu ili kila mmoja wetu aweze kufahamu kwa undani zaidi. Kukua kwa uchumi maana yake ni thamani ya bidhaa zinazozalishwa hapa Zanzibar na huduma zinazolewa hapa Zanzibar. Kuna bidhaa tunazalisha kwa maana katika sekta ya kilimo tunazalisha bidhaa, katika sekta ya afya tunatoa huduma. Kwa hivyo zote hizi tunazozitoa huduma na tunazozizalisha unazitafutia thamani yake katika mwaka ule, halafu unalinganisha na mwaka uliopita hapa unaona ukuaji wa kwa maana ya kasi ya ukuaji. Huo ndio uchumi.

Wengi walisema kwamba uchumi kukua hauonekani kwa mtu mmoja mmoja. Dokta Salmin na Mhe. Ali Juma Shamuhuna walitoa ufafanuzi mzuri jana, ni kweli kwa ukuaji huu ambao tunakwenda nao na maeneo ambayo tunayoyafanyia kazi hatutoweza kuuona kwa mtu mmoja mmoja. Lakini tutauona kwa maendeleo yetu, ujenzi wa barabara, ujenzi wa Viwanja vya Ndege, ujenzi wa maskuli, ujenzi wa vituo vya afya, baadhi ya wananchi wetu wanavyokuwa na magari. Idadi ya wanafunzi wanaomaliza vyuo vikuu. Unaanza kuona katika maeneo hayo ndio unaweza ukaona kwa ujumla.

Mhe. Spika, unapokuja kwa mtu mmoja unapoangalia kipato chake huwezi ukaanza kuona kwa *speed* hii, huwezi ukaanza kuona kwa *activities* tunazokwenda nazo kwa ujumla wake nini cha kufanya katika hili. Cha kufanya katika hili Mhe. Waziri wa Uwezeshaji atakuja kulitolea maelezo ya kina katika hotuba yake. Awawezeshe wananchi wetu katika maeneo yao, katika *economic activities* zao ili waweze kukuza mazao katika maeneo yao na kukuza huduma katika maeneo yao madogo madogo. Ili hali iweze kukua, lakini huyu peke yake Waziri wa Uwezeshaji hatoweza kulifanya peke yake, hilo ni lazima awezeshwe na Waziri wa Fedha.

Ndiyo ile hoja ambayo niliyoisema katika mwaka huu wa fedha tayari nimeanza na kumuwezesha 1.0 bilioni aanzie mwaka huu. Vile vile nimesema hata mimi nikimuwezesha Waziri wa Elimu na yeye ana jukumu kubwa sana kwa hawa vijana wetu. Kuwaelimisha katika *economic activities* zao ambazo zitachangia katika suala zima la kukuza uchumi na mapato yao. Lakini hata nikimuwezesha mimi Waziri wa Elimu, bado kuna nafasi kubwa sana kwa Waziri wa Biashara katika kuwatafutia masoko hawa vijana, ni lazima na yeye awatafutie masoko ili bidhaa zao watakazozizalisha wataziuza katika maeneo gani na kwa bei nzuri.

Hapa kuna uwiano wa sekta mbali mbali. Waziri wa Miundombinu akisaidiwa na msaidizi wake Dokta Gavu, lazima na wao watengeneze barabara ili huyu mkulima na mvuvi mazao yao yaweze kufika kwenye soko. Utaona kwamba huo ni mlolongo mzuri na mzima na hapa ndipo nitakapowanasihi mawaziri wenzangu lazima tuwe na usimamizi wa karibu katika maeneo muhimu, ili hii bajeti tunayoipitisha leo iweze kufika kwa

walengwa, vyenginevyo Wajumbe wa Baraza hili kila siku watakuwa wanatuhoji, wanatuuliza hatusimamii utekelezaji wa yale tuliyokuja kuwaambia hapa.

Mimi ninachokiogopa kimoja tu kwa upande wangu, kwamba Waziri hasimamii utekelezaji wake ndani ya sekta yake ningeweza kumnyima bajeti. Lakini sitaki nifanye hivyo kwa sababu nitawaumiza wengi zaidi. Lakini kutokana na hilo nataka niwaombe sana Waheshimiwa Mawaziri wenzangu tusimamie utekelezaji wa bajeti, ili tuweze kutekeleza haya.

Lakini vile vile nataka niseme ndugu zangu Waheshimiwa Wawakilishi tumeulizwa hapa utumiaji mzuri wa raslimali zetu. Hoja nyengine hii ni muhimu sana, lakini nataka nikubaliane na Mwanasheria Mkuu, raslimali kubwa ambayo hapa tuliyonayo sisi ni amani na mshikamano wa wazanzibari. Tukiipoteza raslimali hiyo ya amani tunaweza tukaomba misaada, tukapewa misaada lakini hakuna atakaetupa amani, ni sisi wenyewe lazima tusimamie amani. Hii ndio raslimali muhimu, amani inapotoweka hakuna mchumi, hakuna mvuvi, hakuna mkulima, hakuna Mwakilishi anayeweza kuirudisha amani hiyo. Nikawanasihi sana wazanzibari wenzangu badala ya kuangalia raslimali ardhi, badala ya kuangalia raslimali bahari, badala ya kuangalia raslimali maji, kwanza tuangalie raslimali amani.

Haya yote ni matokeo ya amani, tumeizungumza sana raslimali ardhi inatumiwa vibaya, inatolewa vibaya nataka niseme ndugu zangu, nitashirikiana na Waziri wa Ardhi tuandae utaratibu mzuri wa utoaji wa ardhi. Tukimaliza bajeti hii nitamuomba Waziri wa Ardhi na watendaji wake na watendaji wangu na mimi mwenyewe, tuandae utaratibu ambao kila mmoja atauelewa. Tutaitazama sheria yetu ya ardhi, tuone kama kuna mapungufu yoyote tuiweke kwenye Baraza hili tuirekebishe. Tutaweka viwango vya malipo ili kila mmoja avielewe hakutokuwa na ubabaishaji tena. Inavyoonekana leo Waziri huyu wa ardhi akija anaweka kodi hii, Waziri huyu akija anaweka kodi hii, Waziri huyu anapunguza hiki. Sasa tutaweka utaratibu mzuri, lakini yote hayo raslimali amani iwe ni ya kwanza. Suala hili Mhe. Spika, limeulizwa na Waheshimiwa wengi, sitapenda kuwataja kwa majina nataka ninusuru muda.

Jengine limeulizwa na Waheshimiwa wengi sitopenda kuwataja kwa majina ili nataka ninusuru muda. Jengine ni ajira. Kwanza nataka niwaambieni Waheshimiwa Wawakilishi kitaaluma mimi ni mtakwimu, sitofanya kosa hata siku moja kukuleteeni takwimu za uongo hapa. Nilipopewa digirii zangu mbili, mimi sikula kiapo kama daktari lakini mimi ninaheshimu taaluma yangu sitofanya kosa hilo nataka nikuhakikishieni. Utafiti tulioufanya wa kaya 2009/2010 ndio uliotwambia katika kila vijana watano mmoja hana ajira 17.1 percent. Inawezekana ni tafsiri iliyotolewa na ILO, hapa ndipo ambapo Waheshimiwa Wawakilishi nimeona tunababaika kidogo, tulikwenda tukauliza nini hata akakwambia kama mimi sina ajira. Suala lilikuwa katika wiki mbili zilizopita, ulikuwa na ajira ya kukupatia kipato suala lilikuwa ni hilo. Na hiki ndio kigezo cha kuuliza kwa mujibu wa *definition* za ILO.

Kwa hivyo tafsiri ile ndio Waheshimiwa Wawakilishi wengi tumekuja kidogo kubabaika, nimesikia wengine walikuwa wakali hapa kuhusu hiyo *one out of five* sitakudanganyeni kwa takwimu hata siku moja. Na takwimu ambayo mimi mwenyewe siiamini sitoitia katika mdomo wangu nikakuleteeni. Ninakubaliana na nyinyi kwamba vijana wetu wengi hawana ajira, nimeshakaa na Waziri wa Uwezeshaji tukalizungumza kwa kina, tuna kamati yetu hapa mimi ndio Mwenyekiti wao, ya kuangalia jinsi gani tutakavyoweza masuala ya vijana wetu kuanza kupata ajira. Lakini tusizungumzie ajira za Serikalini.

Tatizo jengine kubwa la Wazanzibari tuseme ule ukweli ndugu zetu watusikie kuchagua kazi, tusichague kazi tuchukue kazi ambazo ni halali. Leo tukichagua kazi Wazanzibari na kama ajira zimetengenezwa hapa lazima wenzetu watatafuta watu wengine waje wazibe zile nafasi. Kwa hivyo tumeandaa utaratibu mzuri tutaanza kuivamia sekta ya uvuvi kwa kishindo kidogo. Lakini vile vile tumefanya majaribio mazuri sana kwa wenzangu ambao waliopo Kaskazini kilimo cha maua, soko la maua ni kubwa sana Europe. Lakini sisi Watanzania hata asilimia kumi hatujalijaza lile soko na kuna maua mazuri sana yanaota maeneo ya Kaskazini. Tutafanya jitihada hizo na mimi nataka nikwambieni vijana watachezea *foreign currency*. Hatuwezi kukaa tukaanza kuchagua kazi.

Suala jengine ambalo Mhe. Spika, limezungumziwa ni ukosefu au kutopatikana kwa bilioni 18, wazee walikuwa wakali kidogo na mimi nataka niseme na mimi hivyo hivyo niko mkali. Hili suala halikuanza wakati mimi nipo, limeanza tangu kaka yangu Dr. Mwinyihaji, limeanza kule watu wamekwenda mchakato mpaka ikafanywa *study* ikaonekana kwamba kweli hizi pesa zinatakiwa ziende Zanzibar. Vikao vya pamoja vimekwenda tumejadili sana mwisho ikafikia jamani kama kurekebisha sheria basi rekebisheni sheria Zanzibar muwapelekee pesa zao. Sitaki niseme mengi *yaliyopita si ndwele*, lakini wenzetu waliohusika na kurekebisha hawakuwa waangalifu. Hawakulipa uzito katika bajeti yetu, katika kikao cha mwisho kimezungumzwa hapa nadhani Dr.

Salmin amezungumza kikao cha mwisho tulichokutana, Waziri mkuu amewaambia miezi sita imekwisha hamjawapelekea pesa Zanzibar sasa lazima za miezi sita zilizobakia wapelekeeni hawajaleta.

Juzi nimezungumza na Waziri mpya Dr. William Mgimwa namuona ni msikivu nimemueleza, tumekwenda katika kikao chetu cha pamoja cha kodi mimi na Katibu Mkuu wangu, na upande wao wapo tukalizungumza tena hili, tunasubiria sasa. Lakini nataka nikuahidini bado ninakwenda nalo, na Ofisi yangu tumekwishawaandikia barua kuwaonesha athari ya kukosa pesa hizi katika bajeti yetu wenzetu waone hiyo athari.

Nataka nithubutu kusema Waziri Mkuu yuko pamoja nasi katika hili, tulikuwa pamoja na Makamo wetu wa Pili wa Rais tutalifatilia kwa nguvu zetu zote, na kwa sababu leo Makamo wetu wa Rais anakwenda Dodoma nitamuomba azungumze na Waziri Mkuu akituachia sisi tunaweza tukajikuta tumegeuka Tyson.

Jengine ambalo limeulizwa kwa kina Mhe. Spika, ni suala la kushirikiana na sekta binafsi, hapa hatuna ujanja Serikali, ili tuweze kwenda kwa kasi lazima tushirikiane na sekta binafsi. Ndio tumeona kwa upande wetu na katika hotuba yangu nimeeleza tumeona hapa Wizarani nani unampa majukumu haya ya kushirikiana na sekta binafsi, ukitupa sote kwa ujumla maana yake nini, maana yake nitakwenda kwa wakati wangu. Tumekuja na maelezo humu ndani tunaanzisha kitengo cha PPP, *Public Private Person*. Kitengo hiki sasa kitakuwa kina dhamana ya kila siku ya kushirikiana na sekta binafsi, na kutushtua sisi ndani ya Serikali. Sasa tuna utaratibu wa kukutana na utaratibu wa kukutana nao hata Mhe. Rais tuna utaratibu huo.

Ili kuweza kukuza na kupiga *speed* maendeleo yetu, ni dhahiri kwamba tushirikiane na sekta binafsi. Tunaiangalia vile vile sheria ya *procurement* jinsi itakavyoweza kuwasaidia sekta binafsi ya ndani. Lakini vile vile sekta binafsi yetu lazima tukubali Waheshimiwa Wawakilishi kama unamkamata mfanyabiashara mmoja mmoja hawatazidi kumi wenye uwezo wa kupambana na wa nje. Narudia kama utamtazama mmoja mmoja mfanyabiashara ndugu yangu Othman Masoud mtazame peke yake. Mfanyabiashara Hija mtazame peke yake. Uwezo wa kupambana na sekta binafsi za nje ni mdogo. Mimi nimewambia nimekutana nao Unguja, nimekutana nao Pemba nikawaambia tengenezeni kundi la pamoja. Mradi mkubwa mnauvamia mnakwenda kwa pamoja, mnashiriki kwa pamoja, lakini kila mmoja unamkuta huyu ana milioni mbili, milioni tatu dola, mradi unataka milioni kumi na tano dola. Nadhani watakuwa wamenisikia, na mimi na Mhe. Waziri wa Biashara kila tutakapokutana nao tutawakumbusha.

Jengine ambalo lililozungumzwa na Waheshimiwa wengi, bajeti ya maendeleo mwaka imepungua, kulikoni, nataka nieleze sababu mbili tu. La kwanza kuna miradi mikubwa ambayo imeanza kukamilika, kwa hivyo tunaanza kuiondoa sasa, mradi wa waya wa umeme na miradi mengine. Waheshimiwa watakapokuja watatoa maelezo miradi ambayo ilokuwa imekamilika katika maeneo yao. Lakini mwaka huu tumekuwa waangalifu kidogo tumesema tusiuingize mradi katika bajeti yetu kama hatuna *commitment* ya uhakika ya barua na ya mdomo kutoka kwa wafadhili. Nayo vile vile imetusaidia mpaka kuwa na bajeti ya uhakika.

Lakini ukija ukiichunguza *realistically* bajeti ya mwaka jana kile ambacho kilichotolewa kimekuwa ni kidogo kutoka kwa wafadhili. Ndio maana na sisi tukashtuka tukasema mwaka huu hapana. Tusiende tu nikisikia wafadhili wako tayari kutusaidia mradi huu aah, lakini jambo ambalo linatufurahisha Waheshimiwa Wawakilishi na Mhe. Spika, *contribution* ya Serikali katika bajeti ya maendeleo imeongezeka. Tumetoka bilioni 37 mpaka bilioni 47. Lengo letu Mhe. Spika, tunataka tuweze kujitegemea. Mhe. Rufai jana amezungumza kitu kizito sana, amesema huu utegemezi huu wa miradi wa fedha kutoka kwa wafadhili, na sasa hivi wamekuja na mtindo kwamba ili upate pesa sharti muoane ndoa ya jinsia moja.

Kwanza nataka niwahakikishie Wazanzibari sisi hatutokubali masharti hayo. Kama kuna nchi inataka kutupa msaada kwa sharti kwamba wanaume kwa wanaume waoane, wanawake kwa wanawake waoane tutamwambia msaada huo peleka katika nchi ambazo wanaotaka kufanya hivyo. Dini yetu ya kiislamu na dini zetu nyengine haziruhusu vitendo kama hivyo, huu ni uchafu haupaswi kuwepo miongoni mwetu. Kwa hivyo Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba tunataka tujitegemee na *Inshaallah* utafika muda tutajitegemea.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lililozungumziwa kwa kina, Waheshimiwa walitaka kujua sababu za mfumko wa bei kwa Zanzibar. Sababu ziko nyingi lakini naomba nizitaje kwa uchache tu kwa upande ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu.

La kwanza tunaagiza chakula kutoka nje sana badala kuzalisha ndani, na hasa mchele, unga na sukari. Lakini Mhe. Spika, na hapa vile vile nataka niwaombe Wazanzibari wenzangu tunachagua sana chakula. Mzanzibari ukimkaribisha bila ya wali anakwambia aa kapika nini huyu, hatuji-*encourage* tunapofanya hivyo maana yake

nini, maana yake huwasaidii wazalishaji wa muhogo, wazalishaji wa viazi wanaona hata wakizalisha hamnunui kwa wingi, kwa hivyo wanakuzalishieni kidogo halafu bei inakuwa kubwa. Lakini ndio kwa maana tumejikita katika uzalishaji wa mpunga. Nitakuja huko wengi walifikiria kwamba kilimo hatujakipa *priority*, tumejikita mwaka jana tumeeleza kwa kina Nerika tumeshazalisha mbegu za kutosha sasa, na zimeanza kusambazwa ili wananchi waanze kuvuna mpunga wa Nerika nitakuja huko. Kwa hivyo Mhe. Spika, tuhakikishe kwamba tunazalisha zaidi ndani hasa mazao yetu ya chakula ili tupunguze uagiziaji.

Lakini la pili sasa hivi kumetokea uharamia katika bahari kuu maeneo ambayo meli zinapita kwa hivyo umeongeza gharama, gharama za usafirishaji bidhaa zimeongezeka sasa hivi. Meli inabidi sasa zizunguke, kwa hivyo usafirishaji umeongeza nao, kwa hivyo mazao yanayoingia ndani yatakuwa ni ghali.

Lakini la tatu Mhe. Spika, nalo limezungumzwa sana na nitalizungumza umeme usiokuwa wa uhakika. Umeme sasa hivi upo mara umeshakatika maana yake nini, ukikatika wenzetu *production* wale hawawezi kuzalisha. Wakiwasha majenereta tayari gharama imekuwa kubwa zaidi, tutakuja huko na zoezi la kuwa na umeme wa uhakika.

Lakini la nne, kushuka kwa thamani ya shilingi. Mhe. Spika, yapo mengi ambayo yanachangia mfumko wa bei na sisi yanatuhusu. Lakini tukifikia pahala tukaweza kuzalisha chakula chetu, mimi ninaamini mfumko wa bei utaanza kupungua. Asilimia 51 ya mfumko wa bei wa Zanzibar unachangiwa na chakula. Mwaka jana tulifanya zoezi moja zuri sana, tukaangalia chakula kwa chakula tukagundua kwamba mfumko wa bei samaki nao wamechangia kuongeza mfumko wa bei, tukafanya kazi moja nzuri zaidi tukaenda *deep* zaidi, tukaona kwamba wenye hoteli kumbe hawanunui samaki kutoka nje wananunua samaki kutoka ndani asilimia mia moja. Kwa hivyo wavuvi wamepata bei, ndio hapa tulipomwambia Waziri wa Uwezeshaji anzisha vikundi vya uvuvi tunataka tuwe na boti sasa zinazokwenda chini huko. Samaki tunao wengi tunaweza tukawavua na wakatusaidia.

Mhe. Spika, jengine lililojitokeza zaidi na ninamshukuru sana Waziri wa Biashara na Viwanda, msukumo wa Serikali katika sekta ya viwanda. Nataka niwaambie hivi Serikali haifanyi biashara tena sasa hivi tumejitoa huko wengine walisema tulikuwa na kiwanda cha sukari, tulikuwa na kiwanda cha sigara, tulikuwa na kiwanda cha viatu tumejitoa huko. Kwa sababu mwanzo tulikuwa tunaambiwa sekta binafsi haiwezi ikakua kwa sababu Serikali imeshindana nayo. Serikali ikasema sasa inaacha kufanya biashara, sisi tutasimamia tu mazingira mazuri. Kwa hivyo Serikali katika hili tumejipanga nataka nieleze matatu.

La kwanza tumempa mpango Waziri wa Miundombinu maeneo yote ambayo Serikali ina mawazo ya kuweka viwanda apeleke barabara. Tunamshukuru sana amekwenda vizuri na ukiyatizama sasa hivi maeneo ambayo yanayokwenda na barabara utaanza kuona viwanda vinaanza kuja ili kuwe na *accessibility to the market*. Lakini vile vile tumepata *challenge* moja kubwa sana, bandari yetu ni ndogo kwa wawekezaji wanaotaka kuwekeza kwenye viwanda wanasema bandari yetu ni ndogo. Tuko katika utaratibu wa kuangalia jinsi gani tutapokuwa na bandari ya Mpiga Duri, ameeleza Mhe. Waziri wa Miundombinu.

Lakini la tatu tuna matatizo ya umeme, nitaeleza nikifika kwenye kile kifungu cha umeme, wafanyabiashara wengi wa viwanda wanasema hili ni tatizo sugu lazima tuanze kulitatua.

Lakini la nne ambalo sisi wenyewe tumeligundua, lazima kuwe kuna vivutio tofauti baina ya vivutio vya wawekezaji wa viwanda na vivutio vya wawekezaji wa hoteli, tunalifanyia kazi ili tuweze kutoa vivutio vizuri zaidi wenzetu wa viwanda waweze kuweka viwanda zaidi. Ninachoomba Waheshimiwa Wawakilishi tushirikiane. Wengi tunasafiri kwenda nje nikitoa mfano tu hivi karibuni somo yangu alikuwa Uingereza kule, ukipata nafasi zungumza na wafanyabiashara wa viwanda. Mhe. Mshimba alikuwa Spain huko Barcelona, omba wenyeji wako uzungumze na wafanyabiashara, wawekezaji katika sekta ya viwanda, hukatazwi, zungumza nao walete.

Mhe. Asha Bakari alikuwa China tuzungumzeni nao waje tusiwaachie Waziri wa Biashara na Waziri wa Fedha peke yao, sote tuna wajibu wa kufanya jukumu hilo. Tukifanya kwa pamoja mimi ninaamini kwamba Zanzibar itapata manufaa makubwa sana.

Jengine Mhe. Spika, ambalo limeulizwa kuwasaidia Watumishi wa sekta ya Afya. Nataka niseme kwamba hii ni hoja nzito na ni nzuri. Huwezi ukajivuna unatembea lakini siku utakayopindwa na mshipa wa ngiri utamtafuta mtu huyu wa sekta ya Afya akusaidie. Sote sisi hawa ni wenzetu, hatuna sababu tusisikilize maoni yao, maombi yao. Nataka niseme kwa kifupi Waziri wa Afya, Waziri wa Utumishi wa Umma watakapokuja wataeleza kwa kirefu zaidi. Mawaziri watatu tumekaa na watendaji wetu, Waziri wa Afya, Waziri wa Utumishi wa Umma na

Waziri ninaesimamia fedha, tumekaa tokea mwezi uliopita pamoja na madaktari wenyewe tumesikiliza hoja zao. Nataka nithubutu kusema baadhi ya hoja zao tumeanza kuzifanyia kazi katika bajeti hii inayoendelea, na nyengine zimo kwenye bajeti inayokuja.

Wenzetu hawa wa Afya wamekula kiapo hawa, lazima na sisi tukae pamoja tuweze kuwasaidia kwa kila hali na mali kwa mujibu wa uchumi wetu unavyokwenda. Na wala hawataki mambo makubwa. Nitamuomba sana Waziri wa Utumishi na Waziri wa Afya basi wayasimamie haya katika kuyafikisha kwa watendaji wapya.

Jengine ambalo limeulizwa Mhe. Spika na Wawakilishi wengi kidogo, walitaka kujua hii bakaa ya bilioni 5.9, Mhe. Rashid Seif aliweka vizuri zaidi jana akasema huku tayari kuna mambo hatujayatekeleza, hili bakaa la nini. Ni suala zuri kama Wawakilishi na wananchi kufahamu, vile vile naomba nitoe ufafanuzi Mhe. Spika, kwa ridhaa yako.

Kwani nataka niseme hivi, serikali haiwezi ikaamka haina kitu. Ni kosa kubwa sana serikali ikiamka halafu inajikuta mifuko mitupu na nyinyi mnaona mara unashitukia UAMSHO wamefanya fujo hapo huna kitu, umeamka huna kitu. Kwa hivyo, serikali kila siku lazima ikiamka asubuhi iwe ina kitu mfukoni, mimi mmenipa dhamana ya kuwa waziri msimamizi wa fedha ninahakikisha kila siku serikali ikiamka iwe ina kitu. Sasa terehe 1 Julai nikiamka mimi niwe nina kitu gain, nitakuwa ninazo shilingi 5.9 bilioni nimezipataje? Sasa naomba nieleze nimezipataje Mhe. Spika.

Sisi tunakusanya kodi kila siku, tarehe 1 nakusanya, tarehe 2, tarehe 3, tarehe 29 nakusanya na tarehe 30 nakusanya; mwezi huu wa sita kwa mujibu wa taratibu zetu ikifika tarehe 25 mpaka 28 tayari ninatakiwa niwe nimeshakamilisha kuzifunga, kwa hivyo, mapato nitakayokusanya tarehe 29, 27, 30 niyapeleke wapi, si ndio ninayotaka kuamka nay ohayo. Kwa hivyo, mapato haya nitaamka nayo tu sina ujanja, ndio maana kila bajeti utakuta mapato ambayo utaamka nayo. Sasa kwa utaratibu huu kila bajeti utakuta mapato utakayoamka nayo, huwa tunaangalia miaka ya nyuma *trend* ilikuwaje, mapato yaliyoingia tarehe 27, 28, 29 *trend* ilikuwaje na mwaka huu *trend* itakuwaje kulingana na mlolongo wa biashara zinazoingia.

Kwa hivyo, hili lisitupe matatizo *as long as* bajeti hii tunayokwenda nayo kuna pesa tuliamka nazo tukazitumia na hii tutaamka nazo zitatumiwa. Nilikuwa naomba Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu tufahamiane katika eneo hilo. Uvujaji wa mapato bado unaendelea tukusanye zaidi. Mimi nataka niwapongeze Waheshimiwa Wawakilishi wale wote wanaonisaidia.

Mhe. Spika, nimekaa nikafikiri sana nikaona kuna baadhi ya Wawakilishi humu ndani wana upeo mkubwa sana wa ukusanyaji wa mapato, nikasema mimi kama waziri hainizuii nikateuwa angalau wawili watatu tukakutana ikawa wananisaidia saidia, nimewaona humu ndani, tukakutana wiki mara moja ofisini kwangu kwa bajeti yangu na kunywa nao chai halafu tukawa tunajadili wakanisaidia.

Mhe. Spika, sijui kama nitahitaji ruhusa kutoka kwa Makamo wa Pili wa Rais, lakini kama nitahitaji ruhusa kutoka kwake ya kufanya hivyo namuomba Makamo wa Pili hapa aniruhusu. Nitawatafuta humu ndani ili wanisaidie.

Sasa hivi nataka nikwambie Mhe. Spika, hawa wakiniona mimi ninavamia Bandarini na *airport* nina askari kanzu wangu nimewaweka huko, tena nimewaweka askari kanzu kweli kikiingia chombo kina mafuta ya magendo wananipigia simu, kikiingia chombo kimeleta sukari haijalipa kodi wananipigia simu, kwa sababu waziri macho yako mawili lakini Watanzania, Wazanzibari *1.3 million multiply by 2* hayo ndipo macho yetu kwa nini tusiwatumie. Kwa hivyo mimi nasema kwamba wapo Waheshimiwa hapa nadhani watanisaidia katika suala zima hili la mapato na ninawaomba waendelee kunisaidia, nchi yetu, mapato yetu, kwa ajili yetu, kwa ajili ya shughuli zetu, tusaidianeni Waheshimiwa na mimi nitafarajika sana tukiwa tunasaidiana katika utaratibu ule ambao Mhe. Spika, nimekuomba kwa amani na utulivu.

Jengine ambalo limezungumzwa sana matumizi ya fedha yasiozingatia mahitaji, wengine walitumia lugya ya ubadhirifu. Nataka niseme hivi Mhe. Spika, niwaombe sana Waheshimiwa Mawaziri wenzangu tuwe karibu na Makatibu Wakuu wetu na watendaji wetu. Mimi ninaelewa tuko karibu nao sana, lakini twende nao karibu kidogo kuangalia hata mipango yetu ya kila mwezi, OC zetu tunapozitoa tunazipanga zitumike katika maeneo gani, *are we all satisfied?*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu alinambia waziri angalia *stationeries*, angalia safari, na mimi nawambia mawaziri wenzangu tuangalieni basi hayo na mambo mengine ili ule utaratibu wa kutumia kwa mujibu wa mahitaji ukienda vizuri mimi naamini sana sana tutafanikiwa. Lakini nataka niseme tu kwamba haya ndio Mhe. Rais sasa

anayafuatilia moja kwa moja, ile lugha tumeiita tu ya Bango kitita, lakini utaratibu wa kueleza umetumiaje fedha ambazo tumekupa sisi, ngojeni nikupeni hadithi moja.

Mhe. Rais alipoanza suala hili *quarter* ya kwanza alipoanza takriban wizara zote zimekwenda hatujapata pesa, hatujapata pesa, ukishakusema hatujapata pesa kutoka Hazina suala hakuna, *quarter* iliyomalizika hakuna wizara hata moja iliyosema hatujapata pesa. Kwa sababu zinaonekana pale kwenye bajeti ulizozipata zinaonekana sasa umezitumiaje? Hilo ndilo Mhe. Rais akisaidiana na mkamo wake wawili wanatuhoji sisi mmezitumiaje, pesa mmepata kwa nini mmezitumia huku wakati huku ndiko mlikoziombea. Nashukuru baada ya wizara zote baadae Mhe. Rais na Makamo wake wawili wanaiita Wizara ya Fedha sasa kuwaambia *budgetary implication* yake katika maeneo tofauti na nini au vipi twende. Kwa hivyo, hili kwa kweli ni *challenge* ambayo tutaichukua na tutaifanyia kazi.

Utegemezi wa Bajeti. Waheshimiwa wengi wamelisikitikia sana kwamba bado bajeti yetu ni tegemezi, tumetoka asilimia 24 mwaka jana mpaka asilimia 21. Lakini ukiangalia kwenye bajeti ile ya 294 bilioni ni shilingi 106 tu ndizo ambazo tumepata misaada nyengine tumekopa wenyewe. Nataka niseme ili tujitegemee lazima sisi wenyewe tukubali kujituma, tukubali kujituma ndugu zangu. Hata hivyo, tutahakikisha kila muda tunapunguza huu utegemezi.

Naomba nikwambieni ndugu zangu, wenzetu hawa kodi zao wanazotozwa wananchi wao ndizo zinazokuja kutusaidia sisi, wengine wameziweka katika sekta maalum, katika maeneo maalum, mnasikia Europe huko hali zao zinavyokwenda, tunamshukuru sana *DANIDA* ametusaidia katika kipindi kirefu kwenye eneo la madawa tumeshapata sijui niseme *yellow card* baada ya miaka mitatu ijayo anatupa jukumu lile wenyewe. Kwa hivyo, lazima tujiandae katika kuhudumia wananchi wetu kwa upande wa madawa. Kw a hivyo suala la utegemezi nduguzanguni si zuri hata kidogo, *measure* tunazozichukua hizi ndio tunataka kuanza kidogo kidogo kupunguza utegemezi ili tusije tukawa na utegemezi mkubwa kwa wakati mmoja.

Suala jengine bajeti haikulenga kuanzisha vyanzo vipya vya mapato. Nataka niseme tu Mhe. Spika, kwamba kuanzisha vyanzo vipya vya mapato haisaidii sana, kitakachosaidia hasa ni kupanua wigo wa *economic activities* lile ambalo mmelizungumza kwamba uvuvi wa Bahari Kuu hatujaugusa tupanue wigo huko tuuguse. Wenzetu watakwenda watavua basi zitapatikana pesa. Tutizame na wigo mwengine tupanue wigo huo hii ndio itakayotusaidia, lakini vyanzo vipya wengine mmesema kuna vyanzo vingi, kodi nyingi ndio kwa maana haisaidii lazima tuwe tuna vyanzo vichache lakini tuna *economic activities* nyingi ili ziweze kutusaidia.

Misamaha ya kodi imezungumzwa vile vile kwamba bado ni mikubwa. Nataka nikubaliane na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu misamaha ya kodi bado ni mikubwa lakini inapungua, hii misahama imetokana na sheria zetu wenyewe sheria hizi ambazo tunazoziwasilisha leo hapa zitasaidia nyengine kupunguza hiyo misamaha ya kodi.

Naomba kutoa mfano, mwaka 2008/2009 misamaha ya kodi ilikuwa ni shilingi 22 bilioni, mwaka 2009/2010 ilikuwa ni shilingi 27 bilioni, 2010/2011 mwaka jana ni shilingi 18 bilioni. Asilimia 51 ya misamaha ya kodi inakwenda kwa wawekezaji, asilimia 19 inakwenda kwa Mashirika ya Umma haya ndio yale mashirika ambayo tunapiganayo kelele, mashirika haya hayana mchango kwenye serikali lakini bado yanaomba misamaha ya kodi. Asilimia 16 misamaha ya kodi inakwenda kwenye Serikali Kuu na asilimia 14 inakwenda kwa Wafadhili na Taasisi Binafsi pamoja na sisi Waheshimiwa Wawakilishi na wengine ambao wana misamaha ya kodi. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba baadhi ya sheria zetu tukizifanyia marekebisho hii misamaha *automatic* itashuka.

Nitakupeni mfano mmoja mimi, leo mwekezaji anakuja anawekeza katika programu yake anaomba gari mbili au tatu, lakini cha kushangaza mwekezaji analeta gari zilizokwishatumika, gari ile tunamsamehe kodi lakini mwananchi wa kawaida akileta gari ile ile anatozwa kodi. Sasa hao nimeona hapatusaidii mwekezaji tutamwambia lete gari mpya ndio tukusamehe kodi, kama gari kuukuu toa kodi, hilo tunataka tulirekebishe.

Lakini la pili vifaa hivi ambavyo vinatumika sahani, gilasi, vikombe kila akileta anasamehewa kodi, hivi vitu vinatakiwa vitoke katika *operation cost* zako. Kwa hivyo, navyo hivi mimi nasema hapana tuviondoe.

Lakini la tatu ambalo mimi nataka tulifanye na hili nataka nilifanye mimi mwenyewe binafsi kila taasisi ambayo tutaipa misamaha ya kodi hasa wawekezaji tufuatilie tuone kweli *value for money*. Huwezi leo ukampa mtu msamaha wa kodi kwa sababu tu anajenga hoteli anakwambia nimeleta kontena 50 za *tiles*, kontena 50 za *tiles* unakwenda kufanyia hoteli gani hiyo! Huo mfano tu ninakupeni kwa sababu hatuna ule ufuatiliaji wa karibu kuona *value for money*. Kwa hivyo, hili nalo tunataka tulifanye *physically* tuone wale wote ambao tumewapa misamaha ya kodi haya yatatusaidia.

Jengine Mhe. Spika, hili wala sihitaji kusema sana, kupandisha kodi na ada. Takriban wazee wote wamesema, Wawakilishi wote wamesema lakini wengine walikuwa wanasema tujitegemee. Namshukuru sana Mhe. Haji Faki Shaali na Waheshimiwa wengine waliosaidia kutoa ufafanuzi wa haya, jamani kodi ya Bandari tumepiga kelele sana kodi ya Bandari hebu nambieni ndugu zangu tunaosafiri kwa meli nambieni ule ukweli mwananchi wa kawaida anasafiri mara ngapi kwa mwaka.

Jamani hatufanyi ile *critical analysis*, mwananchi wa kawaida anasafiri mara ngapi kwa meli hebu tuwaulizeni wananchi wetu, haizidi mara mbili wa kawaida nasema, anayesafiri mara kwa mara Mhe. Jaku Hashim mfanyabiashara huyo, mwananchi wa kawaida hasa muangalieni jamani anasafiri mara mbili tu pengine skuli zimefungwa anakuja kutizama watoto wake na jamaa zake mara mbili tu kwa mwaka, akisafiri mara mbili kwa mwaka maana yake anaichangia serikali yake shilingi 4,000 kwa wanaotoka Pemba, 1000 akirudi kule na akienda na mara ya pili hivyo hivyo shilingi 4,000 kwa mwaka.

Lakini hebu tuangalieni jamani, *I am not professional,* mimi si daktari, nimekwambieni angalieni ile picha wale ndio wanafunzi wana kompyuta wamekaa chini wamepinda migongo, leo tunataka kila wakati tuipatie Sekta ya Afya fedha nyingi za matibabu kama leo hatuoni shilingi 4,000 kupeleka kwenye madawati mtakuja kupeleka US$ 10,000 kwa Mhe. Waziri wa Afya kutibu mgongo. *I am serious*.

Mimi mwanangu niliyempa mume mwaka jana darasa la kwanza alikaa chini Skuli ya Vikokotoni. Aliporudi marehemu bibi yake anataka kumpiga sketi yote ina vumbi, akasema bibi mimi sichezei vumbi tunakaa chini, alipokuja kunambia marehemu bibi yake nikamwambia bwana mimi wa kwangu nitampelekea dawati, lakini walimu walinambia haiwezekani wa kwako akakaa juu ya dawati hawa wengine wakae chini. Angalieni akinamama wetu hawa wanavyofua sare za watoto kwa sababu wanakaa chini, shilingi ngapi wanatumia za sabuni kila mwezi kufua sare ya mtoto anayekaa chini.

Mimi nakuombeni sana ndugu zanguni, nakuombeni sana tuache hizi shilingi 2000, 1000 ziende tuje tufaidike na watoto wetu watoto wanatucheka leo, watoto wanatucheka wananambia baba angalia, baba na mama Baraza la Wawakilishi wanawakataza mababa na mamama zetu wasitoe shilingi 2000 ili sisi tuendelee kukaa chini, *that is unfair*.

Mimi ninakuombeni sana ndugu zanguni sisi ndio wenye watoto, sisi ndio tunaolipa, mimi nasema tulipeni ada hizi ili watoto wetu wakirudi nyumbani wawe wanacheka na sisi wana bashasha. Hebu jamani tujiulizeni, zinahitajika ngapi Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali nimekaa naye pale toka alipokuwa Mzee Ramadhani sasa hivi yupo Dr. Ali Juma Shamuhuna, madawati yanahitajika shilingi 27 bilioni ikiwa hatutazaliana tutakaa hapa hapa tulipo.

Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto leo amesema hapa tunaendelea kuzaliana tu, shilingi 27 bilioni mchango huu ambao tunausisitiza hapa utachangia shilingi bilioni mbili kwa mwaka, miaka 14 mpaka mmalize hiyo. Lakini imetupa faraja tumezungumza na baadhi ya wafadhili wakati tulipokuwa Arusha, Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali nilikuwa naye, Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, Waziri wa Ardhi, Makazi, Maji na Nishati, Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, wote nilikuwanao Arusha tunazichunga chunga US$ milioni nane na nusu ili zitupunguzie huu mzigo.

Lakini ndugu zanguni mimi nataka nikwambieni tu kwamba hawa watoto mtawafanya tuje tupasue viuno kwa kukaa chini itazameni ile picha. Mimi ninakuombeni sana katika eneo hili zangu nimeshatoa kabisa katika msaada wa kusaidia madawati.

Mhe. Spika, hoja nyengine ni ya mafuta. Serikali katika mafuta toka ilipopandisha ile kodi yake ya mafuta karibu miaka mnne au mitano sasa hivi hata ile thamani ya ile kodi imeshuka. Tunachoongeza hii shilingi 50 kuirejesha ile thamani tu sio kupandisha kodi, kuirejeshea *the value, you are taking back to its original value*, thamani yake unairejesha, lakini tumesema nazo zitatusaidia.

Mimi nasema nduguzangu jana hapa ameeleza baadhi ya waziri mmoja ni Mhe. Mansoor Yussuf Himid (Waziri asiyekuwa na wizara maalum) ameeleza kodi za Afrika Mashariki ni kubwa zaidi kuliko hata za kwetu, tumekuwa *very scientific* katika hili. Nakuombeni sana tuzikubalini hizi ili tuwasaidie wananchi wetu.

Mhe. Spika, Mhe. Amina Iddi Mabrouk alizungumzia kuhusu habari ya Kodi ya Majengo, alikuwa mkali sana jana dada yangu. Kodi ya Majengo tutaleta sheria hapa, kulikuwa kuna upungufu mmoja Mhe. Spika, katika sheria ile ya majengo imeeleza kwamba awepo mtathmini wa mejengo, kwa upande wa Zanzibar hakuna sheria

ya mtathmini, mngeanza kutozwa kodi ya majengo mwananchi angeweza kukupelekeni Mahkamani, mtathmini yuko wapi na nyinyi kwenye sheria yenu mlisema? Kwa hivyo, tumeshashirikiana wizara yangu pamoja na Wizara ya Ardhi, Makazi, Maji na Nishati tumeshaandaa *draft* ya *valuer*.

Namshukuru sana Mwanasheria Mkuu alitupatia kopi za *valuer* za sheria za *valuer* kutoka nchi mbali mbali Australia, Kenya, anazikumbuka alizonipatia, Quiz land zote nimekuwanazo tumefanya kazi hiyo vizuri ni matarajio yangu kwamba sheria hii itakuja haraka iwezekanavyo kupitia Wizara ya Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban ili tuweze kodi hii nayo tuanze kuifanyia kazi.

Bajeti haikutoa kipaumbele kuhusu kilimo. Mhe. Spika, mimi nataka niseme programu zetu za mwakajana zinaendelea bado, pembejeo zitaendelea kama kawaida, tumenunua baadhi ya vifaa vya kilimo ambavyo tumeahidi, Waziri wa Kilimo na Maliasili atakapokuja ataeleza zaidi. Lakini nasema tu wale ambao wamesema kwamba hatujakipa kipaumbele labda wameangalia bajeti ya *development* ya mwaka jana na bajeti ya *development* ya mwaka huu kwenye kilimo. Tulichokifanya ni nini? Mwaka jana pembejeo tumeziweka kwenye *development*, lakini pembejeo ni *recurrent*, mwaka huu tumetoa *2 billion* tumezipeleka kwenye *recurrent.* Wao wenyewe nao wametoa *300 million* kwa hivyo wana *2.3 billion* za pembejeo ziko kwenye *recurrent.* Kwa hivyo, bado kilimo tunakipa msukumo zaidi kwa sababu asilimia 42 ya pato letu la taifa tunachangiwa na kilimo. Kwa hivyo, nduguzanguni tukiisikiliza vizuri zaidi Bajeti ya Wizara ya Kilimo mtaweza kuona.

Lakini nataka nikwambieni katika baadhi ya sekta kama ya kilimo tusiisome kilimo peke yake. Nitakupeni mfano mmoja, Waziri wa Ardhi kuna baadhi ya maeneo ya kilimo anayapelekea umeme, anayapelekea maji; Waziri wa Vikosi mkija mkisikiliza mpango wake kwenye Kikosi cha JKU mtaona kuna Sekta ya Kilimo pale, kwenye mafunzo mtaona Sekta ya Kilimo pale, hizi zote ni bajeti za kilimo. Kwa hivyo uwezeshaji vile vile nay eye, kuna sekta pale kuna pesa anazipeleka kwenye Sekta ya Kilimo, sasa zote hizi ukijumlisha utaona umuhimu wa Sekta ya Kilimo.

Kuna moja hili Mhe. Spika, namalizia sasa, Uwiyano baina ya Walimu na Wanafunzi. Mhe. Ashur Sharif Alialikuwa mkali kidogo na hasa alikuwa mkali kwa ile *data* waliyoisema wote, nataka nisaidie tu kidogo. Kama nilivyosema mwanzo mimi kama takwimu ina matatizo sitokuleteeni, naomba nisome takwimu Mhe. Spika. Wanafunzi wa Zanzibar *primary* na *secondary* na ndio ile *figure* yangu nilivyokuwa ninai-*refer* narudia, Wanafunzi wote walioko Zanzibar *primary* na *secondary*, *public and private schools* 319,543; walimu tulionao *primary and secondary*, *public and private schools* ni walimu 11,722 hawa wamepatikana kutokana na kwenye *pay roll*, serikalini wana pay roll yao na *private sector* nako wana *pay roll* zao; ukigawa hiyo Mhe. Spika, ndio utapata walimu kwa wanafunzi ratio ni *one to twenty seven* si takwimu zangu ni takwimu zetu wenyewe.

Lakini nakubaliana na tatizo alilolisema kwamba tatizo letu tuna *class room ratio* na wanafunzi hilo lipo, la kwanza tunalo wanafunzi wengi kwenye darasa tuna upungufu wa madarasa. Lakini tuna tatizo jengine Mhe. Spika, la walimu wa sayansi, ukitizama mwalimu wa hesabu *vis-as-vis* wanafunzi unaweza ukakuta *one to one hundred* na haya ndio mambao tuliyoyaeleza safari hii katika Mfuko wa Mikopo yako wazi kabisa. Tumeya-*address* katika Utumishi wa Umma kwa ajili ya mishahara wazi kabisa, tumeshampa pesa katika mwaka huu aajiri walimu 500 wa sayansi, ataeleza mwenyewe kapata 200 na kitu hawapo, kama hawapo maana yake nini tuwafunze, tuanzishe huku tuwatengeneze na sio kutengenezwa katika Mfuko wa Mikopo tuanze *from the primary* kwenye mizizi huku, hilo ndio lengo letu Mhe. Spika.

Kwa hivyo, hiyo takwimu niliyompa dada yangu Mheshimiwa na Waheshimiwa wengine ni halali kabisa, *it is authentic.*

Jengine kuwa na chanzo chetu cha umeme. Waheshimiwa Wajumbe wengi wametilia mkazo kuwa na chanzo chetu cha umeme. Na wakasema *soon is better*. Ninataka niwahakikishie kwamba chungu kipo jikoni kinatokota. Wapo wawekezaji wengi sana wameshaonesha nia ya kuekeza katika umeme hapa Zanzibar.

Tatizo letu lilikuwa ni moja, tunaelewa Wazanzibari tunataka umeme wa aina gani? hilo ndilo tatizo letu. Kuna umeme wa taka, jua, upepo, mawimbi ya bahari, diesel, kuna umeme unaotolewa katika *power pug*, tunataka umeme rahisi.

La kwanza tunataka umeme *affordable and sustainable*. Umeme rahisi ambao utakuwa ni endelevu. Ukisema unataka umeme wa diesel, wakati diesel ikipanda huko na wewe unapandisha. Subirini tumeshawapa kazi wenzetu wa *European Union*, wameshatengeneza *study* ndogo, wameshatupa ripoti yao.

Mambo yapo mazuri tu na wawezekezaji wapo mikononi. Tukimaliza hili Mwenyezi Mungu akitujaalia katika miezi mitatu inayokuja ninanusanusa mimi na Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban, miezi mitatu inayokuja hii mambo yataanza kuonekana. Tuombe Mwenyezi Mungu lakini hilo ndilo litakalotuokoa sisi Wazanzibari kuwa na viwanda (*Makofi*).

Mhe. Spika, la mwisho kabla ya sijamalizia kwa shukurani yapo mengi nasema mengi nimeyachukua, sitoweza kila mmoja aliyechangia kwa sababu ni 256.

Lakini la mwisho Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, naomba hili niwe *specific* kidogo. Alilalamika kidogo kuhusu uuzaji wa majengo ya serikali. Mimi kama Omar Yussuf Mzee ambaye Mhe. Rais amenipa dhamana ya kusimamia fedha za nchi na mali ya nchi hii, sitouza kiholela ninataka muniamini.

Lakini twende mbali kidogo. Tuangalie majukumu ya Baraza la Wawakilishi na *Executive* kwa maana serikali. Kuuza na kununua ni jukumu la serikali. Tusitake kwenda mbali sana. Sisi wajumbe wa Baraza lako tukufu tusimamie taratibu na sheria zilizotumika katika kuuza.

Hapo mtakubaliana na mimi, mukija mukiniambia Omar Yussuf Mzee umeuza jengo hili, tuambie umetumia sheria gani na utaratibu tueleze, nitazieleza. Lakini ukiiambia serikali isiuze mpaka uje ukione wewe aah! Sasa hapo tunaingiliana kwenye majukumu na mimi nisingependa kwenda huko.

Tusimamie taratibu na sheria, na tuelewe anayeuza ni nani? Isiwe kila wizara inauza? Sheria ipo muuzaji anatakiwa awe ni nani? Leo Wizara ya Utawala Bora wakiwa na jengo, Kilimo wakiwa na jengo wakiuza, Nishati wakiwa na jengo wakauze. Sasa huu ni utaratibu mbovu ambao nyinyi ndio munatakiwa muusimamie. Hapo tutafahamiana, lakini kusema tusiuze sisi mpaka mikataba inuswenuswe. Sasa mimi hapo ninasema Mhe. Spika, *with due respect, I respect* wawakilishi wangu wote chini ya moyo wangu. Lakini tusiingie kwenye majukumu. Hizi ni taasisi tatu nzito na kila taasisi ina majukumu yake. Kuna *executive* na sisi hapa tunaitwa *parliamentary* na halafu kuna wale watu wa sheria.

Kila mmoja ana jukumu lake. Mhe. Spika, mwisho ninataka nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Rais kwa kuendelea kuniamini na kuniruhusu bado niendelee na nipumue katika nafasi hii pamoja na wasaidizi wake wawili, pamoja na wawakilishi na Wazanzibari wote, nitakutumikieni kwa kadri ya uwezo wangu. Na popote ambapo nitakapokosea basi naomba muje munifahamishe na munieleweshe.

Lakini Mhe. Spika, vile vile nimpongeze na nimshukuru sana mke wangu Narman Nassor Mohamed. Kama si huyu lazima nikubali leo nisingesimama hapa. Siku tatu nzima alikuwa katika redio anasikiliza, anatuangalia, nikirudi ananipa nasaha nzuri, mawazo mazuri, leo nimesimama hapa lazima nimshukuru. Namshukuru vile vile kwa kunilelea watoto mpaka leo tunafika hatua ya kuozesha *alhamdullilah*. (Makofi).

Mhe. Spika, namalizia kwa kusema kwamba amani ni muhimu bila ya amani uchumi wetu hautoweza kuendelea. Sitaki niseme mengi katika suala la mjadala wa Katiba. Mwanasheria Mkuu ameeleza mengi jana wala sitaki nitie doa.

Nasema muda ukifika tutoe maoni yetu. Maoni tunayo mengi. Hata mimi nina maoni mengi na nitakwenda kutoa maoni yangu lakini tudumishe amani ya Wazanzibari.

Nilikwenda mkutano wa mwaka jana wa ADB Mhe. Spika, kule Ureno nikatetea sana mkutano ule ufanyike Tanzania mwaka huu, *alhamdullilah* tumefanikiwa umefanyika Tanzania mwezi wa Mei. Lengo langu ilikuwa ni kuitangaza Zanzibar vile vile watalii waje.

Kipindi kile tupo Arusha ndio kipindi kilichotokea matatizo. Tulitarajia tungepata kama watalii mia tano hivi, bahati mbaya kwa sababu wengi walinijia wakaniambia *we are sorry, we have to cancel to Zanzibar*. Nilijaribu kuwanasihi kuwa siku mbili tatu yatakwisha lakini mengi ndio mgeni. Naomba sana ndugu zangu Wazanzibari, sote tunaipenda Zanzibar yetu, hakuna aliyekuwa haipendi Zanzibar. Amani ni kitu muhimu sana.

Pili tujitume Wazanzibari. Tukijituma Wazanzibari mimi ninaamini sana uchumi wetu utakua, wananchi wetu wataweza kuwa na matumizi mazuri na hatimaye mabadiliko yataonekana. Leo ukenda nyumba nyingi sana wananchi wamevunja nyumba zao wameanza kujenga kwa matofali, wengine wameezeka kwa mabati *alhamdullilah* tunakwenda vizuri.

Lakini la tatu Mhe. Spika, naomba kumalizie kwa kusema kwamba tuvipeni nguvu sana vyakuka vyetu tunavyozalisha ndani kwa kula. Tukivipa nguvu kwa kula wananchi watapata nguvu za kuzalisha na hatimaye uagiziaji huu wa mchele utapungua, ukipungua na mfumko wa bei vile vile utapungua.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa heshima na taadhima, naomba sasa kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa niaba yenu ninataka nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kutoa ufafanuzi katika majumuisho yake juu ya hoja aliyoiwasilisha mapema tarehe 13 Juni, 2012 na michango kuanza tarehe 18 Juni, 2012 na hadi hii leo ametufanyia majumuisho hivi asubuhi.

Nichukue nafasi hii kumshukuru sana kwa niaba yeuu ambaye amekuwa mtulivu katika kutoa majibu na pia kuahidi kwamba atawatumikia kwa nguvu zote. Lakini wakati huo huo akiahidi kwamba yale ambayo hakuyatolea ufafanuzi tuelewe kwamba ameyachukua na kuyafanyia kazi.

Baada ya hapo Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya wenyeviti wa kamati nimemsikiliza sana Mhe. Waziri alipokuwa akitoa ufafanuzi, sikuwemo humu ndani kwa sababu nilikuwa ninakamilisha taarifa yangu ambayo nitaisoma hapo baadae baada ya *speech* ya Mhe. Waziri ya jioni.

Mhe. Spika, tulikubaliana na Mhe. Waziri katika suala la ada ya bandari katika kikao cha kamati. Katika ufafanuzi alioutoa nimemsikia vizuri na akamsifu sana Mhe. Haji Faki Shaali kwa kutoa ufafanuzi wa kiuchumi, ingawa mimi ufafanuzi alioutoa Mhe. Haji Faki Shaali wa kiuchumi ninauona katika mazingira ya kwetu Zanzibar hauko sahihi, yeye alikwenda katika mtandao akaangalia ukuaji wa uchumi, pato na taifa na deni, na akatoa mfano katika nchi ambazo, samahani Mhe. Spika, nishakufahamu ninakuja katika hiyo hoja kwa vile ninajenga hiyo hoja yangu.

Mhe. Spika: Kuhusu utaratibu chini ya kifungu kipi cha Kanuni.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Samahani sana sikuangalia kifungu cha Kanuni, lakini kwa kuwa tunapitisha bajeti ya serikali na tukiunga mkono, ina maana yote aliyoyasema Mhe. Waziri tumeyakubali. Lakini sasa kuna mambo ambayo tumekubaliana katika kamati na yeye alikubali kwamba atayaondoa.

Sasa ndio maana ninajenga hoja katika suala la ada ya bandari hatukukubaliana ada ya bandari tuliyokubaliana ni ya kwendea Dar es Salaam, lakini ya kwendea Pemba hatukuikubali, kwa hivyo tukishaipitisha hapa ina maana ndio imetoka.

Sasa ndio maana nikasema Mhe. Spika, naomba univumilie kwamba hili suala samahani sikuwahi kuangalia Kanuni lakini kwa busara ili hii bajeti yetu iwe nzuri na iende kwa mashirikiano ya pamoja na kuikubali kwa roho safi Mhe. Spika, naomba nitoe ufafanuzi mdogo.

Kwa watu wanaokwenda Pemba Mhe. Spika, hakuna mtu anayekwenda peke yake. Mtu anayekwenda Pemba anaondoka na watoto watano sita na ushahidi mzuri katika meli iliyozama. Leo tunaposema shilingi elfu moja sio kubwa, kwa Mpemba anayesafiri na watoto wake ni kubwa.

Mhe. Spika, mimi Jimbo langu ni la Kwamtipura, wananchi wangu mtu anatoka Darajabovu kwa mguu anakwenda bandarini hana pesa ya daladala. Sasa tunaposema shilingi elfu moja ni pesa kidogo kwa vigezo vya Mhe. Haji Faki Shaali kwa kuwa yeye anazipata, sawa ni kidogo lakini kwa mwananchi mnyonge anayeuza maandazi ni nyingi. Tunaomba kodi ya bandari inayokwenda Pemba ifutwe. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Kuhusu utaratibu. Bado Mhe. Hamza anasema makubaliano ilikuwa kodi ya bandari iondolewe. Mimi sitaki kile mulichokubaliana huko, ninataka kile ambacho kimezungumzwa hapa na kutolewa maelezo. Maelezo tumeyasikia sote kwa upana kabisa.

Tukija namna hii tutakuwa tunavunja utaratibu wa majadiliano kwamba tumejadili mpaka mwisho na ufafanuzi ukatolewa tena kwa msaada pamoja na Mhe. Waziri. Tukumbuke kwamba jambo hili ilikuwa tumalize jana,

lakini tukasema ni vizuri Waheshimiwa Mawaziri wote wale waliomba wasaidie katika kujibu masuala ya hapa na pale, wakafanya hivyo.

Tukasema tuchukue muda kidogo, leo ilikuwa tuanze mswada ili sasa tumpe Mhe. Waziri aweze kutoa majibu. Majibu ameshatoa na ninadhani tumefahamu. Tukiendeleza mjadala tena baada ya majibu haya, inatokezea sana kuna jambo ndani ya kamati mumelipendekeza lakini hapa ndani likabadilika kutokana na michango, kwa sababu kamati ilikuwa inafanya kwa niaba ya Baraza kwa kiasi fulani, lakini uamuzi halisi unatoka hapa Barazani.

Sasa kwa kuwa maelezo yameshatoka tusifungue mjadala tena juu ya hili. Ndio mtiririko wa mijadala yetu kwa Kanuni zetu zilivyo tunakwenda kwa utaratibu huu.

Mhe. Hamza nikiombe kitabu chako cha Kanuni na niwahoji Waheshimiwa Wajumbe. Mhe. Hamza ukae.

(Hoja ilitolewa na kukubaliwa)

Mhe. Spika: Nichukue nafasi hii tena Waheshimiwa Wajumbe kuukubali mpango huu wa maendeleo pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka huu.

Baada ya hapa ilikuwa moja kwa moja hii haina kupitisha vifungu kama kawaida ni wizara kwa wizara ndio tunapitisha vifungu hapo baadae wizara zitakapofika.

Kwa hivyo, kwa mujibu wa taratibu ilikuwa sasa tuwasilishe mswada, lakini Mhe. Waziri amefanya kazi kubwa, akiniambia kama yupo tayari kuwasilisha hivi sasa ninasema sawa. Lakini mimi ninadhani tumpe muda akakae ajitayarishe ili jioni aje kuwasilisha mswada.

Lakini nilitaka katika kazi ya jioni ili iwe nyepesi niwarudishe Waheshimwa Wajumbe kwenye Kanuni zetu toleo la mwaka 2012 chini ya ibara ya 83, na moja kwa moja twende kwenye ibara ndogo ya 83 na 83 (4).

Kwa hivyo ibara ya 83 (3) inaelezea kama hivi ifuatavyo;

> “Bila ya kuathiri fasili ya 2 ya Kanuni hii mswada wa dharura uliwasilishwa kwenye Baraza kwa masharti ya Kanuni ya 80 hizi unaweza kusomwa kwa mara ya kwanza, kwa mara ya pili na mara ya tatu ndani ya mkutano huo huo mmoja wa Baraza”.

Kanuni hii nimeona niiseme kwa sababu kwa mujibu tulivyoanza kushughulika na Kanuni hii marekebisho yake, tulikubaliana miswada iwe inawasilishwa kwa utaratibu wa kusomwa mara ya kwanza, mara ya pili na mara ya tatu.

Mara ya kwanza inategemewa iwe inawasilishwa kwenye mkutano ule uliomalizika lakini hii ni bajeti, na kwa kawaida bajeti inakuwa ni siri isipokuwa kwa kamati tu zinazohusika ndizo ambazo hupata nafasi ya kuona mapema kabla ya kuwasilishwa ndani ya Baraza.

Kwa hivyo isingekuwa vizuri na wala sio sahihi kuweza kuwasilisha kipindi kile wakati baadhi ya mambo hayajawa tayari na ule usiri utakuwa haupo. Tulipomkaribisha Mhe. Waziri wa Fedha aliingia mwisho na mkoba wake hapa na bado ulikuwa haujafunguliwa, ukaanza kufunguliwa hapa wakati huo kamati imeshakaa na imeshazungumza.

Mswada huu unakuwa kama vile wa dharura. Ukenda kwenye kifungu cha 83 (4) kinasema hivi:

> “Mswada uliosomwa kwa mara ya kwanza utapelekwa na Spika kwenye kamati husika na kamati hiyo itauchunguza mswada huo mapema iwezekanavyo isipokuwa mswada wa dharura unaweza kupelekwa kunako kamati husika hata kama haujasomwa kwa mara ya kwanza”.

Sasa mswada huu hatukuwahi kuusoma kwa mara ya kwanza. Usomwaji wake kwa mara ya kwanza ni pale ilipowasilishwa hati Barazani asubuhi ya leo na usomaji wa mara pili utakuwa ni pale atakapouwasilisha kwa ajili ya mjadala, mara ya tatu pale utakapopitishwa mswada huo basi.

Shughuli hiyo yote inafanyika katika mkutano huu na kwa bahati katika siku ya kikao cha leo. Kikao cha asububi aliwasilisha hati, jioni anawasilisha rasmi na hatimaye mjadala unaanza hapo, utakuwa ni usomaji wa mara ya pili na baadae utakuwa unapitishwa.

Kwa hivyo tuelewe kwamba kwa dharura ya mswada huu ambayo haikuwa inawezekana kuusoma kwa mara ya kwanza katika mkutano uliopita, kusema kutakuwa na mswada huu wa namna ya hii kwa sababu matayarisho yalikuwa bado hayajakamilika.

Ndio mswada unaruhusika kuweza kusomwa kwa mara ya kwanza, ya pili na ya tatu katika mkutano mmoja. Nilitaka niseme hayo, huo ndio utaratibu wa Kanuni zetu baada ya marekebisho tuliyofanya kwenye mkutano uliopita.

Sasa Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo mswada huu utawasilishwa na kusomwa kwa mara ya pili jioni ili wajumbe muujadili, mswada ambao unahusiana na bajeti hii muliyopitisha punde ili ikifika Julai 1 iwe kuna sheria ambayo tayari imetiwa saini na Mhe. Rais kuwawezesha kukusanya kodi ili bajeti hii itekelezeke ipasavyo.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo naomba sasa tusitishe shughuli zetu hadi jioni saa 11.00 jioni leo.

(Saa 6.18 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Mswada wa Sheria ya Fedha Usimamizi wa Mapato ya 2012

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Mswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2012.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza letu, kwa kuupitia kifungu kwa kifungu mswada huu, kutoa ushauri na maelekezo ya namna ya kuimarisha na hatimaye kuidhinisha mswada huu uwasilishwe Barazani. Kwa kamati hii nina dhima ya kutoa shukrani maalum kwa Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa uongozi wake imara namshukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, madhumuni na sababu za mswada huu zimeoneshwa kwa kirefu katika mswada wenyewe, naamini Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wamepata muda wa kuupitia kwa makini kama ilivyokawaida yao kwa kifupi.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu unakusudia kufanya marekebisho katika sheria zilizotajwa za kodi na fedha, ili kuimarisha ufanisi, udhibiti ukusanyaji wa mapato ya serikali kwa kupitia utekelezaji wa sheria hii. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni hizi zifuatazo.

1. Sheria ya kodi ya ongezeko la thamani nambari 4 ya mwaka 1998.
2. Sheria ya ushuri wa stempu nambari 6 ya mwaka 1996.
3. Sheria ya kodi ya hoteli nambari 1 ya mwaka 1995.
4. Sheria ya ushuru wa mafuta ya petroli nambari 7 ya mwaka 2001.
5. Sheria ya ada za bandari nambari 2 ya mwaka 1999.
6. Sheria ya usimamizi na uratibu wa kodi nambari 7 ya mwaka 2009.
7. Sheria ya bodi ya mapato ya Zanzibar.
8. Sheria ya mfuko wa hifadhi ya jamii nambari 7 ya mwaka 1996.
9. Sheria ya mafunzo ya amali nambari 8 ya mwaka 2006.
10. Sheria ya ufutaji vitega uchumi nambari 8 ya mwaka 2004.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu wa sheria umegawika katika Sehemu 10, ambapo Sehemu ya Kwanza ya mswada inahusiana na vifungu vya utangulizi, ambavyo vinaelezea jina la sheria na utumiaji wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya Pili ya mswada inahusiana na marekebisho ya sheria ya kodi ya ongezeko la thamani nambari 4 ya mwaka 1998, ambapo umefanyiwa marekebisho yafuatayo.

Kwanza, kifungu cha 2 kwa kuweka tafsiri ya maneno ‘hati ya usajili’ na kurekebisha tafsiri ya maneno thamani ya kodi.

Pili, kifungu 7(4) kimefutwa na kuwekwa kifungu kipya, ili kutanua wigo katika ukusanyaji wa kodi kutokana na huduma za simu na huduma nyenginezo Zanzibar.

Tatu, kifungu cha 13 kimerekebishwa kwa kuondoa maneno ‘kifungu hiki’ na kuweka kifungu cha 4 cha sheria ya usimamizi wa kodi.

Nne, kifungu cha 14 kimerekebishwa kwa kuondoa maneno ‘kifungu cha 13’ ambacho tayari kimeshafutwa katika sheria hiyo na kuweka kifungu cha 4 cha sheria ya usimamizi wa kodi.

Tano, kifungu cha 16 kimerekebishwa na kuweka kifungu kipya cha 4 na 5 na kijifungu cha (5) kusomeka kijifungu cha (6) kwa lengo la kuweka utaratibu katika kodi katika manunuzi.

Sita, kifungu cha 66 kwa kufuta maneno ‘kifungu cha 43 na kuweka maneno ‘sehemu ya nne ya sheria ya usimamizi wa kodi’.

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu ya mswada inafanyiwa marekebisho sheria ya kodi ya stempu nambari 6 ya mwaka 1996 katika sehemu zifuatazo.

Kwanza, kumewekwa maelezo kuhusiana na sera za Bima ili kuweza kusimamia vyema ukusanyaji wa mapato katika mikataba ya Bima na makubaliano mengine.

Pili, kifungu cha tatu kwa kuongeza vijifungu (6) na (7) ambavyo vitampa waziri mamlaka ya kuteuwa mawakala wa ukusanyaji wa kodi ya stempu.

Tatu, kijifungu cha (12) kwa kufanyia marekebisho kijifungu cha (2) (c) kinachotoa fursa ya misamaha ya kodi ya stempu kwa sheria mbali mbali.

Nne, kwa kuweka kijifungu kipya cha (13) (d) ili kuweka wazi ukusanyaji wa kodi ya stempu katika huduma na bidhaa.

Tano, kwa kuondoa maelezo ya vifungu ambavyo vimeshafutwa katika sheria hii vilivyojitokeza katika kifungu cha 15.

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya Nne ya mshwada inaifanyia marekebisho sheria ya kodi ya hoteli nambari 1 ya mwaka 1995 kama ifuatavyo.

Kwanza kufuta maneno ‘kifungu cha 14’ yaliyojitokeza katika tafsiri ya neno ‘kanuni’ na kuweka maelezo kifungu cha 66 cha sheria ya usimamizi wa kodi.

Pili, kwa kufuta maneno ‘asilimia 15’ yaliyojitokeza katika kifungu cha 3(1) na kuweka maneno ‘asilimia 18’.

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya Tano ya mswada inaweka marekebisho ya sheria ya mafuta nambari 7 ya mwaka 2001, kwa kuweka kifungu kipya cha 15(A) kuhusiana na mafuta ya magendo, ambacho kimeongeza faini kuwa shilingi milioni moja hadi shilingi milioni ishirini.

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya Sita ya mswada inaweka marekebisho ya sheria ya ada ya bandari nambari 2 ya mwaka 1999 kwa kuweka utaratibu wa kutoza ada ya usalama wa uwanja wa ndege na kufuta kifungu cha 14, ambacho kwa sasa kimeingizwa katika sheria ya usimamizi wa kodi.

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya Saba ya mswada inafanyia marekebisho sheria sheria ya usimamizi wa kodi nambari 7 ya mwaka 2009 kama ifuatavyo.

Kwanza, kuweka tafsiri ya maneno ‘kipindi cha hesabu’.

Pili, kuweka kijifungu (2) katika kifungu cha 45 ili kuwa na utaratibu wa kugomboa kodi na.

Tatu, kijifungu cha (57) kwa kuondoa mamlaka ya kusamehe riba.

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya Nane ya mswada inafanya marekebisho katika sheria ya bodi ya mapato nambari 7 ya mwaka 1996, kwa kufanyia marekebisho yafuatayo.

Kwanza, kwa kuongeza kazi za kushauri kuhusu sera ya mapato na usimamizi wa kodi katika kifungu cha 5.

Pili, kifungu cha 9 kwa kuondoa 'mjumbe yeyote' na kuweka maneno 'kamati ya bodi'.

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya Tisa ya mswada inafanyia marekebisho sheria ya mfuko wa hifadhi ya jamii nambari 2 ya mwaka 2005 kwa kuondoa msamaha wa kodi kwa mapato mengine yaliyo chini ya mfuko huo.

Mhe. Mwenyekiti Sehemu ya Kumi na mswada inaifanyia marekebisho sheria ya mafunzo ya amali nambari 8 ya mwaka 2006 kwa kuongeza vijifungu vya (4) na (5) katika kifungu cha 15 ili kutoa msamaha kwa idara za serikali na taasisi ambazo haziendeshwi kibiashara na ambazo zinagharamiwa zaidi kupitia mfuko mkuu wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya Kumi na Moja ya mswada inafanyia marekebisho sheria ya ukuzaji vitega uchumi nambari 11 ya mwaka 2004, katika kifungu cha 19 kwa kupunguza muda wa msamaha wa kodi za ardhi kwa wawekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kimsingi walikwishakubaliana na mapendekezo ya msingi ya mswada huu, wakati wa kuidhinisha mpango wa maendeleo na mikakati ya mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka 2012/2013. Sasa kwa ruhusa yako na kwa ridhaa yako, naomba wapitie na kukubali mapendekezo ya mswada wa sheria ya fedha ya mwaka 2012.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi).*

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza Kuhusu Mswada wa Sheria za Kutoza Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali naMambo Mengine Yanayohusiana na Hayo

Mhe. Hamza Hassan Juma: (Mwenyekiti wa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu): Mhe. Mwenyekiti, kwanza hatuna budi kwa sote kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa mara nyengine tena kutukutanisha hapa jioni hii, tukiwa wazima kabisa wenye afya njema kuja kujadili, mipango ya maendeleo ya nchi yetu.

Vile vile nimesimama hapa kutoa maoni ya kamati ya kudumu ya Baraza la Wawakilishi, kamati ya wenyeviti ambayo inahusu mswada wa sheria ya kutoza kodi, unaohusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya serikali, pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuingia katika kutoa maoni nataka nianze, pamoja na yale marekebisho aliyosema au aliyoyataja swahibu wangu Mhe. Waziri na mimi ilikuwa kidogo nataka niongezee baadhi ya machache, ambayo naamini watakao andaa mswada huu wa sheria hapo baadae, watajaribu kuunganisha yale aliyoyasema Mhe. Waziri, pamoja na haya ambayo ninayoyasema mimi.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 6 kwenye jina la mswada katika mstari wa tatu kutoka juu, kuna neno 'uthibiti', tumefanya marekebisho lisomeke udhibiti.

Vile vile ukurasa wa 70 wa mswada huu Sehemu ya Pili, marekebisho ya sheria ya kodi ya ongezeko la thamani nambari 4 ya mwaka 1998, katika kifungu cha 3(b) mstari wa kwanza, maneno 'thamani ya kodi' yasomeke 'thamani ya kutoza kodi'.

Aidha, katika kifungu hicho cha 3(b), mstari wa kwanza kutoka juu neno la mwisho, 'baada' lisomeke 'badala'. Hayo ni mambo ya *typing error*.

Lakini vile vile nikiendelea ukurasa wa 71 wa mswada wetu huu kifungu cha 7(b) cha mswada, kinachorekebisha kijifungu cha (5) cha kifungu cha 16 cha sheria mama katika mstari wa tatu, neno 'atajaaliwa' lisomeke 'atahesabiwa'.

Vile vile Sehemu ya Saba ya mswada marekebisho ya usimamizi wa kodi nambari 7 ya mwaka 2009 ukurasa wa 75, kifungu 26(b) cha mswada kinachoongeza kijifungu kipya cha kifungu cha 45(4) cha sheria mama katika mstari wa pili kutoka juu, neno 'hichi' lisomeke 'hiki'.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia katika marekebisho ya mswada huu Sehemu ya 11 marekebisho ya sheria ya ukuzaji vitega uchumi nambari 11 ya mwaka 2004, ukurasa wa 76, kifungu cha 35 cha mswada. Mstari wa kwanza kutoka juu, maneno 'sheria ya ukuzaji uchumi' yasomeke 'sheria ya ukuzaji vitega uchumi'.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 36(b) cha mswada kinachorekebisha kijifungu cha (19) cha sheria mama, mstari wa kwanza kutoka juu neno 'kjifungu' maana yake hiyo 'k' ilikuwa haina 'i', hivyo lisomeke 'kijifungu' ndio yale maneno iliyosema mwanzo *typing error*.

Aidha, katika kifungu kipya cha pili kinachowekwa cha sheria mama, kwenye 'tohizo' katika mstari wa pili kutoka chini neno la tatu lisomeke 'msahaa' lisomeke 'msamaha'.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya marekebisho haya ya *typing error* na baadhi ya mambo madogo madogo, sasa naomba niingie moja kwa moja katika maoni kuhusu sheria ya kutozwa kodi kuhusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha kanuni za Baraza la Wawakilishi, kifungu 83(7) kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, naomba kuchukua nafasi hii kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu maoni ya kamati yetu kuhusu mswada uliouainisha hapo juu.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda uniruhusu kutoa shukurani zangu za dhati, kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwa kutuwasilisha mswada huo muhimu mbele ya Kamati yetu na Baraza lako tukufu, ili ujadiliwe kwa kina na baadae upitishwe na Baraza lako tukufu kwa maslahi ya wanannchi wetu wa Zanzibar, serikali na nchi yetu kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, napenda kuchukua fursa hii niwashukuru kwa dhati wajumbe wote wa kamati yetu, kwa michango yao ya kina waliyoitoa wakati kamati yetu ilipokuwa inaijadili, ambapo utekelezaji wake unaanzia tarehe 01/07/2012. Napenda niwataje Waheshimiwa Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Ali Abdalla Ali	-	Mjumbe
3.	Mhe. Asha Bakar Makame	-	Mjumbe
4.	Mhe. Amina Idd Mabrouk	-	Mjumbe
5.	Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	-	Mjumbe
6.	Mhe. Omar Ali Shehe	-	Mjumbe
7.	Mhe. Salmin Awadh Salmin	-	Mjumbe
8.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu
9.	Ndg. Ramadhan Khamis Masoud	-	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu katika kuupitia Mswada wa Sheria za Kutoza Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Mengine imefanya marekebisho mbali mbali kama ifuatavyo:-
Mhe. Mwenyekiti baada ya marekebisho hayo sasa naomba kidogo nitoe maoni ya kamati kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Marekebisho ya Mswada katika kifungu cha 7 na 13, yatasaidia kuongeza mapato ya Serikali kupitia Makampuni ya Simu ambayo hayakusajiliwa hapa Zanzibar, lakini yanatoa huduma zao na kutengeneza faida kubwa hapa nchini kwetu. Hata hivyo, Kampuni hizo zitapaswa kufungua ofisi zao hapa Zanzibar, ili kufanikisha suala hilo pamoja na kurahisisha kuweka mawasiliano ya karibu katika nchi.

Mhe. Mwenyekiti, taasisi inayoratibu huduma hizo na kukusanya data za matumizi yao na uniti walizotumia, ndio itakayokuwa kigezo cha tozo ya kodi hizo pamoja na huduma nyingine wanazozitoa hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inafarajika na marekebisho ya Sheria hii, kwani huko tunakotekea Serikali yetu ilikuwa haikusanyi baadhi ya makodi za Makampuni ya Simu yasiyosajiliwa hapa Zanzibar, lakini yanafanya biashara na kutumia huduma za kijamii hapa kwetu. Hivyo kurekebishwa kwa Sheria hii kutaiwezesha serikali kukusanya na kuongeza mapato yaliyokuwa hayapatikani hapo mwanzo kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 16 cha Sheria Mama, kinarekebishwa ili kutoa adhabu kwa wafanyabiashara au wawekezaji, wanaodanganya katika thamani ya bidhaa kwa kuweka bei ndogo ili watozwe kodi ya chini. Suala hili ni kubwa sana kwani hivi sasa kumejitokeza kwa baadhi ya wafanyabiashara na wawekezaji wanaoingiza bidhaa na vifaa hapa nchini, hushusha thamani ya ununuzi wa bidhaa na vifaa hivyo ili wapate kuzilipia kodi za chini.

Aidha, tunaiomba Serikali iende mbele zaidi kwani kuna baadhi ya wafanya biashara wakubwa hapa nchini, hudanganya kwa kuorodhesha bidhaa kwa kupunguza idadi kulinganisha na idadi halisi wanazoziingiza nchini na kupelekea kuikosesha Serikali yetu mapato makubwa. Kwa hiyo marekebisho haya yatasaidia sana kupambana na wafanyabiashara wadanganyifu wanaikosesha serikali mapato yake.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 10 cha mswada huu kimeweka tafsiri ya Sera ya Bima ambapo hapo kabla haikuwepo, ingawa Sheria ya Bima ilikuwa inaruhusu kutoza kodi. Kuwepo kwa tafsiri hiyo kisheria kunapelekea kuweka wazi mfumo wa utozaji wa kodi. Mbali na tafsiri ya sera ya Bima, mswada pia umetambua kuwepo kwa tafsiri ya sera ya Bima ya maisha, ili kutoa ufafanuzi wa sera hiyo na kusaidia kuweka utaratibu mzuri wa kulipwa fidia ya muajiriwa au mdau wa Bima ambae amesajiliwa na Bima.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 11 cha mswada kinaainisha kuwepo kwa mabadiliko katika kifungu cha 3 cha sheria mama, ambapo vimeongezwa vifungu vipya nambari 6 na ambacho kinampa uwezo waziri kwa kushauriana na Kamishna, kuwateua mawakala au kundi la maofisa walioidhinishwa na sheria hiyo ili waweze kusaidia kukusanya Kodi ya Bima.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu pia inafarajishwa na suala hili, kwani litasaidia kuongeza mapato ya Serikali. Hata hivyo, hapa tungependa kutoa angalizo kwa serikali kuwa makini kwani tumekwisha shuhudia kuwa kuna baadhi ya Makampuni, mfano ambayo yako Tanzania Bara ambayo yalikuwa ni Mawakala ya Kampuni za Bima, na waliweza kukusanya pesa nyingi kutoka kwa wateja na baadae kukimbia nazo, na hadi leo hazijarejeshwa.

Aidha, tunaomba kuitanabaisha serikali kuwa makini na mawakala watakaoteuliwa kufanya kazi hiyo kuhakikisha kuwa kodi wanayoikusanya inawasilishwa Serikalini bila ya kucheleweshwa, ili kuepusha upotevu au hujuma yoyote inayoweza kutokea na kupelekea kuvuruga malengo na mipango ya serikali iliyojiwekea.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu pia imefurahishwa na kuongezwa kwa kifungu kipya cha 7 katika kifungu cha 3 cha Sheria mama kuwa waziri kwa kushauriana na Kamishna, anaweza kufuta uteuzi wa wakala au kundi la watu wasiokuwa waaminifu katika kazi za ukusanyaji Kodi ya Bima. Kamati yetu inaamini kuwa uwepo wa kifungu hiki, pamoja na utekelezaji wake utasaidia kuepusha wizi na udokozi katika shughuli za ukusanyi kodi.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo, kamati yetu inataka kuelewa ikiwa wakala au kundi la watu limeshateuliwa na kufanya kazi ya ukusanyaji kodi, na baadae ikabainika kuwa wakala huyo hana huaminifu katika kazi yake, kwa maana amebainika kuwasilisha Serikalini mapato pungufu kinyume na uhalisia wa makusanyo au anashirikiana na wateja wasiokuwa waaminifu kwa kukwepa kulipa Kodi ya Bima. Mhe. Mwenyekiti, katika hatua hiyo, hatujajua ni hatua gani za kisheria zitachukuliwa. Kama hakuna sheria basi kamati inapendekeza kuwepo kwa sheria ya kuhakikisha kuwa wakala huyo anairejeshea serikali mapato aliyoyavujisha pamoja na hatua nyengine za kisheria zifuate.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 12 cha mswada huu, kinaainisha kuwa kifungu cha 12 cha sheria mama kinarekebishwa kwa kuweka kifungu kipya, kifungu cha 12(1), ambacho kinatoa mamlaka kwa waziri, kutoa aidha punguzo au msamaha wa kodi au taasisi za kiraia, kidini na hata wafanya biashara na wawekezaji. Suala hili lipo hapa Zanzibar na limetumika kwa muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, eneo hili kwa kweli tunatakiwa tuwe makini sana, kwani ni moja katika maeneo yanayolalamikiwa kwa kupoteza mapato ya serikali, na ni eneo ambalo linalolalamikiwa kuwa linatengeneza rushwa kubwa katika nchi za kiafrika, kwani kuna baadhi ya viongozi, mfano mawaziri waliopewa dhamana hizo wanashutumiwa kwa kufanya udanganyifu kwa kushirikiana na baadhi ya wafanyabishara kwa kukwepa kulipa kodi za serikali, ili sehemu ya kodi hiyo iingie mifukoni mwao.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mifano katika Bara la Afrika, kwamba kuna baadhi ya mawaziri waliotoka katika mifupa ya umaskini, ambao wamepewa dhamana ya kusimamia masuala ya kupunguza au kusamehe kodi, lakini baada ya kuwa katika nafasi hizo kwa muda fulani wamethubutu hata kumiliki miradi mikubwa. Mfano meli, viwanda au vitu vyengine ambayo hailingani na uwezo wao kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, tunaliainisha hili ili kumtanabaisha waziri, kuwa kifungu cha 12(1) asije akakitumia kwa maslahi yake binafsi na kupelekea kuikosesha serikali mapato ambayo yanahitajika kwa maendeleo ya nchi, kitu ambacho naamini kwa waziri wetu huyu mpendwa hawezi akafanya suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile Kamati yetu inakubaliana na utaratibu utakaowekwa wa Waziri, wa kutunga kanuni ili kuongoza utaratibu wa utoaji wa msamaha. Kamati inaamini kuwa kuwepo kwa kanuni hizo pia kutachangia kumdhibiti waziri husika kuitumia misamaha ya kodi kwa maslahi yake binafsi. Hata hivyo, kamati yetu inaagiza kwamba kanuni hizo ziandaliwe kwa haraka lakini pia ni vizuri zikawasilishwa Barazani au kwa kamati, ili tujiridhishe na hasa ikitiiliwa maanani kuwa hivi sasa kwa mujibu wa kanuni zetu mpya za Baraza la Wawakilishi, Baraza limepewa uwezo wa kuunda Kamati ya sheria ndogo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile si vibaya kanuni au sheria zikaelekeza ni hatua gani zichukuliwe kwa waziri au afisa yeyote aliyejitwishwa jukumu la waziri kwa kukitumia kifungu cha 12 (1) kwa maslahi yake binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla katika suala hili la misamaha au upunguzaji wa kodi, ni vyema kwa serikali kuleta taarifa ya misamaha itakayotolewa kila mwaka hapa Barazani, ili tujue ni nani amesamehewa na kwa kiwango gani cha pesa kwa mwaka, ili kuweka uwazi kwa umma, kwani suala hili la kodi ni la wananchi na huu ndio utakuwa mfumo mzuri wa utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, katika marekebisho ya kifungu cha 3, kamati yangu inaipongeza serikali, kwa kuweka utaratibu maalum kwa kutoza kodi kwa mikahawa na watembeza wageni kwani kulikuwa na baadhi ya wenye mahoteli kuamua kulipa kodi kwa kutumia kiwango cha bei ya chini ya kiwango kilichowekwa, lakini kwa marekebisho haya itaondoa ukwepaji huo wa kodi na itaongeza mapato ya serikali. Suala hili tulilizungumza kwa muda mrefu, lakini tunashukuru kwa hivi sasa waziri wetu msikivu ameamua kulitekeleza kwa vitendo kwa kuleta marekebisho haya.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 19 cha mswada kinaainisha kufutwa kwa kifungu cha 15 na kuwekwa kifungu kipya cha 15A, ambacho kwa ujumla kinadhibiti upotevu wa magendo ya mafuta na upotevu wa mapato kupitia biashara ya mafuta. Kifungu hiki kinaweka utaratibu wa uingizaji, uuzaji na usafirishaji wa mafuta kwa lengo la kuepukana na upotevu mkubwa wa mapato ya serikali, kupitia magendo ya mafuta. Hivyo, kupitia marekebisho haya ni dhahiri kuwa mapato yataongezeka na kusaidia uchumi wa nchi. Kamati imefarajishwa kwa kuwekwa adhabu kwa yeyote atakaekiuka utaratibu utakaowekwa kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 26 cha mswada kinaelekeza kufanyiwa marekebisho kifungu cha 45 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ambacho kinampa uwezo Kamishna kuweza kuomba mahkama kumlazimisha muekezaji kulipa kodi aliyokwepa moja kwamoja kwa Mamlaka ya Mapato. Kwa ujumla Kamati yetu imefurahishwa na hatua hii kwani itasaidia kuhakikisha malipo kwa wale wawekezaji sugu wanaoikosesha mapato serikali yanapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaipongeza serikali kwa kufanya marekebisho katika sheria ya mafunzo ya amali nam 8 ya 2006. Inayorekebishwa kwa kuweka mgao wa ada ya 60% elimu ya juu na 40% kwa mafunzo ya amali. Kiukweli huu ni mwanzo mzuri lakini bado kamati yangu ingelipendelea zaidi kuwa pesa zote hizi 100% ziende kwenye mafunzo ya elimu ya amali, kwani vijana wetu wengi hawana elimu ya amali na hupelekea wengi wao kutegemea kuajiriwa serikalini, kwani suala la elimu ya juu, tunaelewa ni suala la Muungano, na kuna fedha nyingi kila mwaka hutengwa kwa ajili ya elimu ya juu, lakini bado kama kawaida yetu siku zote tunasema, lakini tunashindwa kujenga hoja kwenye Bodi ya Elimu ya Juu ya Muungano ili kuzipata pesa hizo kama katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inavyosema.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kabisa, sasa naomba nije katika suala la mwisho ambalo nitaomba suala hili nitoe mchango wangu moja kwa moja binafsi, nikiwa kama Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kutokana kwamba nilisahau kifungu cha Kanuni wakati wa mchana, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na kwamba alivyosema mwanzo tayari tumeshaunga mkono Bajeti Kuu ya Serikali na tulikubali mipango yote iliyopangwa ya maendeleo ya ukusanyaji pamoja na matumizi ya fedha za umma.

Pamoja na hayo, Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa sasa tunataka kufanya marekebisho ya sheria za hizi kodi, basi naomba nimkumbushe kwamba tuliwahi kushauri katika kamati kwamba suala hili hasa Kodi ya Bandari na ukizingatia wanachi wetu wa Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba mara nyingi huwa wanasafiri katika visiwa vyetu hivi.

Kwa bahati nzuri katika Visiwa vya Unguja na Pemba si aghalabu sana kwenda kufanya biashara, lakini zaidi wanakwenda kwa ajili ya shughuli za kifamilia kama vile misiba, harusi pamoja na nyengine mbali mbali. *(Makofi)*

Kwa hivyo, bado namuomba sana Mhe. Waziri kwamba ada hii ya bandari ya kodi ya shilingi 1,000/= kwa ajili ya usafiri wa Pemba, basi namuomba sana Mhe. Waziri wetu ambaye ni msikifu, makini kabisa na mwenye huruma, hivyo kodi hii aiondoe ili kuwapunguzia mzigo wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa asubuhi nilitoa mfano hai kabisa kwamba wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura karibuni asilimia 35 ni wananchi wanaoishi katika Kisiwa cha Pemba wanaishi na familia zao na wakati mwengine huamua kwenda bandarini kwa miguu kutokana na ukosefu na nauli ya daladala. *(Makofi)*

Sasa kama nilivyosema wakati wa asubuhi au mchana suala la shilingi 1,000/= tutaliona dogo kwa sisi ambao tunaopokea mishahara. Lakini wananchi wetu wa kawaida hasa wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura naamini na majimbo mengine kutokana na kwamba uwezo wao kipato ni mdogo, yaani uhakika wa kupata ni mdogo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Waziri yeye mwenyewe shahidi alikuwa Mbunge, sisi inafika pahala asubuhi anakuja mtu anakuomba shilingi 2,000/= angalau apate mikate ya watoto.

Kwa hivyo, kutokana na suala hili ndio maana tumejaribu kushauri na Mhe. Waziri akiangalia kwenye Ripoti yangu ya Kamati ya Wenyeviti nilishauri maeneo mengi ambayo serikali mpaka hivi sasa bado hatuyakusanyi, pengine Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaelezea tukusanye fedha na sisi tunashindwa kuzikusanya kutokana na hizi kero ndogo ndogo ambazo tunazozipata.

Vile vile katika baadhi ya maeneo tunayopeleka fedha ambazo fedha zile wakati mwengine ni za miradi ya wafadhili au za ndani zinatumika vibaya. Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwamba Mhe. Waziri amewaagiza mawaziri kukaa na Makatibu wao Wakuu, ili kuangalia fedha zote zinazoainishwa kwenda katika miradi ya maendeleo kuhakikisha wanazisimamia vizuri, ili mambo haya yasitokezee. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie kwa kusema fedha ambazo Mhe. Waziri alizosikitika shilingi bilioni 18 alizozikosa kupitia katika kodi ya wale wafanyakazi wa Serikali wa Jamhuri ya Muungano ambao wapo hapa Zanzibar, kwani shilingi bilioni 18 si kidogo. Kwa mfano, ametutajia kodi ambayo ingekusanywa bandarini tulitegemea karibu shilingi bilioni mbili zingelikwenda kwenye madawati.

Sasa kama leo tungezipata zile bilioni 18 ambazo tumezikosa kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nafikiri zingelibakia shilingi bilioni 9 tu, lakini kusema kuchanga shilingi bilioni mbili kama alivyosema kwamba tunahitaji shilingi bilioni 24 kwa ajili ya madawati.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli zaidi ya miaka 7 tungeliweza kukusanya fedha hizi. Lakini bado naamini na ninawaomba wananchi wa Zanzibar kuangalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuangalia vifungu vyote ambavyo vinatukwaza Zanzibar katika ukusanyaji wa mapato, ambavyo vimo ndani ya Orodha ya Kwanza ya Nyongeza ya Kwanza katika Mambo ya Muungano, mambo ambayo yamo katika Katiba ya Muungano na tulipaswa kupata fedha zile kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar fedha hizi hatuzipati.

Sasa wakati umefika ambao ni muafaka kuangalia na tuache jazba kama walivyosema wenzangu na Mhe. Mwanasheria Mkuu amezungumza vizuri sana leo, yaani kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar hatuna uwezo hata ya kuitisha Kura ya Maoni kuhusu suala la kuulizwa wananchi kama muungano wanautaka au hawautaki, isipokuwa ni Bunge tu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kwenye Orodha ya Pili mambo manane yale ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania peke yake, ndilo linaloweza kuitisha au kupeleka hoja na kuijadili na kuweza kuamua kama muungano uwepo au usiwepo. Lakini Zanzibar bado hatuna mamlaka hayo, Rais wa Zanzibar hana mamlaka hayo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hana mamlaka hayo.

Kwa hivyo, nafasi pekee iliopo tunawaomba wananchi watulie na waangalie Katiba na wasome kifungu kwa kifungu, ili kuweza kujua marekebisho gani ambayo wanayahitaji na Zanzibar yale maslahi tunayoyahitaji kwa maslahi ya watu wa Zanzibar yapatikane.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru kunipa nafasi hii kuweza kutoa maoni ya kamati, pia nitoe maoni yangu kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura pamoja na wananchi wote wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwenyekiti wa Mwenyekiti wa Wenyeviti, kwa hotuba yako mwanana ambayo tumeisikia na tumeielewa na sasa wakati wa majadiliano umewadia na tuanze na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kuweza kunipa fursa hii jioni ya leo kwa ajili ya kuchangia Mswada wa Sheria ya Ongezeko la Kodi ya Thamani.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nisifanye dhambi ya kutokumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo hasa leo pale alipokuja kutoa hotuba yake ya aina yake. Kwa kweli tokea nikae katika Baraza hili sijapata kuona utaratibu wa hoja alizojibu Mhe. Waziri ambazo nimejaribu kwenda kwenye *dictionary* na bado sijaona namna kama ile.

Kwa kweli namshukuru sana Mhe. Waziri na mtaalamu uliyempata Mwenyezi Mungu akujaalie uende naye hivyo na sijui ndiye yule Katibu wake kipenzi au mwengine atajua mwenyewe, lakini amefanya vitu vizuri sana na hongera sana Mhe. Waziri.

Vile vile nishukuru sana katika mswada wake huu aliotuletea leo hii, ili kuweza kutoa yale ambayo tunayoyaona, kwa ajili ya kuisadia serikali na hasa katika masuala ya kodi kama tunavyojua.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Waziri ameonesha dalili ya kutaka kukusanya kodi katika serikali yake, kwanza ni msikivu pia ni mtu mwenye kukubali ushauri. Kwa mfano, unapomwambia usiku basi asubuhi ameshafika sehemu inayohusika, yaani sehemu inayovuja mapato na Mhe. Waziri anafika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni shahidi kwa sababu nimemuona kwenye vyombo vya habari na hata sehemu za bandarini nilifikiri labda anataka kupanda majahazi kumbe vile yumo katika kuangalia utaratibu wa mapato yake yasitoke.

Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti ametueleza hapa na mara nyengine wakati anaposema Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti na sisi huku wenyeviti inapaswa tuweze kumuunga mkono kwa ile hotuba yake alivyoeleza. Mhe. Mwenyekiti, mimi namuunga mkono Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti kwa hotuba yake nzuri sana aliyoitoa jioni ya leo.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti ni mtaalamu sana na mtu mwenye kuhamasisha tena anaumwa sana na uchungu na nchi yake kukosa mapato na sisi tuko pamoja na yeye. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu ni mzuri sana na unaweza kutufikisha pahala pazuri, lakini na mimi nianzie hapa kwenye kodi ya shilingi 1,000/= ya kuwatoza ndugu zetu wanaotoka Unguja kwenda Pemba kwa kweli haistahili lakini tena ndio tunaifanya tu iwe stahili.

Mhe. Mwenyekiti, tulipokuwepo sisi wenyeviti siku hiyo tulijaribu kuizungumzia sana na tuliangalia uzito wake. Lakini imefika pahala kwenye *red carpet* sasa hapa tunatakiwa tuichambue, kwa sababu mtu mwenye kutoka Unguja na kwenda Pemba sio wengi wanaokwenda kibiashara na hili tulikubali Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Kwa kweli tunakwenda kuliokoa zao la karafuu tu, hivyo ndivyo ilivyo lazima mtu uchumi wake akaulinde pamoja na kwenda kuutetea, lakini akirudi masuala yamekwisha, yaani tayari ameshaokoa na serikali imeshapata tija. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mara hii kama tulivyosema kwamba tunakwenda kifua mbele kwamba watu wamepata fedha nyingi, serikali pia imepata faida. Mhe. Mwenyekiti, suala hili namuomba Mhe. Waziri alione na kuweza kuliondosha.

Mhe. Mwenyekiti, labda kidogo nimuangalie Mhe. Mwanasheria Mkuu. Kwa kweli kwanza na yeye nimsifu sana Mhe. Mwanasheria Mkuu na leo kama atanipandisha cheo chengine au atanishusha, lakini kuna mambo inabidi lazima Mhe. Mwanasheria Mkuu akubaliane na sisi watu wa *backbenchers*. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wetu anajitahidi kuzidisha makodi kwa sababu hana kitu na huu ukweli tuuseme Mhe. Mwenyekiti. Lakini hatari yake mwisho yule ng'ombe ukimkamua kwa wingi matokeo yake utamtoa damu na hasara yake ndio kama hii. Kwa mfano, vikodi vidogo kama hivi kwenda Pemba na Unguja tunatoza, yaani hiyo ndio hatari yake Mhe. Mwenyekiti, lakini tunazo kodi nyingi tu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa tunayo mashirika humu na yanafanya biashara na wala kodi hawatoi na Mhe. Waziri ameliona hilo. Kwa mfano, *ZSSF* wanazo hoteli, Shirika la Bima Zanzibar wanavitu vyengine ambavyo tayari nao hao tuwatoze kodi.

Suala hilo ameliona Mhe. Waziri kwamba *ZSSF* na wao ni watu wa miradi, yaani hivi sasa wanazo hoteli kubwa na lile suala la Kiwanja cha Kufurahishia Watoto Kariakoo sijui limeishia vipi, lakini hayo tuyaache, kama lingefanikiwa basi na ule ungekuwa ni mradi.

Mhe. Mwenyekiti, bado uvujaji wa mapato unaendelea. Kwa kweli ukusanyaji umekuwa ni mdogo sana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti kwamba atembelea tena uwanja wa ndege na kama kawaida yangu nakwambia tembelea, kwani mapato bado yanavuja, pia arudi tena bandarini bado mapato yanavuja na kuendelea na uzi ule ule, ili tuzidi kile kiwango ambacho tulichokiweka na wananchi wawe na fedha za maendeleo na kwenda kufanyiakazi.

Mhe. Mwenyekiti, alizungumza Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti kuhusu suala la Katiba. Lakini mimi nitarudi nyuma kidogo naomba samahani kama alivyosema Mwenyekiti wangu kuwa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na alivyosema mwalimu wangu sisi hapa tunapiga ngoma tu. *(Makofi)*

Lakini mimi hushangaa humu ndani ya Baraza tunao Wabunge tumewachagua kwa kura zote na hizi kelele zetu naamini zingewafaa wakaondoka nazo na kuzipeleka kule kwa ajili ya kutusaidia, ili kuweza kupata mapato yetu. *(Makofi)*

Jambo la kusikitisha Mhe. Mwenyekiti tunao humu na wao huwa wanachangia sasa mimi je, Mhe. Mwanasheria wangu na mimi hufanya makosa kujiuliza swali hilo, kwa sababu unapomchagua Mbunge ndani ya Baraza, ili aende kule na kutusemea yale ambayo yanayotukera sisi Zanzibar kukosa mapato. Sasa kitu hicho mimi ndicho kinachoniuma Mhe. Mwenyekiti naomba nikwambie. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, siwageukii pengine wengine ni wanachama wangu wa *backbenchers*, lakini ukweli ndio huo na ikifika pahala tuseme basi tutasema, kwa sababu lazima tuseme tuwaambie wenzetu. Kwa kweli tumewachagua kwa kura zote waende kule Bungeni wakatusemee pamoja na kututetea haki zetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, siku zote husema kuna baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri huwasifu sana na kuwaunga mkono kwenye hotuba zao. kwa mfano, leo amezungumza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na alieleza vizuri sana kwamba tatizo lipo la kukosa haki zetu katika muungano, pia Mhe. Waziri wa Fedha ambaye ni kipenzi changu ameeleza na kusema kwamba hakubaliani nalo, kwa maana hiyo ataendelea kuzidai. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi namwambia Mhe. Waziri kwamba aliomba nafasi leo kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kupitia Mhe. Spika, mimi wakati ule nilikuwa nikisema chini chini kwamba mwambie Mhe. Spika aondoe Kanuni na achague hao watu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nawambia kwamba wanapokuwa tayari kwenda kule kwenye Kamati yao ya Muungano kwenda kudai maslahi yao, basi ondoa Kanuni na Katiba na tupeleke sisi na tutarudi na mafao Mhe. Mwenyekiti na wala kodi za thamani zisingepanda hapa. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Mhe. Mwanasheria Mkuu tutafutieni sheria, kwani na mimi si kiongozi, kwa sababu mimi ni Waziri Nisiyekuwa na Ofisi Maalum, tayari hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tuseme ukweli ni sheria, kwani mimi ni Waziri Nisiyekuwa na Wizara Maalum, kwa sababu wakati wowote Mhe. Rais atanichagua niwe waziri na hiyo nasema tu na wala sitaki uwaziri au sina mantiki kama ninautaka uwaziri, lakini nasema kutokana na kile cheo changu. *(Kicheko/Makofi)*

Hivi mimi sina haki ya kwenda kule kwenye tume kwa ajili ya kudai haki ya Wazanzibari, lakini leo kila siku tutaleta makodi tu haya, basi hata hiyo kwenda Pemba ni shilingi 1,000/= na fedha zote za nini hizo wakati fedha zetu nyingi zipo kule.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri ambaye ni hodari sana, basi Mhe. Waziri nipeleke sasa tukadai fedha zetu Wazanzibari. Kwa kweli tumechoka na ukweli tuuseme jamani uko wazi, kwa sababu ninachozungumzia ndani ya Katiba na Mwanasheria Mkuu ambaye ni mwalimu wangu yumo, yaani kitu kimo ndani ya Katiba kwamba Wazanzibari mtakuwa na fungu lenu mpaka leo hatulioni.

Vile vile kuna suala la gesi asilimia mpaka leo fedha hatuzioni, kwa sababu tungezipata fedha hizo Mhe. Mwenyekiti, *Wallahi* Mhe. Waziri asingetia hivi vikodi vidogo vidogo naamini hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwa uchungu tumechoka na tulipokosea sasa turekebishe tuunde timu na tukesha kuunda timu basi tupelekeni na tuone na *Wallahi* nakwambia Mhe. Mwenyekiti na wala sio utani. Mimi kwanza kule sitoingia na *briefcase* hata siku moja, isipokuwa naingia na Katiba yangu tu na nitaeleza kifungu hadi kifungu na kusema nipeni haki yangu ya Wazanzibari nirudi nyumbani na kazi imekwisha. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna gazeti hili hapa linatembeza Mtandao wa Gesi Asilia na hili ni suala la muungano, mbona mpaka leo hatujapewa haki yetu. Mhe. Mwenyekiti, mambo haya tufike pahala tumsadie Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Nakumbuka Mhe. Waziri alisema peke yake hatoshi, kwa sababu kijana mdogo na wala simkubwa bado hajazeeka, yaani anazo nguvu lakini haziendi nguvu zile kama hakupata watu kama sisi na fedha hazipati tutakwenda na kurudi hivyo kila siku na wala hamzipati.

Mhe. Mwenyekiti, tukikaa na kusema jamani tuweke Kanuni zetu kando kumbe Waheshimiwa Wajumbe wetu wanao uwezo wa kuingia kwenye Kamati za Kero za Muungano, basi tupelekeni kwa ajili ya kumaliza kwani Wazanzibari wanaumia na njaa. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Waziri alisema kwamba leo anataka kuwabana wawekezaji. Lakini wanasahau wakati wanapokwenda nje tunapomu-*organize* yule *investor* kwamba njoo Zanzibar tutakuwa *freemen* katika masuala moja, mbili, tatu.

Sasa wakati tunapoingia hapa tunamgeuka na kuja kupoteza *billion* za fedha kwa kununua ardhi kwa wananchi, mwananchi pale tayari ameshapata tija na kwanza tukubaliane hilo na baadaye anaanza yeye kufanya maandalizi ya kuweza kutaka kuleta kitu ambacho cha msingi. Mhe. Mwenyekiti, tunarudi tena kwa yule na kumnyang'anya *land lease* ile wakati tayari amepoteza fedha zake nyingi, hivi tunakwenda wapi? *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hizi kodi kwa wawekezaji tuziangalie vizuri na leo Mhe. Waziri amesema masuala ya vikombe na wala haina tatizo. Lakini mambo mengine lazima wapewe kodi yao na wala wasiachiwe na hivyo ndivyo wanavyokwenda wenzetu nchi za nje.

Mhe. Mwenyekiti, aliniambia Mhe. Waziri kwamba mimi nilikwenda *Barcelona*, kweli wala si uongo. Kwa kweli mechi ile ya Chelsea na *Barcelona* mimi ndani ya uwanja nimo, yaani *live* kabisa na wala si utani, wanacheza na mimi nauona namuona Mesi hivi hapa na hapa. *(Makofi)*

Lakini tuangalie wenzetu uchumi wao kupitia utalii, hebu tuangalie wenzetu wanavyowakumbatia *investors* au watu wa *Tourism* wanaokwenda kutembea kule. Kwa mfano, lile *Open Bus* la kupanda *Tourists* kodi yake ni rahisi sana, kwa sababu wanakushawishi kwamba uingie kwenye basi lao na utembee kwenye sehemu zao zinazohusika, ili uvutiwe na mwengine aletwe.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri asimshawishi mtu kwa sababu kodi hizi kwa hawa *investors* lazima uwasaidie na hilo tuseme ukweli. Kwa kweli hatupotezi mapato kwani tunazo fedha zetu kule. Mhe. Mwenyekiti, wakati umefika na hili lazima tuseme, Mhe. Waziri alisema hapa kwamba mawaziri wetu wasimamie fedha za maendeleo.

Kwa mfano, juzi nilimuuliza swali Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nilimuuliza swali kwa kumwambia jamani ee hili Bango Kitita tunalompelekea Mhe. Rais lina ukweli ripoti zake za maendeleo na ikiwa ni hivyo je tukimgundua Mhe. Waziri amefanya suala kama lile yuko tayari kujiuzulu, yaani kabla Rais kumtangazia na tuliambiwa kwamba atajiuzulu mtu.

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba wakae tayari kuna watu wataweza kujiuzulu wenyewe kabla kuambiwa wajiuzulu. Sababu moja kuu ambayo, Mhe. Mwenyekiti mimi nitakuwa nikichangia jumla jumla ndio kodi yenyewe inavyotakiwa hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, umebakiwa na dakika tano.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, bado dakika tano na hilo si tatizo.

Kwa hivyo, ninachomalizia Mhe. Mwenyekiti hivi sasa wakati umefika kama alivyosema Mhe. Mwenyekiti wangu kwamba tusiwe na fujo, tuwe na utulivu, ili tuweze kudai haki yetu, kwa sababu kule kuna fedha nyingi tunadai na mtu anayemdai usimnunie na wala usimfanyie fujo, kwanza ikamate fedha na baadaye ndipo mtakapojua tena kama mtanuniana au utapumua ama vyenginevyo utajua mwenyewe, lakini itakuwa ile haki yako tayari umeshaipata.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilisikia kwenye matangazo kwamba deni letu limefutwa na *TANESCO* na wala tusidanganyane, deni bado lipo pale pale. Kwa kweli kila siku tunaletewa risiti na kuambiwa deni letu bado lipo. Sasa mambo mengine Mhe. Mwenyekiti, na juzi nilisema tulete umeme mbadala kwa ajili ya kutusadia na kuwaokoa wananchi wetu kutoka kwenye umasikini. Mhe. Mwenyekiti, kodi zote zile wakija *investors* kama wale wa masuala ya viwanda, basi kodi ndio wanazibeba wale na wala Mhe. Waziri wangu hapati tena kutoza kodi kwa wananchi wanyonge.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kwamba sasa tuingie katika masuala ya kutafuta *investors* wakubwa kwa lengo la kupunguza kodi kwa walalahoi. Kwa mfano, mshahara angalau uweze kupanda pamoja na mambo mengine yote na hii kodi ya thamani angalau lugha baadaye ije kubadilika badala ya kuwa kodi ya thamani iwe kodi ya tija. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia dakika zangu napenda kusema kwamba wananchi wangu wa Jimbo la Kitope wananiambia hivyo kwamba niwatetee kwenye haki zao. Kwa kweli kodi hizi ndogo tuwape msahama na badala yake tulete *investors* na watu watauza taka na kuweza kupata kazi mbali mbali, kwa upande wa serikali nao watapata fedha zao na itapumua na kuweza kufanya shughuli zao za kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache naunga mkono mswada huu wa Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja. Lakini ahahikishe wazi kwamba katika Tume ya kwenda kudai fedha zetu mwaka huu, basi atualike sisi watu wa *backbenchers* kwa lengo la kuleta fedha zetu za muungano. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe ahsante. Waheshimiwa Wajumbe, ningependekeza kwamba tuchangie zaidi katika mswada na sasa tunampa nafasi Mhe. Asha Bakari Makame. *(Makofi)*

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii adhimu na mimi niweze kugusia hapa na pale.

Kwanza nichukue nafasi hii Mhe. Mwenyekiti nimpongeze sana Mhe. Waziri, yaani nimpongeze kwa makusudi kwanza jinsi alivyotupa mambo katika kufanya majumuisho kwake, kwa kweli ametusaidia sana na ametufafanulia mambo mengi. *(Makofi)*

Vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti nampongeza sana jinsi anavyothamini maamuzi katika mikutano yetu. Kwa hivyo, na mimi niungane mkono kuhusu suala la kodi ya jamaa zangu ile shilingi 1,000/=. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna siku nilizungumza hapa kwamba sisi asili ya kisiwa cha pili kule Pemba tukenda twike na tukirudi twike na watu wakaniuliza twike ni kitu gani? Twike ni kukokota mpaka kijukuu hutaki ukikose, yaani ukitoka Pemba kuja Unguja na ukitoka Unguja kwenda Pemba mpaka kile kijukuu hutaki ukikose na hiyo ndio twike na mbali twike ya zawadi, mizigo pamoja na mambo mengine.

Kwa hivyo, na mimi nikaona kuna haja Mhe. Mwenyekiti kwa heshima na taadhima tukubalie suala hili, ili na sisi tupungukane na mzigo mkubwa kama alivyosema Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti, yaani ni mzigo kwetu. Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti kwamba suala hili alifikirie na ninamuomba sana atukubalie yale maamuzi ya wenyeviti ambapo tulikaa pamoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe tena Mhe. Waziri kwamba tulizungumza hapa kuhusu masuala ya kodi mbali mbali. Lakini mimi nasema bado fedha zipo na tunaweza kuisaidia serikali kama alivyosema wenyewe Mhe. Waziri wa Fedha kwamba wengine tunaweza kuisaidia na kufichua baadhi ya mambo ambayo yanaweza kuisaidia serikali yetu. Lakini jambo kubwa niseme pombe na sigireti kodi yake inaridhisha. Wewe sigireti ipandishwe hata kiasi gani siye wavutaji tutakuwa tutahemea kifuani. Pombe ni hali kadhalika kwa sababu tunapiga nini vita, mvinyo. Hili naomba uliangalie tena upya wale wenye kustarehe kwa mambo haya wajijue.

Mhe. Waziri niiunge mkono wale wanzetu waliosema kuhusu habari ya bilioni 18. Hii ni haki yetu wala haitaki ndondondo. Naomba sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kama ulivyozungumza wewe Mhe. Waziri, jukumu lote unalo wewe Mhe. Waziri. Kwa sababu wewe ndio tuliekukabidhi ufunguo. Kwa imani yangu na tunavyokujua Mhe. Waziri wa Fedha suala hili utalipigia mbio, utalivalia njuga ili kuhakikisha kwamba fedha hizi tunazipata. Mengine lazima tuyadai yale waliyokuwepo kwenye mstari. Kwa hivyo hili nakuachia wewe mwenyewe kwa dhamana tuliyokupa.

Mhe. Spika, si vibaya nikagusia, japo tugusie mambo ya kodi na nini lakini haya nayo pia yanaingia. Nasema naunga mkono kwa Profesa Mshimba alivyosema kwamba tumechagua Wabunge wetu kutoka Baraza la Wawakilishi kwenda kutusemea Bungeni. Mimi nadhani iko haja, natia ushawishi tutakapobadilisha katiba hizi nafasi tuzifute. Hazina maana kwanza zinatuletea ugomvi simtofahamu, huyu kapata, huyu hakupata, inakuwa tena hatuelewani. Kwa sababu nafasi hizi tumeziweka kwa mujibu wa taratibu ya kwenda wenzatu kule wakaseme. Kwa sababu sisi kuna shughuli nyengine ni za Muungano.

Nyiye wenzangu nakuulizeni nyie Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mlimsikia nani kusema chochote kuhusu habari ya mambo ya Muungano tu, labda enzi ya Mhe. Ismail Jussa. Ndiye mtu ambaye alikuwa kwa kweli hataki mchezo, alipoteuliwa tu. Sasa mimi nasema msifikirie kwamba tunayazungumza haya kwa sababu ya choyo au chuki au nini. Tumeteuwa wenzetu wa kwenda kusaidia, hivyo mazungumzo yote haya tunayozungumza, hawajui wao kama tunadai bilioni 18. Nani kati yao aliyesimama akazungumza. Mimi nasema sisi wenyewe tunajikosesha haki zetu za Muungano. Kwa sababu hatwendi tukatetea mambo ambayo yanahusu Muungano.

Nawaomba sana hawa watakaomalizia, maana keshokutwa tukimaliza katiba nashawishi zifutwe hazina maana. Kuanzia sasa zile Wizara za Muungano wazisemee maana huwa humu hatuwezi tukasema. Hata tukisema sisi kule hatupigi kura wala hatufanywi chochote. Nawaomba Wabunge wanaotoka katika Baraza la Wawakilishi kuwakilisha watusaidie kwa hilo Mhe. Mwenyekiti. Watanisamehe sana kuwazungumza kwa sababu imefika wakati sasa sisi wenyewe kudai haki zetu kwa mujibu wa taratibu na sheria tulizoziweka. Tumo kwenye Katiba, miye nakuombeni sana Waheshimiwa Wabunge ambao mnatuwakilisha Baraza la Wawakilishi, mseme mzungumze, madai haki zetu, tusigombane na wenzetu wakati nyinyi mnao uwezo wa kuzungumza kule.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, maana lilikuwa linanikereketa hili. Mimi Wallahi nasema tungempa Mhe. Hamza angezungumza kule. Samahani kusema hivyo, kati ya hawa watano (5) Mhe. Hamza angepata basi angezungumza, mawili yangetokea, angetia moto au pangekuwa hapakaliki. Lakini ndio rizki ikishakuandikwa kwa mtu haiwezi ikafutika.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, nilisema na mimi nitoe dukuduku langu kidogo kama kawaida yangu mimi huwa siwezi kuficha kitu. Nitamtakia kila la Kheria na namuhakikishia Mhe. Waziri katika mambo haya tutamsaidia na tuko pamoja. Ahsante sana naunga mkono.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mhe. Mwenyekiti, mimi nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naomba nitoe mchango wangu mfupi sana kwenye hoja hii ya kaka angu mpenzi Mhe. Omar Yussuf Mzee, hoja ambayo ni hoja ya kuongeza na kuzidisha sheria ya kodi.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani kwanza tungejiuliza kwani Zanzibar tuna tatizo la pesa. Mtu mwenye akili timamu ajiulize tatizo ni nini? Tatizo fedha au usimamizi wa fedha. Mimi watu wa Kiwani wamenambia tatizo ni usimamizi wa fedha. Sisi ambao tumejenga hoja kwamba hakuna haja ya kupandisha ada ya usafiri, pamoja na kwamba hatukusoma uchumi kama Mhe. Haji Faki Shaali. Tumejenga hoja kwa kuangalia mazingira ya hali halisi ya Wanzibari wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naendelea kusema kwamba pamoja na marekebisho haya ya kodi Mhe. Waziri wa Fedha ameyarudisha kwa nia safi, lakini wenzake wamsaidie. Wamsaidie kuibua na kusimamia kodi badala ya kusubiri Hija na Hamza waseme wawakosoe.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilisema hapa kwamba msamaha tu wa fedha ambazo zinapatikana kwa manunuzi ya rada ni Pound milioni 29.5 ni sawa sawa na bilioni 72 ni sawa sawa na 3.3 bilion kwa 4.5 kwa asilimia tuliyopewa. Sasa badala ya kusubiri mtu azungumze humu akosolewe, nadhani hiyo ndiyo kazi ya serikali kusimamia. Mimi ningemshauri Mhe. Rais kwa nia safi kabisa hawa Mawaziri ambao hawana ofisi maalum basi awatumie huko wakatetee fedha yetu badala ya kutafuta Wawakilishi wamsaidie Mhe. Waziri.

Maana mimi Mhe. Waziri sijui kazi ya Mhe. Haji Faki Shaali mpaka hii leo, nasema kweli yangu, siijui. Nadhani badala Mhe. Waziri kutaka msaada wa Wawakilishi ambao kwa kweli hatujui hatuna mfano wa uchumi nadhani angetafuta ushauri wa Mhe. Haji Faki Shaali. Wakaenda kudai kodi zetu ambazo Wazanzibar wananyang'anywa.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo Mzanzibari gani hata yule anayekaa kule Muwambe ndiyo mtu wa mwisho kule Shamba, utakae mwambia kwamba serikali imeshindwa na kutetea kodi ya bilioni 18, ambao Mhe. Waziri anakiri zipo, lakini ziachwe tutafute kodi mpya ya usafiri wa baharini ya wanyonge. Si haki wala si utawala bora. Nadhani Mhe. Kwanza angesimamia kodi hii ambayo ni halali yetu kwa mujibu wa katiba. Bilioni 18 maana yake ni miaka tisa (9) ya hii bilioni mbili 2 ya kodi ya usafiri wa bahari. Wazanzibar wangepumua miaka tisa hawakatishwi kodi hii. Leo wanatwambia kwamba tusimamie kodi. Wala sio sahihi kwamba Wawakilishi hawataki kutoa kodi kwa kuwaumizi watoto wetu migongo. Kila mtu anataka mtoto wake asome vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, tumejenga hoja hii kwa sababu fedha zipo, tatizo usimamizi. Ndio maana Mwanasheria mdogo akasema tutumeni basi. Hili tumesema zamani kama kwamba tumeshindwa basi tutumeni. Lakini maskini Mhe. Hamza hata aseme Mungu Mmoja atakuwa ni mkorofi tu, tatizo kubwa.
Tunajenga hoja kuangalia kwamba wananchi wetu wanaumia vipi. Mimi nashangaa kweli unafikiria kuzalisha kodi mpya wakati mna fedha zimakaa, tena haki yetu. Kwa kweli inanisikitisha. Mimi Mhe. Waziri namuamini sana na ana nia safi lakini peke yake afanye nini? Mhe. Waziri mimi nakushauri watafute wenzako wakusaidie. Hawa Wizara wao wache wapumzike wafanye kazi hili sio la wizara, wao waende kule wakadai haki yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema hayo kwa uchungu sana, sioni mantiki yake, kwamba tumekaa na kutafuta kodi hizi mbadala. Unapopandisha kodi ya gari maana yake unawaambia wanafunzi waongezewe nauli, ndio maana yake. Hata ukizungumza lugha yako unayoitaka lakini ukipandishwa kodi ya gari maana yake madereva wanaongeza nauli na nauli hiyo kwa wanafunzi wetu wanyonge. Kama fedha zipo lakini mmeridhika kusubiri muembe uzae ili msubiri mauwa mkodishe mauwa, mimi nashangaa sana. Kama kweli nia ni kodi basi bilioni 18 zitafutwe haraka iwezekanavyo. Hili sio ombi bali hii ni haki yetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ninachotaka niseme ni kwamba sio hoja kutafuta vyanzo vya kodi. Tatizo ni usimamizi wa kodi yenyewe. Mhe. Mwenyekiti, kamati zako zinapokwenda huku chini wanegundua kwamba watu wanapewa misamaha ya kodi kiholela. Watu wanapewa misamaha ya kodi kwa kujuana. Watu wanapewa misamaha ya kodi kwa malengo binafsi. Sasa hata hii kodi ya meli ya Sh. 1000/- ambayo Mhe. Haji Faki Shaali amesema yeye si tatizo. Inawezekana kwa watu wa Mkanyageni lakini kwa watu wa Muwambe tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakiri kwamba kwa jimbo la Kiwani Sh. 1000/ ni tatizo. Mtu ambaye anatoka Mtangani mpaka Ukutini kwa mguu maana hakuna gari, hakuna barabara. Bahati mbaya Mhe. Waziri juzi alisema nitoe milioni 10 ijengwe barabara, nimeshindwa sikuweza. Lakini mtu ambaye anatoka Mtangani kwa miguu mpaka Kenya anaitafuta Mkoani na watoto wanne watano na kila mtoto ana tiketi. Maana yake atoe fedha kila tiketi moja, kwa wengine si tatizo mimi nakiri ni tatizo kwa Kiwani. Mtu huyu huyu atoe kodi ya mafuta iliyopanda. Msifikirie kwamba kodi ile kapandishiwa tajiri. Kodi ya Sh. 50 kwa kila lita ni kodi ya mnyonge. Mtu huyo huyo atoe kodi kwa magari yaliyopanda bei wakati fedha ipo.

Mimi nadhani Mhe. Waziri mimi nikuombe sana kwa nia safi kabisa japo kidogo wambie wenzako wakusaidie. Mimi sina wasi wasi na wewe najua unafanya kazi, lakini wambie wenzako wakusaidie wasisubiri, maboshelea watafute *point* wawabomoe tu. Wafanye kazi, wakusaidie, lakini watu wamekaa wanasubiri Hamza aseme, aaaah Hamza, Hamza, tatizo. Tatizo wewe usiosema.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana, baada ya hayo nasema kwamba kodi hii mimi siungi mkono ni lazima irekebishwe, kwa sababu fedha zipo, tatizo usimamizi mbovu.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi hii kuweza kusema mawili, matatu juu ya Mswada huu wa Sheria ya Kutozwa kodi na kubadilisha baadhi ya sheria za fedha na mambo mengine yanayohusiana na ukusanyaji wa kodi.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaanza kusema chochote, nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Anayeshughulikia Masuala ya Fedha kwa majumuisho ambayo ameyafanya kwa staili nzuri, takriban sote tumefarijika. Isipokuwa kuna moja tu hilo nitakuja kumwambia pembeni silisemi hapa. Hilo hakwenda vizuri, moja tu, lakini tabaan masuala yote ni mazuri, yamekwenda vizuri tunashukuru, yamejibika vizuri na bajeti yetu imepita.

Mhe. Mwenyekiti, madhumuni ya Mswada huu ametueleza Mhe. Waziri kwamba anakusudia kufanya marekebisho katika sheria ya kutoza kodi na kurekebisha baadhi ya sheria za fedha. Haya ndiyo madhumuni makubwa ambapo kuna sheria kadhaa humu sheria kama 10 mpaka 11 zimejaribu kufanyiwa marekebisho ili ziendane na azma hiyo ya kukusanya kodi. Mimi Mhe. Mwenyekiti, sina tatizo na marekebisho haya.

Mhe. Mwenyekiti, zaidi ukizingatia tumeanza kujaribu kuupitia wakati wa Kikao cha Wenyeviti. Moja ambalo nadhani Mhe. Waziri angetukubalia hili pendekezo linalozungumzwa na wengi. Waswahili wanasema wengi wape, kama hujawapa watachukua kwa mikono yao. Ukiona kila mmoja analielekeza jambo hilo basi ujue lina mantiki. Kila mmoja analisema hilo basi ujue lina misingi. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri alitizame hili ama kwa kuliondosha kabisa au kwa kulipunguza makali. Kwa vyovyote vile vitakavyokuwa lakini ni lazima jambo hili liangaliwe kwa makini.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema hivyo kwa sababu hapa kuna kodi zilizoongezwa za aina mbili, kuna Kodi ya Ada ya Bandari ya kwenda Pemba lakini kuna kodi ya Bandari ya kwenda Dar-es-Salaam. Lakini watu wamekuwa wakizungumza kwa upande wa Pemba zaidi kuliko hata Dar-es-Salaam. Kwa hivyo inaonekana lina mantiki. Kwa sababu Visiwa vya Pemba na Zanzibar bado tupo ndani ya nchi yetu ya Zanzibar si vyema kukawa na kodi za aina hii. Hili namuomba Mheshimiwa kwa kweli aliangalie kwa umakini. Mhe. Mwenyekiti tunakusudia au tumefanya marekebisho kwa ajili ya kupata fedha za kuendesha nchi.

Mhe. Waziri kwenye bajeti yake alitueleza kwamba marekebisho haya tukiyakubali basi katika kipindi hichi cha mwaka mmoja tunaweza kukusanya zaidi ya bilioni 13.2 pesa hizi sio nyingi, lakini ni nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri lazima ajipange katika kutafuta fedha. Kwa sababu hatuwezi kuendelea kukusanya kodi kwa kuwakamua wananchi wetu, hiyo haiwezekani. Ni lazima tutafute taratibu nyengine ambazo zitatuwezesha kupata fedha. Ni kweli huwezi kuendesha nchi bila ya kodi, lazima wananchi walipe kodi. Wasimamizi wa kodi wasimamie kiipasavyo kodi ili ziweze kupatikana kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu, bila ya kodi maana yake hakuna maendeleo, hilo tunakubaliana nalo. Lakini kila wakati serikali itafute njia ya kuzitafuta fedha zetu zilipo kwa ajili ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu unaotumika sasa hivi wa kukusanya kodi ya mapato yanayotokana na viza ya Uwanja wa Ndege haufai. Hili tumekuwa tukilisema kila wakati, huwezi ukategemea kukusanya kodi ya Uwanja wa Ndege kodi ya Viza kwa kugonga muhuri wa viza. Hili tumekuwa tukilisema kila wakati kwamba pale kuna mapato mengi sana ya fedha za serikali yanavuja. Hivi fedha tunazowakamua wananchi pale zipo zaidi ya zile tunazowakamua watu. Lakini serikali haitaki kuchukua *action* yoyote.

Tuambie Mhe. Waziri pale pana fedha za kutosha katika Viwanja vya Ndege. Wakati wa msimu kama huu wa utalii pale panamiminika ndege pale utashangaa. Ndege zinapishana, ndege kubwa, ma – *air bus* yanateremka pale, pote pale panajaa, wote wale wanalipa viza, lakini utaratibu wa kukusanya pesa pale kwa kweli utaratibu tunaotumia umepitwa na wakati. Wenzetu Tanzania Bara wameshaachana nao sasa sisi tunasubiri nini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli taratibu za utafutaji wa fedha ni lazima tuurekebishe ili tuone kwamba tunazikusanya kodi ipasavyo na tuachane na hizi tabia za kuachia watu kuingiza fedha mifukoni mwao. Jengine ni kwamba juzi nilimuuliza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuhusu fedha zinazotokana na gesi hizi ni lazima tuzipate ni haki yetu. Kwa sababu vitu vile bado ni vitu vya muungano na wenzetu mabilioni kwa mabilioni ya fedha wanakusanya kwa nini haki yetu tusiipate kutokana na gesi. Hizi ni pesa nyingi sana, ambazo tukizipata zitatusaidia kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti mimi sina maelezo mengi lakini nimsisitize Mhe. Waziri kwamba kila pahala penye haki yetu basi tuidai. Bilioni 18 ambazo ni haki yetu na tulikuwa tumekubaliana zipatikane kwa ajili ya maendeleo ya watu wetu. Hizi bilioni 21 ambazo safari hii wametwambia wenzetu watapitisha Mswaada zipatikane. Hivi kama hazikupatikana safari hii hapa patakuwa hapatoshi Mhe. Mwenyekiti. kwa sababu wenzetu wameshatugeuka kama watoto wa kuku. Taarifa tulizokuwa tunazo kwenye kikao kile kilichokaa kwa ajili ya kudai hizi pesa, zilipokumbushwa habari ya hizi pesa na wale wenzetu wakaambiwa jamani lakini hizi pesa mnakumbuka kwamba tulikubaliana kwamba mtatupa. Basi kuna mjumbe mmoja akasema nadhani tulikosea

tulivyosema hivyo. Eti anadhani walikosea. Hivi katika maamuzi kama hayo makubwa kati ya nchi na nchi unasema unadhani ulikosea. Hilo ni jambo la utani kweli kweli Mhe. Mwenyekiti. Cha kusikitisha Waziri Mkuu anatoa amri kwamba fedha hizi basi zilizobakia bilioni 9 zipatikane, hadi hii leo hazijapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo Wabunge wetu hawaelewi kwamba sisi tunadai, mbali ya wabunge wetu wanaotoka katika Baraza la Wawakilishi hata wale wabunge wetu wa katika majimbo pia hawaelewi kama tunadai pesa hizo kwa maendeleo ya nchi yetu. Wanataka tutoke sisi twende tukadai katika majengo ya Bunge. Wao wamepelekwa na wananchi kwa ajili ya maslahi ya nchi hii. Tuwasihi sana wenzetu Waheshimiwa Wabunge lazima watimize wajibu wao kwa nchi hii. Ni lazima wasimamie maslahi ya nchi hii ndani ya Jamuhuri ya Muungano, vyenginevyo itakuwa hawatusaidii.

Mhe. Mwenyekiti, fedha hizi tunazozikosa zingeweza kusaidia mambo chungumzima ya maendeleo katika nchi hii. Lakini leo katika hali ya utani utani tu inaonekana kama kitu cha maskhara. Mimi nikubaliane na Mswada huu isipokuwa kama nilivyotangulia kusema kwamba haya mapendekezo ya Mhe. Waziri ayaangalie sana, ayasikilize ili kifungu hichi kiweze kufanyiwa marekebisho kwa manufaa ya watu wetu, watu wetu ni wanyonge. Kwa hivyo ni lazima tutizame au tupandishe kodi kulingana na hali za watu wetu pamoja na kwamba tunazitaka, kweli watoto wetu wanakaa chini kwenye sakafu na fedha kweli zingeelekezwa kwenye vikalio, lakini lazima tuangalie na hali halisi ya watu wetu. Tutafute njia mbadala ya kuhakikisha haya madeski tunayapata na mambo mengine na uwezekano wa kufanya hivyo za kuzipata hizo fedha upo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa upande wangu ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika suala zima ambalo tunalizungumza hivi sasa la sheria ya kodi mbali mbali ambayo imefanyiwa maekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, mimi au sisi tuliopo katika Baraza hili hatutaki kumuona Waziri kwamba ameleta kitu hiki hakukifanya kwa sababu maalum. Lakini bila shaka zipo sababu kwa nini akaleta marekebisho haya. Kwa sababu yeye ni Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo basi ni wajibu wake yeye kama alivyochaguliwa na Rais, kuweza kuipatia nchi hii fedha za kuendesha nchi kwa ajili ya kupatikana mishahara, posho pamoja na maendeleo ya nchi hii.

Ni lazima hana namna akitaka asitake ni lazima atuletee hapa, ili tuhalalishe shughuli yake nzima ya kuweza kupata kodi hizi ili nchi iweze kuendelea. Hatuoni taabu kwa baadhi ya mambo, lakini tunaweza tukamuomba Mhe. Waziri na tukatoa vigezo kwa nini hili liendelee na libakie lisitolewe.

Kwa mfano tukianza kuzungumza ya ada ya bandari. Kwa kweli suala hili kwa wasafiri wa Unguja na Pemba na wanaokwenda Dar es Salaam, mantiki yangu ya kuzungumza hivi ningemuomba Mhe. Waziri hili akaiachilia kodi hii ikaondolewa, ninazo sababu zangu za msingi.

Watu wa Zanzibar na Tanzania Bara hawana nia nyengine yyoote isipokuwa safari zao ni za kawaida ni za kizamani, watu baina ya nchi na nchi au kisiwa na kisiwa kwenda kuonana na kusabahiyana. Watu wamezaana upande huu na huu wanakwenda asubuhi, mchana na jioni.

Kwa hivyo kwa Wazanzibari ambao waliomo ndani, na wengi hali zao za kiuchumi zipo chini au tuseme mapato yao ni madogo, na wana shughuli nyingi ambazo zinawakabili siku hadi siku zinawaandama kwa kodi mbali mbali.

Kwa suala hili kwa kodi za bandari ambapo kwa Pemba ni shilingi elfu moja na Dar es Salaam ni elfu mbili, hili tungelimuomba Mhe. Waziri akaliangalia tena. Mimi mantiki yangu ya kusema hivi ni kwa sababu katika safari zao za Unguja, Pemba na Dar es Salaam hakuna kigezo cha mapato. Ingelikuwa kuwa kuna kigezo cha mapato ndani yake tungefanya ukapatikana huu ushuru, lakini hawa ni watu wanaokwenda kutembea na kurudi tu, na wanajuliana na familia zao. Kwa hivyo hapa hapana mantiki ya kutoza kodi kwa watu hawa ambao wanatembeleana. Ni watu wa kawaida wa visiwa hivi tangu asili watu kutembeleana. Kwa hivyo hili suala hili ninaona tungeliweka upande.

Kwa upande mwengine mimi ningeweza kuunga mkono kwa sehemu nyengine ambazo mimi nitazizungumzia hapa. Watu ambao wanavuna kipato hapa tungeweza kuweka kodi, lakini kwa safari za Unguja na Dar es Salaam na Pemba, hizi hazina kipato. Kwa hivyo tunamtoza mtu ambaye hana kipato.

Hii itakuwa si haki. Kwa hivyo ninafikiri haki itakwenda kwa wale ambao ndani yake wanazalisha, hivyo tunaweza tukawawekea kodi. Kwa mfano ni jambo zuri ni ule ushuru wa stempu. Ushuru wa stempu ni ushuru ambao ndani yake mtu ana kazi maalum anaifanya. Kwa mfano ushuru ule wanaokwenda kwenye hoteli, ushuru ule unakwenda kwa wawekezaji, kwa wenye mikopo.

Hapa pana mantiki ya kusema kwamba hapa tuweke kodi kwa sababu ndani yake hawa wanapata madukhuli ndani yake, wanapata chochote. Kwa hivyo ukipata madukhuli ukatozwa kidogo na wewe hakuna ubaya. Lakini wananchi wa Unguja na Pemba wanakwenda kwa madukhuli gani? Hakuna madukhuli yoyote ni kuwaonea tu, hawa ni watu wanaokwenda kutembelea familia zao.

Kwa hivyo hapa mimi ninaweka hoja ya kwamba hapa kwa wawekezaji, watu wa biashara, hoteli, mikopo, hapa ni haki yao kuweka ile kwa sababu ndani yake muna kitu maalum. Kwa hivyo hapa ushuru unaotoka au ada inayotoka hapa ni kuanzia ni *one half percentage*, moja na nusu mpaka kuendelea asilimia tatu.

Kwa hivyo hapa Mhe. Mwenyekiti, hapa naunga mkono kwa hii ya pili lakini kwa hii ya kwanza ningelimuomba Mhe. Waziri kidogo akaifinyia tahafifu. Halafu inaonesha hapo zamani si kwamba watu walikuwa hawatoi kodi kwenye usafiri, wanatoa kodi lakini ilikuwa ndogo kodi yenyewe sio kubwa sana.

Tunaweza tukafanya njia nyengine ijapokuwa ni ndogo ya kupunguza kama inalazimisha ni lazima watu wa Unguja na Pemba watozwe hii ada basi ingefanywa ni ndogo si shilingi elfu moja. Mimi nikiifanyia tathmini Mhe. Mwenyekiti, mimi ninakwenda Pemba mara tatu, nne au tano na si mimi peke yake ninakwenda na familia yangu, watu wanne watano na sote tunalipa shilingi elfu elfu.

Aangalia kwa *trip* ni elfu ngapi? Kwa mwezi nitatoa ada hiyo kiasi gani kwa mimi mmoja ukinifanyia hesabu. Kwa hivyo bado ninawatetea wasafiri wa Unguja na Pemba ada hii iondoshwe haina mantiki kabisa, hawa ni watu wanaotembeleana.

Lakini jengine ambalo ninalolifikiria ambalo kidogo ni muhimu, hapa Mhe. Waziri unajua hapana cha kuzungumzia kwa sababu ni ndogo sana, mengi sana yapo sawa sawa. Lakini sasa nimuulize Mhe. Waziri ndani ya bajeti yake aliyokuja nayo kipindi hichi, sisi tumekosa kuelewa mambo mengi kodi ambazo zipo katika muungano na ni nyingi sana, hapa hajaziona na wala hatujaelezewa na wala hakuna taarifa tuliyopewa.

Hawa watu wa *TCRA* ipo kodi pale. Tunataka tuelezwe kiasi gani Zanzibar inapata kwa *TCRA*. Kodi ya *TAA* ipo wapi mbona hatuioni hapa Zanzibar. Mgao wetu ni kiasi gani. Haya ni mambo ya kuweza kuelezwa tuweze kujua ndani ya muungano, sisi muungano huu tunakwenda *very blind*, kama watu vipofu hatujui linalokwenda wala linalorudi, tunavurugwa tu.

Kuna mambo ya ndani fedha ya kule ya muungano hapa hatuisikii. Kwa hivyo hiyo ni moja. Posta na Simu zipo fedha, hatujui chochote na ni muungano. Mamlaka ya Hali ya Hewa hatuoni kitu. Lakini la mwisho ambalo ni la muhimu zaidi ni hili mwenzangu aliloligusia, suala zima la mafuta na gesi asilia.

Hawajabahatika Tanzania Bara kuchimba mafuta lakini gesi wanayo, na wameweza kuichimba. Katika Katiba yetu inasema mafuta na gesi asilia ni mambo ya muungano ingawa sisi tunasema si mambo yaliyokuwa ya muungano, mafuta hayamo, *resources* hazimo, lakini ndani ya Katiba yapo ya Tanzania na ya Zanzibar zinasema mafuta na gesi asilia ni za muungano, lakini kama kweli wao walikuwa *serious* kwamba vitu hivyo ni vya muungano, mbona tokea wao walipochimba gesi miaka hiyo huko Songosongo, zaidi ya miaka minane au zaidi wamechimba Zanzibar haijapata hata shilingi moja.

Miaka yote hiyo gesi inachimbwa na wala hapa Mhe. Waziri wa Fedha hajatwambia kwamba tunapata kiasi fulani katika gesi. Kuna tanzanite, dhahabu, uranium, gold, sisi tuna mafuta yetu tena mengi sana. Lakini ninasema *resources* hazimo katika muungano, na ndio maana wao wasitilie mkazo, waliandika tu tokea kipindi hicho mwaka 1984 imetiwa ndani ya Jamhuri ya Muungano bila ya ridhaa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Waseme watu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kweli mafuta na gesi asilia ilikuwa na maridhiano na Zanzibar. Ililetwa tu kutoka Bara akaambiwa Mhe. Warioba peleka hii Zanzibar itiwe katika Katiba ya Zanzibar na imetiwa katika Katiba ya Zanzibar tangu mwaka 1984 lakini bila ya ridhaa ya Serikali ya Zanzibar.

Leo wanataka mafuta yawe yao, haya mafuta si yao bwana. Hii ni raslimali ya Wazanzibari na yatachimbwa na Wazanzibari wenyewe, hatuna habari nyengine na Bara. Ukitizama kumbukumbu mpaka *archieve* ya Zanzibar, ukiangalia historia ya Zanzibar inasema ni ya nani. Inasema kule kuwa raslimali hii ni ya Wazanzibari na

yatachimbwa na Wazanzibari wenyewe. Tunaambiwa *resources* ni za muungano, nani kasema si wapachika wao tu.

Kwa hivyo kama suala hili lilikuwa ni la halali, kuna tanzanite tangu imeanza kuchimbwa na ni *resource*, gold, mafuta, gesi asilia ni *resources* zinachimbwa Tanzania Bara mpaka leo Zanzibar tumepata gawio gani, hatujapa chochote. Kwa hivyo tunasema kama ikiwa Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango na Maendeleo asiangalie hapa Zanzibar tu, kama huu muungano ni kweli na hizi haki zetu tupewe zote za *resources* na Waziri aje atwambie hapa atueleze, kweli fedha ipo tunapewa lakini hatujakwambieni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tunahitaji kujua gawio letu hapa Zanzibar, kiasi gani Zanzibar inapata angalau aje atupe taarifa hizo, kwa sababu mimi nimeona hii karatasi si kubwa sana na ada zake ni za kawaida, lakini nina-*insist* na kumuomba tena Mhe. Waziri hili suala la Unguja na Pemba aliache. Mhe. Waziri aangalie kwenye *target*.

Kama ipo *target*, watu wanavuna kitu, *given take okay*, hii tunakubaliana lakini hapa ipo wapi *given take* kwa wasafiri wa Unguja, Pemba na Dar es Salaam hakuna kitu. Ni watu wana-*enjoy* tu na *traveling* yao ya baharini.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana na mimi ninaunga mkono. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Abdalla Mohamed Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, magharibi haya na mimi kupata fursa ya kusema machache sana kwa sababu na mswada wenyewe unahesabika kurasa zake.

Kwanza Mhe. Mhe. Mwenyekiti, jioni hapa Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti alikuja na utaratibu, pengine labda ulikuwa umeshapitwa na wakati. Lakini alichokuwa anachotaka kukisisitiza ni kwamba, katika kamati yao walikubaliana na Mhe. Waziri kuwa hii kodi iondoshwe.

Sasa kama ni hivyo basi Mhe. Waziri kama walivyomsifu kweli ni msikivu basi angesikia kilio cha watu, chetu sisi au cha wananchi kwa jumla ni kodi. Mhe. Mwenyekiti, inavyoelekea hivi sasa wengi tuna matumizi ya mitandao, na tunaziingiza katika matumizi yetu. Kila anayekuja hapa anakupa mifano lakini wakati wa kufika zile habari tunajisahau. Mhe. Mwenyekiti, katika nchi ambazo ni *less developed* ulimwenguni na kipato chake ni cha chini ni Zanzibar. Sasa ukitoa mfano kwamba watu wanalipa kodi ni sawa na kila mmoja ana mfumo wake wa kodi.

Kuna za wenzetu Mhe. Mwenyekiti, wanatia kodi katika mishahara yao ili mtu apate kuilipia, na kitakachobakia ndio kinakuwa ni chake. Sisi hatuna uwezo huo lakini la pili ni kwamba, kuna kitu kinaitwa *employment*. Sisi katika nchi yetu bado hatuna uajiri wa uhakika. Ajira zetu ni za kukamata leo na kesho ukaachia.

Kwa maana hiyo wale watu wenye uhakika wa pato fulani hatuna, wananchi wetu ni maskini sana. Sasa tukisema kila siku wao tunawabebeshea mzigo ni tatizo. Naomba vitumike vigezo vyengine na kama Mama Asha hapa amesema kwamba twende katika ulevi au vinywaji, sigara basi twende huko. Kwa nini kila siku tumkamate huyu mtu ambaye uhakika wa kupata hiyo shilingi elfu hana kwa sababu hana ajira rasmi.

Sasa kama munakwenda kwenye mitandao mutaona kweli kwamba wenzetu wanalipa, na ni kweli ulimwengu mzima watu wengi wanaendesha nchi zao kutokana na kulipa kodi. Lakini huyu anayelipa kodi ana ajira rasmi ambayo inamuhakikishia kipato chake. Sasa kile ndio kinachokuwa kwenye *tax*. Sasa mimi sina ajira utani-*tax* vipi. Ina maana utanifanyia *exploitation* tu, kile changu nikipokea uniachie, ile ninayoipata kama ni shilingi elfu moja nimeuza ndizi, usiniambie tena niitoe bandarini, niachie mwenyewe.

Sasa mimi ninamuomba Mhe. Waziri awe msikivu kwamba hichi ni kilio, kodi sisi hatuna pa kuitoa. Kwa maana hiyo hata tukafiliwa tutashindwa kwenda kwenye misiba kwa sababu nikenda ni shilingi elfu na kurudi elfu mbili, nauli ya gari itapanda baada ya kuongezeka kwa mafuta. Itabidi sasa kama ninatoka Micheweni nije Mkoani kupanda gari imeshaongezeka, na nikifika pale unataka shilingi elfu moja, haiwezekani.

Namuomba Mhe. Waziri hili alitazame kwa makini kabisa, wala sio suala la kusema watatoa, ni kweli tutatoa kwa sababu *no other alternatives*, hatuna njia nyengine. Lakini athari zake jee? Unatuumiza sana, ondosha Mhe. Waziri ninakuomba utumie busara katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, nikija kidogo katika mswada wetu hapa katika marekebisho ya sheria ya mafuta. Naomba niisome kidogo sheria hii inasema kwamba, hakuna mtu atakayeruhusiwa kushughulika na biashara ya kuuza, kununua, kuhifadhi. Sasa mimi kidogo nilikuwa ninapata wasi wasi. Ukisema unahifadhi, una maana gani. Kule

bandarini ikifika siku saba labda unaanza kulipa. Sasa jee katika sheria hii itakuwa ni siku ngapi itahesabika huyu mtu kwamba yeye ameshahifadhi hichi kitu chake ili tusije tukakamatana, tukawapa watu njia za kupata mapato kwa njia zisizokuwa za halali basi tungeainisha basi *storage* au kuhifadhi itakuwa ni siku ngapi.

Lakini sheria hii hii pia inasema kwamba *petroleum product*. Sasa *petroleum product* ni mafuta ya taa. Sasa kwetu sisi mafuta ya taa ndio tunayotumia wengine katika kupikia wali huko majumbani. Sasa jee lita fulani ambazo zimeainishwa hapa kwamba mtu akihifadhi lita nne, tano au kumi ndio atakuwa amefanya kosa. Mimi ninahisi tusiwape watu *loop hole* wakaja wakapita. Lazima hii sheria itaje kwamba hapa mtu huyu anatakiwa kama kuhifadhi lita kumi au ishirini.

Lakini pia katika hili tusisahau kuna wenzetu wavuvi. Hawa wavuvi pengine wanaweza wakakaa, upepo umevuma akawa tayari ameshachukua lita zake mia sita za kwenda bahari kuu, lakini upepo umevuma akaamua kukaa juu au huko huko bahari kuu akawa nayo hayo mafuta. Sasa huyu naye pia angetambulika jee mtu huyu achukue kibali kwamba anakwenda bahari kuu, asije akakutikana na lita mia saba kule kwa sababu anataka kukaa baharini mwezi mzima ndio alete vibua vyake huku juu. Naomba hii sheria ingeweka mambo kama haya ili tusije tukatoa njia za rushwa, na tukaja tukawadhulumu watu wengine.

Na sisi vile vile tunaokwenda kuchuma karafuu, tunakuwa mara nyingi sana tunaweka kambi, lakini tukieka kambi tunakwenda *petrol station* tunachukua pipa moja au lita mia tatu kwa ajili ya kurahisisha ule usafiri, tunaweka *storage* kule katika kambi zetu, ili wale vibarua wetu tupate kuwapimia kibatari chake pamoja na karabai yangu mimi tajiri. Sasa haya pia ningependa Mhe. Waziri uyaangalie kwa kina, usije ukanisumbua mimi nipo kambini ninakwenda kuchukua mafuta *station* niweke kwa vibarua wangu kwa sababu mvua inanyesha barabara haipitiki, Sheha akaja akaniambia umeweka mafuta hapa mimi nitakupeleka kituoni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache naunga mkono hoja.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mola wetu mtukufu kwa kutujaalia uhai na uzima tukiwa tunaendelea na kikao chetu hiki cha Baraza la Wawakilishi kujadili mambo mbali mbali yanayohusu maslahi ya Zanzibar na watu wake.

Na ni maslahi hayo tu ndiyo yanayotuleta hapa, na ndiyo yanayotuongoza katika Katiba zetu na sheria zetu si jengine lolote. Na ndio maana Mhe. Mwenyekiti, ukiwa unalo suala lolote linalohusu maslahi binafsi Kanuni zetu zinatutaka utangaze maslahi yako, kwa hivyo kinachotuleta hapa ni maslahi ya Zanzibar na watu wake.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze na mimi vile vile kwa kushirikiana na wenzangu waliompongeza sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kazi kubwa ambayo aliifanya asubuhi ya leo, wakati alipokuwa akijibu hoja mbali mbali za Wajumbe. Amejibu kwa ufasaha, utaalamu wa hali ya juu, wengi tumeridhika kabisa na maelezo ya hoja mbali mbali alizokuwa amezitoa.

Lakini pia nimpongeze kwa uwasilishaji mzuri wa mswada huu ya sheria hii ya fedha, ambayo itakayompa nguvu sasa kwenda kusimamia vyanzo mbali mbali ambavyo amekusudia kuvirekebisha vya mapato katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu kwenye mswada huu, kabla ya kuingia kwenye mswada ningemuomba Mhe. Waziri anisaidie ufafanuzi wa mambo machache. Katika hotuba yake ya bajeti kwenye ukurasa wa 49 hadi 64 ndipo alipotutajia dhamira ya kuja kufanya marekebisho ya sheria mbali mbali, ili kuimarisha mapato kama alivyosema kwenye hotuba yake.

Sasa nilikuwa ninazipitia hapa na kidogo nimechanganyika, kwa sababu kaka yetu yeye ni mjuzi wa fani hii, naomba atusaidie inawezekana labda yametupita, na kwa sababu ya dharura mswada unavyokuja huwa hupati muda mkubwa sana wa kufanya mapitio kwa masuala mengine.

Mhe. Mwenyekiti, ufafanuzi ninaouomba ni kwamba nikizitazama orodha ya sheria ambazo amezitaja katika hotuba yake ya bajeti, ambazo ametangaza dhamira ya kufanya marekebisho. Halafu nikiangalia na sheria ambazo zimo kwenye mswada huu, kuna sheria nyengine sizioni.

Sasa labda atusaidie zimesahaulika au zitakuja baadae katika mwaka huu wa fedha? Na kama zitakuja baadae zitaanza kutumika lini kwa sababu ninavyoelewa mimi marekebisho ya kodi mbali mbali na ushuru, huwa yanafanywa kabla ya tarehe mosi Julai ili yaanze kutumika mara mwaka wa fedha unapoanza. Na ili nimsaidie

ninakusudia kwa sababu akija aweze kutujibu vizuri naomba nimtajie baadhi ya maeneo hayo nilikuwa naomba ufafanuzi wake.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 52 wa kitabu cha bajeti, katika marekebisho ya sheria ya stempu alitutajia dhamira ya kuondosha ushuru wa stempu asilimia mia moja kwa thamani ya mikopo ambayo alisema haiongezi mapato kwa serikali, lakini lengo lake ni kushajihisha uwekezaji kwa wale wakopaji katika taasisi za fedha. Sasa hili sikuliona, inawezekana kama kwa sababu ya uharaka wa huu mswada wenyewe unavyokuja, sikuliona ikiwa lipo naomba atusaidie juu ya hilo limezingatiwa kiasi gani katika marekebisho haya ambayo ameyaleta katika mswada.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 54 kwenye sheria ile ya ushuru wa mafuta ya nishati, kuna mambo mawili. Kuna lile ambalo limo kwenye mswada linalohusu kuchukua hatua za kudhibiti magendo ya mafuta. Lakini lipo jengine ambalo amelitaja kwenye hotuba yake ya kuongeza ushuru wa mafuta kwa shilingi hamsini, sikuliona. Sasa kama limo katika Kanuni naomba pia aje atusaidie ili mswada huu ukae vizuri.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 55 wa hotuba yake alieleza lengo la kufanya marekebisho ya viwango vya leseni ya njia kupitia sheria ya usafiri barabarani. Sasa katika mswada huu pia sikuiona sehemu hiyo. Kwa hivyo nilikuwa naomba nipate maelezo, na hapa vile vile kuna mapato anategemea atayapata, ameyataja katika vifungu mbali mbali.

Lakini jengine vile vile kwenye ukurasa wa 61 wa hotuba yake, alieleza dhamira ya kufanya marekebisho ya sheria ya kazi ili kupanga viwango vipya, kiwango cha chini cha kutolea kodi ya mapato kwa wataalamu wa kigeni, nayo vile vile sikuona hilo limerekebishwa katika sheria hii.

Isitoshe Mhe. Mwenyekiti, katika sheria ile ya usimamizi wa kodi, kurekebisha sheria ya usimamizi wa kodi mwaka 2009 iwapo mwekezaji atakodisha au kuteua kampuni ya kuendesha hoteli yake dhamana ya masuala yote, mapato ya serikali ibaki kwa mmiliki wa hoteli husika. Na hilo vile vile katika sheria hii au mswada huu aliotuletea sikuliona katika mswada.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, liko katika ukurasa wa 64, hili linahusu sheria ya mitaji ya umma, ambapo alitutajia kwamba kuna lengo la kufanya marekebisho ili kuasisi utaratibu wa mashirika ya serikali kulipa gawio kutokana na faida. Pia hapa kuna kiwango cha mapato ambacho amekitaja. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais atakapokuja atusaidie ili tujue kwamba hizi zitashughulikiwaje, kwa sababu katika mswada huu sikuziona.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nje ya sheria vile vile naomba anisaidie kwamba hili litakuwa katika sheria ama vipi. Katika ukurasa wa 58 wa kitabu chake cha hotuba ya bajeti alituambia kwamba kuna lengo la marekebisho ya viwango vya mauzo kwa usajili wa *VAT*, kodi ya ongezeko la thamani. Alituambia amekusudia kuongeza kiwango cha mauzo ambacho mfanyabiashara anatakiwa akifikie ili kusajiliwa kwa *VAT* na akakusudia kukiongeza kutoka shilingi milioni 15 hadi shilingi milioni 30. Sasa nilikuwa najiuliza kwamba hili limo katika sheria au katika kanuni. Ningeomba atusaidie Mhe. Waziri kwa sababu hili pia naona ni muhimu sana katika kushajihisha wafanyabiashara wetu wadogo wadogo ili waweze kukuza biashara zao na pia kujiongezea mapato wao, kuiongezea mapato serikali kwa njia nyengine, lakini pia kuongeza ajira kwa watu mbali mbali. Nilikuwa naomba Mhe. Mwenyekiti, akija Mhe. Waziri anisaidie.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo, nije kwenye mswada kama nilivyosema maeneo mengi tuliyakubali kimsingi, lakini kuna hili suala moja ambalo tumeshalipigia kelele wote, na mimi naomba niongezee sauti yangu katika hili, ni hili linalohusu marekebisho ya sheria ya ada ya bandari kwa kutoza shilingi 1,000/- kwa wasafiri wanaosafiri baina ya Unguja na Pemba na shilingi 2,000/- kwa wanaosafiri baina ya Dar es Salaam na Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ukisoma hotuba ya bajeti,na kwa sababu sheria inayotajwa ni sheria ya ada ya bandari, inakupa picha kwamba hapa kilichokusudiwa ni usafiri wa baharini. Lakini nilipoupitia mswada naona zaidi umelenga kuanzisha kodi inayoitwa ada ya usalama wa uwanja wa ndege na katika Kiingereza ni hivyo hivyo. Sasa hili naomba atuwekee sawa Mhe. Waziri akija. Ikiwa shilingi 1,000/- kwa Uguja na Pemba na shilingi 2,000/- kwa Zanzibar na Tanzania Bara inahusu usafiri wa ndege, mimi naunga mkono mia kwa mia hii kwa sababu wanaotumia usafiri wa ndege ni daraja maalum la watu wetu wanaojulikana watakuwa wanajiweza.

Lakini kama ufahamu wa wajumbe walio wengi nikiwemo na mimi nilipochangia hotuba ya bajeti, kwamba viwango hivi vinakusudia pia kuhusika na usafiri wa baharini, basi na mimi navipinga, namuomba Mhe. Waziri

katika hili atukubalie aviondoshe kama hilo ndio lengo lake. Mimi ninatofautiana kabisa na maelezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Mawaziri asubuhi, kusema kwamba hawa wananchi wa kawaida hawasafiri sana.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wetu wa kawaida wanasafiri sana baina ya Unguja na Pemba. Kuna shughuli nyingi za kijamii zinazopelekea kutokana na mchanganyiko wa watu wetu ulivyo hasa sasa kuliko zamani, usafiri baina ya Unguja na Pemba ni mkubwa sana. Lakini isitoshe kama walivyosema wajumbe wengi Mhe. Mwenyekiti, usafiri baina ya Unguja na Pemba kwa Zanzibar ni kama usafiri wa kutoka Makunduchi kwenda Nungwi ni ndani ya Zanzibar. Sasa tunataka tuwaadhibu wananchi ambao wana mahusiano baina ya visiwa hivi, kwa sababu tu tunatoka katika visiwa tofauti, kwa sababu kuna bahari katikati, je hao wengine hawana bahari katikati. Hili Mhe. Waziri alikubali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimesubiri kidogo baada ya kupata mswada nikaona kwamba humu uliotajwa ni uwanja wa ndege, ada ya usalama wa uwanja wa ndege, kama ni hivyo alivyosema, sina tatizo na yeye. Lakini kama tumekusudia katika usafiri wa baharini. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri, mimi naamini kwa imani yake na yeye pia ni mtoto aliyezaliwa katika nchi hii na wazazi maskini kama sisi wengine anajua tulikotoka na anajua hali za maisha ya wananchi wetu zilivyo. Hilo nilikuwa naomba sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niseme jengine la jumla. Mimi nasema mswada tumeupokea na marekebisho hayo machache tuliomuomba Mhe. Waziri nadhani atatukubalia, akiyafanya basi nadhani atakuwa na utaratibu mzuri wa kuweza kutuendeshea bajeti yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala moja lilizungumzwa na wajumbe wengi hapa, kwamba je hivi kutokana na madeni ya madai lukuki ambayo Zanzibar inaidai Tanganyika, tungekuwa kweli tuna haja ya kuwa na mswada huu leo. Kuna wengine walikuwa wanatuambia hapa, hivi wajumbe wanachangia mswada. Nasema tunachangia mswada ndio. Kwa sababu mswada una sehemu mbili, una maudhui ya mswada na vifungu vya mswada. Vifungu vya mswada tumeshavizungumza, lakini maudhui ya mswada ni mambo kama haya, kwamba je haya yaliyokuwemo humu yalipaswa yaje haya Mhe. Mwenyekiti. Mimi nasema hayakuwa na haja.

Mhe. Mwenyekiti, ukitizama hotuba ya bajeti ya Mhe. Waziri marekebisho ya sheria zote hizi yaliyokuwemo kwenye mswada wa fedha, yatampa shilingi 13.3 bilioni, ndio anazozitafuta katika marekebisho yote hayo Mhe. Mwenyekiti. Lakini kumbe tuna mabilioni ambayo tunawadai kando ya pili ya bahari ambayo yangemfanya pengine hata achilie mbali kutafuta bilioni 13, hata misaada ya wahisani angeisamehe.

Mhe. Mwenyekiti, wamesema wajumbe wenzangu hapa. Zanzibar ilipotaka kukuza uchumi wake, tumefanya maamuzi katika Baraza hili kwamba mafuta na gesi asilia yaondolewe katika masuala ya Muungano. Mpaka sasa hivi tunachezeshwa danadana. Lakini mimi ninamwambia Waheshimiwa Mawaziri, chini ya Makamu wa Pili wa Rais, wasubiri na sisi tuwachezeshe danadana humu ndani, kutokana na ahadi yao waliotupa mwaka jana wakati ukifika. Kwa sababu sisi hatuwezi tena kuvumilia Mhe. Mwenyekiti, katika hili. Lakini hili sio mahala pake.

Kwa hivyo, ninachotaka kusema kwamba wakati wenzetu wametuweka kando katika hili, kwa hivyo bado mpaka leo kwa mujibu wa katiba ya Muungano, mafuta na gesi asilia ni suala la Muungano. Sasa kama hivyo ndivyo, imesemwa humu. Wenzetu wanachimba gesi huu mwaka wa tisa na huko kuna mapato. Sasa kama unasema hayo ni ya Muungano, basi tuanze kufaidika na hayo wenzetu walioanza kuchimba, sisi huku hatujaanza kuchimba mafuta huku na gesi. Hebu Mhe. Waziri akija atuambie, kama sio leo basi siku ya mwisho atakuja kutufanyia hesabu katika wizara yake.

Mhe. Mwenyekiti, kumepatikana kiasi gani katika *procedure* za gesi na kwa utaratibu huo huo wa kiwango unachokilalamikia cha asilimia 4.5, Zanziabar kwa kipindi hiki cha miaka tisa tulipaswa tupate kiasi gani. Juzi Mhe. Mwenyekiti, wametutangazia kuwa wana 10 milioni *cubic fit* za gesi wamevumbua kule katika wanaita Zafarani Mtwara. Sasa si jambo la Muungano, sasa kama wanang'ang'ania basi watupe hiyo faida yetu. Lakini mbali ya hilo Mhe. Mwenyekiti, imesemwa hapa, na mwaka jana mimi ni mmoja kati ya waliohoji, kwamba yako mashirika haya katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Hivi Mhe. Hamad Masoud kashindwa kutudaia haki zetu, au serikali imeshindwa kutusimamia haki zetu hizi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niwaombe kitu kimoja, kama kule kuna majibu ya kuchezeana chezeana, basi waje watuambie humu ndani wasiwafichie aibu hii. Mhe. Mwenyekiti, wametajwa hapa, kuna *TCRA* yaani Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Mamlaka hii ina mapato mengi sana, kwa sababu inatoza kutoka na makampuni yote ya simu, mbali ya mapato mengine, haya ya simu. Mimi sizungumzii *TV* wala redio, nazungumza haya ya simu tu, sote tunajua mapato kiasi gani yanayotokana na matumizi ya simu hasa za mkononi.

Mhe. Mwenyekiti, katika vyanzo viwili vikubwa, na Mhe. Omar Yussuf Mzee anajua alikuwa Naibu Waziri wa Fedha. Sekta mbili kubwa zinazochangia ukuaji wa pato na ukuaji wa uchumi kule ni sekta ya madini na sekta ya mawasiliano, yaani simu za mkononi. Sisi tunapata kiasi gani na makampuni haya yana wateja mpaka Zanzibar huku, mbali ya hilo la Muungano, lakini yana wateja sisi tunachangia katika mapato yale. Sasa ni kiasi gani tulipaswa tupewe.

Mhe. Mwenyekiti, imetajwa nyengine hapa Mamlaka ya Usafiri wa Anga, (*TCAA*) yaani *Tanzania Civil Aviation Authority*, zile ndege zinazoruka na kutua pale katika viwanja vya ndege vinaingiza mapato. Kwa sababu wanasema zinatua upande wao, kwa hivyo zibakie kwao, basi tuondoshe katika mambo ya Muungano. Lakini madamu limebakia katika mambo ya Muungano basi tunachetu pale mbona hatupewi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Shirika la Posta mgao wetu uko wapi. Hili zamani lilikuwa ni Shirika la Posta na Simu likagawanywa, kukawa na Kampuni ya Posta na kuna Kampuni ya Simu. Katika Kampuni ya Simu tunapata kiasi gani, kampuni hii ya simu baadae ilibadilishwa kuwa *TTCL* ikafika kununua hisa katika Celtel, ikatoka Celtel sasa imeuzwa imekuja katika Airtel, kuna mapato humu Mhe. Mwenyekiti. Katika uuzwaji wote huu sisi tumepata kiasi gani.

Haya Mhe. Mwenyekiti, yalikuwa ni mashirika yalikuja baada ya kuvunjika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ambapo Zanzibar ilikuwa ni mwanahisa tangu huko nyuma. Lakini hatupati mapato hayo. Mhe. Mwenyekiti, umetajwa hapa mfuko wa elimu ya juu. Elimu ya juu tunaambiwa ni ya Muungano, kwa nini tuweke kodi ya kuwatoza wananchi wetu kufidia elimu ya juu wakati kuna bajeti ya elimu ya juu katika Serikali ya Muungano, liko wapi fungu la Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, pia tuliwahi kuuliza hapa wakati wa mtikisiko wa uchumi duniani benki kuu ilitoa fedha za ziada ili kusaidia kunusuru uchumi, uliambiwa uchumi wa Jamhuri ya Muungano, haukuambiwa uchumi wa Tanganyika na benki kuu ni chombo cha Muungano, zaidi ya trilion moja zilitolewa; Je, Zanzibar ilipata kiasi gain. Halafu kuna hizi ambazo wamezungumza watu wote Mhe. Mwenyekiti, *payee* kodi hii ambayo inalipwa na wafanyakazi wa taasisi ya Muungano waliokuwepo Zanzibar, hawa nimesema wanatumia huduma zetu hapa. Wanapita katika barabara zilizojengwa na walipa kodi wa Zanzibar, wanatumia maji yanayolipiwa na walipa kodi wa Zanzibar, wanakwenda hospitali wakitibiwa kwa madawa na madaktari waliolipwa mishahara na walipa kodi wa Zanzibar, watoto wao wanasoma skuli zinazolipiwa na walipa kodi wa Zanzibar na kadhalika Mhe. Mwenyekiti.

Sasa sisi tuwahudumie wao, lakini kodi iwanufaishe Watanganyika, tunaambiwa hivi sheria itarekebishwa mwaka huu. Mimi siamini Mhe. Mwenyekiti, wameshazowea hawa. Sasa tuchukulie itarekebishwa, lakini waliuliza wengi hapa, zile za mwaka jana je. Halafu lilitolewa agizo la mmoja kati ya viongozi wakubwa, lakini halitekelezwi, sijui tuseme nini Mhe. Mwenyekiti, kama tukisema hakuna nia njema katika Muungano huu, tutakuwa wabaya sisi, hakuna nia njema Mhe. Mwenyekiti, tusidanganyane.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nimalizie hoja zangu kwa kusema kwamba ukijumlisha haya yote na mengine ambayo hatukuyataja, leo muda hautoshi, lakini tutateremka katika kila wizara hapa. Kuna mapato kama nilivyosema lukuki, mamilioni na mabilioni kama hayafiki basi matrilioni ya fedha, sijaigusa BOT, nimesema tuna asilimia 11.02 tunadai tangu mwaka 1966 ilipoanzishwa hadi tulipoanza kulipwa ni kiasi gani tulichokuwa hatukulipwa sisi.

Kwa hivyo, nasema Mhe. Mwenyekiti, nukta yangu ninayomalizia ni kwamba tungekuwa tumeyasimamia haya, basi mswada huu leo ungekuwa hauna haja. Pengine badala ya kuzungumzia *deficit* tungekuwa tunazungumzia *surplus* leo. Sasa Mhe. Mwenyekiti, ninachosema, mara nyingi huwa wanapotoa maelezo yao kule huwa wanatuambia kwamba wamechoka kutubeba. Mimi nawaambia katika Baraza hili, tena nawaambia wasikie hasa hata sisi kama wametubeba basi tumechoka kubebwa watutuwe. Ikiwa kubebwa ndio huku Mhe. Mwenyekiti, mimi natoa wito hasa kwa ndugu zetu wa damu watutuwe mzigo huu, kwa nini wanaendelea kuubeba.

Sisi Mhe. Mwenyekiti, kote nilikotaja huku, tungekuwa tuna mamlaka zetu tungekuwa tunapata mapato yetu hapa. Wameamua kuyabeba yao watupe sehemu yetu, hawawezi kutupa tumekuwa mzigo kwao, nawaomba sana watutuwe. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri na pia nimpongeze kwa majibu yake mazuri aliyotutolea leo hapa, haijafika hata siku moja kumsikia waziri kutoa majibu kama yale leo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hili nampongeza sana na Mwenyezi Mungu amjaalie awe na uwezo wa kutujibu kama hivi. Palipokuwa panataka kujibiwa vizuri, basi aweze kutujibu kwa vizuri na palipokuwa panataka kujibiwa kwa ufasaha vile vile ajibu kwa ufasaha, hilo ndio tunalomuomba Mhe. Waziri Mwenyezi Mungu akubariki.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nije katika kodi ya nauli. Mimi naungana na wajumbe wenzangu kuhusu kodi na ikiwa sikuzungumza hata kidogo Mhe. Mwenyekiti, sitowatendea wanawake wenzangu haki kuhusu suala hili. Mhe. Mwenyekiti, namwambia Mhe. Waziri aone huruma kwa sababu hili suala ni zito sana, zaidi wa wananchi wa kutoka Pemba, wananchi ambao msimu hadi msimu ndio wananufaika na ndio hupata maendeleo yao. Katika msimu wa karafuu hadi karafuu, ukija msimu wa karafuu utamkuta mwanamke kule yuko imara, lakini ukimalizika tu msimu basi mwanamke yule huwa anapata tabu.

Mhe. Mwenyekiti, tuiangalie hii nauli ambayo ni shilingi 28,000/- mwanamke huyo anatafuta nauli kwa mwaka mzima anataka kuja Unguja haipati, na leo mwanamke huyo anaongezewa mzigo tena wa shilingi 1,000/-. Jamani tuwaoneeni huruma wenzetu, tustaghfiru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri afanye ziara, kwa sababu hili suala sisi tumeshalipata katika kamati, ambapo kuna mahoteli huko mashamba yanayojengwa ambayo baadae hukodishwa wazungu. Mhe. Waziri hebu fanya safari uwatembelee ukaone na uulize hawa ndio wakulipishwa kodi.

Pia Mhe. Mwenyekiti, kuna hawa watu wanaokata vibali vya miti ambao na wao hudai shilingi 3,000/- Mhe. Waziri. Hebu na hawa walipie hiyo kodi, lakini wanawake nauli tu ni tatizo kubwa sana ya kutoka Pemba kuja Unguja. Mtu anatoka Pemba kuja Unguja shilingi 28,000/-, anatoka nyumbani shilingi 5,000/- jumla ni shilingi ngapi hizo Mhe. Waziri, halafu na huku umpe tena mzigo wa shilingi 1,000/- jamani Mhe. Waziri mimi ningeomba upandishe kodi kwenye nyumba za kulala wageni, ambapo mtu anatoka nyumbani kwake hana sababu anakwenda kulala kwenye nyumba hizo za wageni, mpandishie kodi Mhe. Waziri. Lakini sio watu kama hawa wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nakushukuru, ahsante.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia mswada ulio mbele yetu. Kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa majumuisho yake mazuri aliyotuletea mchana. Mhe. Waziri hongera sana.

Vile vile nimpongeze kwa ubunifu wa viwango vya mapato katika utozaji wa kodi. Lakini niseme kabisa kama tunachangia bajeti ya serikali hii niliwahi kusema kwamba kodi ya bandari ni mzito kwa wananchi wetu na kama ni mzigo ningemuomba sana waziri wetu, hiki kitu kinachochangiwa na wengi ajuwe ni maslahi ya wananchi wetu. Hivyo unavyofikiria kwamba shilingi 1,000/- basi hiyo shilingi 1,000/- ni ndogo kwa sisi waheshimiwa tu. Lakini kwa mwananchi wa kawaida ni fedha nyingi mno.

Mhe. Mwenyekiti, mwananchi anafikia hadi kuweza kukusimamisha na akakutoa katika makundi ya watu, akakuambia mheshimiwa tuzungumze na *Wallah* akakuomba shilingi mia tu, sasa mtu wa aina hiyo umfikirie kwamba ana hali ngumu kweli kweli. Siku hiyo iwe bahati mbaya uwe hunayo, kakuomba kiasi kidogo cha fedha uwe huna, utajua utakavyopata machungu kwa wananchi wako.

Kwa hivyo, mimi nasema shilingi 1,000/- yakupandisha kodi ya bandari kutoka Unguja na Pemba ni fedha nyingi sana. Nilizungumza hapa katika kuchangia bajeti ya serikali, unapoiona shilingi 50 inayopandishwa ya mafuta ni ndogo kwa kuitaja tu, lakini kila sehemu ya bidhaa muhimu zitapanda bei. Kwa hivyo, tunamuomba waziri wetu wa fedha hili aliangalie kwa kina.

Mhe. Mwenyekiti, mimi napenda kusema tena kama tungesimamia vizuri mapato yetu yanayotokana na Jamhuri ya Muungano, basi kama wenzangu walivyosema, Mhe. Jussa alivyozungumza tungekuwa hatuna dhiki ya kiasi hiki, mambo yetu yangekuwa muruwa, ingekuwa hakuna tabu hata kidogo, bilioni 18 kuzipata Wazanzibari sio mchezo, tunapiga hatua ya maendeleo ya kutosha kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, mapato yetu kama hatuyapati ndio vile vile tunasema kwamba ni kero zisizomalizika siku hadi siku zinaongezeka, ikiwa ni hivyo basi walioungana hawatokuwa na mwisho mwema wa kuaminiana kabisa. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri kwa kushirikiana na wenzake basi asimamie vizuri mapato yetu haya ya Jamhuri ya Muungano na Wazanzibari wapate kunufaika kwa mapato yao wanayotoa katika nchi yao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki niende mbali, lakini tunamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa basi kodi hii ya bandari aiondowe kabisa, kwa sababu wananchi wetu wana hali mbaya kabisa na asifikirie kwamba hao watu wa kawaida wanasafiri kipindi hadi kipindi, hapana, kila siku wako kwenye meli na tunawashuhudia. Mhe. Mwenyekiti, hebu tizama meli ya Serengeti ikenda Pemba hata ikirudi, hebu nenda pale Malindi uone, siku mbili tatu yuko na siku mbili tatu hayuko. Kwa hivyo, hii ni njia kama ilivyo njia nyengine. Mimi sisemi kama ni bahari, bali ni njia kama ilivyo njia nyengine. Wenzangu wamesema hapa ni kama mtu kutoka Mkokotoni akaja zake mjini, au akatoka mjini akenda zake Makunduchi. Ni sawa sawa ni visiwa viwili hivi vimeungana.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri jambo hili tunaomba ulipe uzito sana na mimi sitaki nichangie mengi. Lakini naongezea kwamba jambo hili tupate fursa ya wananchi wetu kuachiwa huru katika kodi hii. Pamoja na hayo Mhe. Mwenyekiti, nasema naunga mkono mswada huu, lakini kwa marekebisho haya ya kodi, ahsante sana.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia fursa hii ya kuweza kuchangia angalau machache tu, au kukazia yale ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameshayazungumza kwa kina.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri mwenye dhamana hii, kipenzi cha wengi, ana nia njema na wengi tunaamini hivyo. Nia yake ni njema kwa serikali yake na ana nia njema pia kwa Wazanzibari wenzake na katika kufanya haya ni ndani ya jitihada ya mambo kwamba sio mazuri sana kama tulivyoona hali nzima ya uchumi wa nchi yetu. Matatizo bado yapo na yataendelea kuwepo, lakini alihisi yeye na wataalamu wake waendelee kupanga hizi kodi za ndani, kodi za ndani hata kama zitaendelea hivyo zilivyopangwa, kama nidhamu ya matumizi ya udhibiti wa kodi hizo haijakuwepo basi tatizo bado litaendelea kubaki.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti ya mwaka jana, serikali iliwaahidi Wazanzibari kwamba haitokuwa na huruma, haitomuonea haya mtu yeyote yule atakaye kwenda kinyume kwa kufuja ama kutumia au kuiba mali ya umma. Hii kauli ilitoka katika bajeti iliyopita na Wazanzibari waliisikia, bahati nzuri Baraza lako hili tukufu kwa kuyaona na kuyasikia, kwa sababu wajumbe hawa wanatafuta na wakishapata wanayaleta hapa, wakaomba kamati teule iundwe ili kwenda kujiridhisha na yale yanayosemwa huko na kamati imeleta ripoti.

Mhe. Mwenyekiti, ile kauli ya serikali hapa ndipo mahala pake, kwa sababu serikali iliji-*commit* kwamba tutamfukuza yeyote, labda serikali ituambie haikuridhika na ushahidi wa ile kamati. *(Makofi)*

Sasa ndipo hapa Waheshimiwa Wajumbe, tunapoona kuendelea na kujenga kodi nyengine kwa hawa masikini wa Mungu si kuwatendea haki. Kwa hivyo, haki kwanza ni hii ambayo tayari ipo, na Waheshimiwa Wawakilishi wao wameyakuta ambayo hayastahiki kufanywa yamefanywa, na wamekuja kulishtakia Baraza lao hili, kwamba yaliyopo ni haya na serikali imesikia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunaendelea kuchangia na kurekebisha sheria za kodi. Bajeti Kuu ya Serikali tayari imeshapitishwa, lakini serikali bado imebaki kimya. Kwa kweli hapa imani za Waheshimiwa Wajumbe, wananchi juu ya ile kauli ya serikali inaanza kufifia, kwamba serikali inataka kodi kwa wananchi wake na huu ndio utaratibu wa dunia nzima serikali zinaendeshwa na kodi zao, lakini wanaozichezea kodi za wananchi serikali huwa haitizami mtu usoni. *(Makofi)*

Nadhani umefika wakati serikali hebu ituoneshe kwamba inatembea kwenye ile kauli yake kwa ajili ya kuwapa imani wananchi, kwa sababu kauli ya serikali ilikuwa nzito, wananchi bado wana imani na serikali na wala wasilazimishwe kupoteza imani.

Mhe. Mwenyekiti, swahiba wangu kuna kodi ambazo nafikiri zitasaidia zaidi, basi ni vyema tukaondoa ile kodi ya bandari. Mhe. Mwenyekiti, tunavyo visiwa vyetu vidogo na wageni wanaokuja huwa wanakwenda kutembea. Taarifa tulizonazo sisi ni kwamba hakuna kodi ya serikali pale, yaani hata wale wanaopanda *vi-boti* pale Mjini, Funguni au Malindi kwa ajili ya kwenda Changuu na kwengineko hawalipi kodi. *(Makofi)*

Sasa utakapowaacha wageni hawa waliokuja kutembea ndani ya nchi hii, ukamwambia biti Bakari anotoka Kwamtipura na wajukuu wake watano wanakwenda likizo skuli imefungwa akalipe shilingi 1,000/= kwa kila kichwa pale, na anakwenda kwao kupumzika, ametoka Kwamtipura kwa mguu nauli ya daladala mtihani. Kwa hivyo, unaposema hii 1,000/= labda mwaka mara mbili ni fedha ndogo si sahihi kwa biti Bakari, kwa bwana Kombo pia si sahihi, kwa Mheshimiwa humu ni sahihi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana swahiba wangu mpenzi, kwa sababu yeye ana sifa kwanza ya kusikia, pia ni muelewa basi na hili alisikie, kwani hichi ni kilio cha Wazanzibari. *(Makofi)*

Kwa kweli hivi sasa wanatulaani kwa hili, ili na sisi waone kwamba tuna imani nao, kwamba tunawatetea haki zao za msingi ndani ya nchi yao, japo tunaambiwa kwamba hatutetei huko kwengine. Lakini *mambo kunga mvungu mkeka*, waliotangulia wanajua zaidi kuliko mimi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme hebu tujitahidi kwanza tuzuie hizi kodi tunazozipata, nidhamu ya matumizi idumishwe. Mhe. Waziri bado tunalo tatizo kubwa mno la matumzi mabaya ya fedha za serikali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, bado mtindo wa mtu kujisikia mambo si mazuri akaunda safari tu, Pemba wiki moja anaingia jioni kwa ndege asubuhi na kurudi tena hapa na posho ni la wiki. Kwa hivyo, haya si madogo kwa nchi ambayo uchumi ni hali mbaya kama hivi ni makubwa, posho ile inalipwa na huyu biti Bakari. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tumekwama wapi tunazungumza shilingi bilioni 18, fedha za *East Africa Currency Board*, mgao wa *BOT*, gesi asilia yote ndiyo hayo tumekwama jamani. Mhe. Mwenyekiti, juzi nilisema na leo nitarudia tumekwama na hatutatuki kamwe Wabunge wetu wote pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi wetu hapa, sote tuimbe nyimbo moja kutaka hizo fedha tulipwe hazilipwi. *(Makofi)*

Hivi tukae tujiulize miaka yote hii hata robo kwa nini wasitupe, kweli wanayo nia ya kutupa hawa. Kwa mfano, *East Africa Currency Board* pamoja na hiyo Afrika ya Mashariki tokea kuvunjika hadi leo ni miaka mingapi? *BOT* 11.5 imetolewa na waliotutawala na hawa Wazanzibari chao hiki. Mhe. Mwenyekiti, maneno ya kebehi *BOT* walituambia, yaani mpaka mkubali kuwa na uchumi mmoja na wala hakuna chumi mbili ndani ya nchi moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wajumbe, nasema haya yote yametukuta, kwa sababu wenzetu imani yao ya miaka mingi tunakwenda kutembea kwenye barabara moja, yaani ile *two to one*, ndipo wenzetu walipo hapo.

Waheshimiwa Wajumbe kama mlisahau kuna mmoja alisema kama si leo ni kesho, kama si kesho ni kesho kutwa, kama si kesho kutwa ni mtondogoo mbili kwenda moja, sasa mbili kwenda moja hapakuwa na haja ya kuyafanya haya na hapa ndipo tulipokwama. Kwa hivyo, tusiwalaumu na kuwapakazia majina mabaya vijana wetu bure, na wao waki-*reflect* kwetu kwamba watupe majina mabaya kwa tuliyoyafanya sisi wazee wao tutatoa ruhusa hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa zama zetu ilikuwa ni sahihi yale tuliyoyafanya, na matunda ni haya ya sasa. Hivyo, kwa zama za leo vijana wetu ni mabaya mno kwao, kwa hiyo tukubali. Mhe. Mwenyekiti, wanasema waachiwe wapumue ni haki yao, kwa sababu tulivyokuwa tukenda sisi na leo huwezi kuwalazimisha wende vile haviwi. *(Makofi)*

Mhe. Waziri hapa ametuambia asubuhi kwamba tutakuja gharamika gharama ambayo hatuna kama vile kuwapeleka Israel, India watoto vigongo havinyooki, *operation* wa viuno hawawezi kuandika juu ya meza kwa kujipinda, tunawapa *laptop* lakini anakaa chini. Mhe. Mwenyekiti, Maalim Haroun Ali Suleiman amefanya kazi kubwa amezileta si haba, lakini ziko juu ya mchanga ardhini na meza haipo. *(Makofi)*

Sasa tunataka deski unamwambia mama yake biti Bakari eti aongeze kodi na kupita pale aende kwao, kwa ajili ya kuchuma karafuu na tupate meza ya mjukuu, hapana hivyo isipokuwa tuwaunge mkono hawa vijana wetu ambao wanataka kupumua si watoto wetu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nasema tuwaunge mkono yale madai yao halali, ili wapate kupumua na wasitukere, jambo la msingi ni kuwasimamia na wasilete fujo, kwa sababu mambo hayendi kwa kwara mambo mazuri. Waheshimiwa Wajumbe wengi humu wanafahamu akiwemo *Professor* Mhe. Ali Mzee Ali anafahamu vyema kwamba mambo hayendi kwa kwara. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mazungumzo, maelewano pamoja na makubaliano tunafika mahala pema, basi tuyasimamie hivyo, yaani vijana tuwasimamie waende mwendo huo na wala tusiwape majina yasiyofaa, kwa sababu wanataka wapumue hapana, kwani kupumua ni haki ya kila mtu. *(Makofi)*

Sasa kwa nini tunataka mazuri tupate kodi kubwa, kwa ajili ya kuendesha mambo yetu, leo wao tumeshindwa kuwapa ajira kumudu mambo yao na wanahisi matatizo ni haya, na tunayazungumza hapa kwamba fedha hatuna na imekwama wapi ndani ya Jamhuri ya Muungano. Kwa hivyo, wakisema tuachiwe tupumue ndipo wanapopaona hapo na hii ni zama yao, kwa sababu zama zetu sisi tukubali kwamba zimepita.

Mhe. Mwenyekiti, wakati wetu sisi tulikuwa tunakwenda “Mwalimu kasema tuimarishe chama”, yaani asubuhi sisi ndio tulikuwa *Youth League* tunaandamana kuunga mkono na hizo ndizo zama zetu hizo, akina mama kesho na wao wanaitikia wanasemaje Mwalimu huyo “Bega kwa bega tusirudi nyuma” na hiyo ndio zama yetu. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa kweli kijana huyu wa *digital* ukimwambia kasema Mwenyekiti wa Wenyeviti hakubali, kwa sababu tumetanua demokrasi. Kwa hivyo, maana ya kutanua demokrasi ni kupata uwanja mpana. Mhe. Mwenyekiti, haki yao wadai na haki inadaiwa haiombwi. *(Makofi)*

Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipatia fursa ya kutia nyalio katika hoja iliopo mbele yetu, na mimi sina mengi isipokuwa ni machache sana.

Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri sana, mtoto wangu kwa kuleta huu mswada ambao anataka tumruhusu aweze kufanya mambo ya kutoza kodi. Mswada huu wa Kutoza Kodi una mambo yaliomo katika mswada huu naomba kidogo Mhe. Mwenyekiti uniruhusu ninukuu “Sheria za Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato”.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimwambie mtoto wangu hapa Mhe. Waziri wa Fedha kwamba, kila mwenye kukata kitambaa, basi ni fundi wa kushona, yaani huwezi kukata kitambaa kama si fundi wa kushona. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niliwahi kusema hapa kwamba nilinukuu maneno ya bwana mmoja anayeitwa Kim-Il-Sung kwamba “*The worst slavery in the world is slavery of fear”* na hii mnaweza kuiona kwenye kitabu cha *Freedom and Unity* cha bwana Kim-Il-Sung *(Makofi)*

Kwa kweli hakuna utumwa mbaya sana duniani kama utumwa wa hofu, kwa sababu kuna utumwa wa aina mbili Mhe. Mwenyekiti. Kwanza kuna utumwa wa bwana na mtwana, na ambao huu umeondoka zamani wala hauna tatizo sana wa bwana na mtwana, kwa sababu bwana lazima mtwana wake atamshibisha ndio amtume, lakini huu wa hofu ni hatari zaidi, na ndipo aliposema bwana Kim-Il-Sung kwamba “*The most worst slavery is slavery of fear”. (Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna jambo ambalo Wazanzibari hatuna tatizo, nalo kwa wakati huu ni mapato. Lakini tumekuwa watumwa wa hofu, kwa sababu ya kuwahofia ndugu zetu wa damu, yaani Watanganyika. Kwa mfano, hivi sasa kuna Gesi ya Songosongo na wala hatujapata hata siku moja sisi hiyo asilimia 4, pia kuna zile fedha za rada hatujalipwa, samaki wa Magufuli halikadhalika kuna fedha nyingi tu hatujalipwa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, leo sisi tunakuwa *Muumiani* twende tukamtoe damu mpaka mwananchi wa chini, hili haliwezekani, kwa sababu hivi tunavyozungumza ni kwamba tatizo la nchi yetu ni udhibiti. Kwa mfano, tuangalie hii Kodi ya Ufundi *Study* (*Skilled Development Levy*) imekwama kwa sababu hatukuidhibiti vizuri na vyuo vinasuasua hivi sasa. Kwa hivyo, nadhani ni vyema tudhibiti hizi kodi ambazo tumezianzisha nyuma. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante sana Inshaallah kesho tukijaaliwa utaendelea tena. Baada ya kumaliza dakika zako 10 atafuata Mhe. Mwanasheria Mkuu na baadaye Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo atafanya majumuisho.

Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuruni sana kwa namna tulivyoshirikiana hadi tukafikia hapa kwa leo hii. Kwa hivyo, nachukua fursa hii kuahirisha Baraza hili hadi kesho tarehe 22/06/2012 saa 3:00 asubuhi. Ahsanteni sana.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 22/06/2012 saa 3:00 asubuhi)